# Nipashe

Jumatatu Julai 9, 2018 • Tanzania 1,000/- Kenya 100/-

MWANGA WA JAMII

ISSN 0856 • Na. 0579623

www.ippmedia.com

twitter.com/nipashetz

www.facebook.com/nipashetz

www.instagram.com/theguardian_newspaper

LIKE & FOLLOW US




## Wasiosomeka mfumo TRA wasamehewa kulipa faini

UKURASA 3




UKURASA 13

# Mwarobaini ajali za bodaboda huu hapa

UKURASA 2




Rais Dk. John Magufuli akikata utepe na Makamu wa Rais, Samia Suluhu Hassan, Waziri Mkuu Kassim Majaliwa pamoja na viongozi wengine baada ya kuwasili kwa ndege mpya aina ya Boeng 787-8 Dreamliner. **PICHA: IKULU**

## Ahueni kwa wenye viwanda

UKURASA 2

## JPM ataja sababu 3 kufufua ATCL

UKURASA 2




# JPM ataja sababu tatu kufufua ATCL

**Na Gwamaka Alipipi**

WAKATI ndege mpya aina ya Boeing 787-8 Dreamliner ikiwasili nchini jana, Rais John Magufuli ametaja sababu tatu za kulifufua Shirika la Ndege Tanzania (ATCL).

Ndege hiyo ambayo ni ya nne kati ya saba ambazo serikali imeshazinunua iliwasili katika Uwanja wa Ndege wa Kimataifa wa Julius Nyerere (JNIA) jana majira ya saa 11:15 jioni ikitokea Marekani, na kupokelewa na Rais Magufuli.

Akizungumza kabla ya kuipokea ndege hiyo, Rais Magufuli alisema endapo kutakuwapo na watu ambao hawajafurahia ujio wa ndege hiyo, "watapata tabu sana".

Rais Magufuli alitaja sababu ya kwanza kuwa ni kujenga heshima na kulinda heshima ya taifa.

Alisema Tanzania ni taifa kubwa, hivyo ilikuwa ni aibu kutokuwa na ndege.

"Watu milioni 50 na ushee, nchi kubwa yenye kila kitu, ina dhahabu, tanzanite, wanyama, hakuna hata ndege, ilikuwa ni aibu, na ndiyo maana tukaamua kuitoa hii aibu," alisema Rais Magufuli.

Rais Magufuli alitaja sababu ya pili ni kuimarisha na kuboresha huduma za anga nchini, akisema katika ulimwengu wa sasa hakuna watu wasiohitaji huduma ya ndege.

Alisema bila ya usafiri wa ndege wa uhakika wafanyabiashara wa maua walioko katika mikoa ya Mbeya, Njombe, Arusha, watashindwa kusafirisha bidhaa zao.

Alisema bila uwapo wa ndege wavuvi walioko katika Ziwa

INAENDELEA UK. 8

PUMZIKA



Baadhi ya wananchi waliohudhuria Maonyesho ya Biashara ya 42 ya Kimataifa Dar es Salaam, wakiwa wamepumzika huku wakila 'ice cream'. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Dawa ajali za bodaboda yaja

**Na Mary Geofrey**

SERIKALI imesema itafunga matela kwenye bodaboda zote nchini lengo likiwa ni kupunguza na kumaliza ajali za barabarani zinazosababishwa na vyombo hivyo.

Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi, Kangi Lugola, alitangaza mpango huo wa serikali, alipotembelea banda la Jeshi la Polisi katika Maonyesho ya 42 ya Kimataifa ya Biashara yanayoendelea jijini Dar es Salaam.

Lugola alisema matela hayo yatafungwa nyuma ya pikipiki na yatawezesha kupakiza abiria hadi wanne kwa wakati mmoja.

Alisema lengo la serikali ni kupunguza mwendokasi kwa pikipiki hizo na kusimamia usalama wa abiria wanaozipata.

"Serikali inakuja na mpango madhubuti wa kupunguza kama si kumaliza kabisa ajali za barabarani zinazo sababishwa na madereva pikipiki ambao wanapenya penya. Dawa yenu inachemka bodaboda, tutawafungia matela ya kubebea abiria na nyie mkae kwenye foleni kama bajaji na magari mengine," alisema.

Lugola alisema pikipiki zote za abiria zitafungwa hayo matela isipokuwa za watu binafsi.

Alisema "Tukishafunga hayo matela naamini hamtakimbia zile mbio zenu za kuchupa (kupenya) zinazosababisha ajali na mtatulia barabarani."

Lugola akijibu swali lililoulizwa na mmoja wa wananchi aliyetaka kufahamu sababu za askari polisi kukamata pikipiki zikiwa kwenye mwendo mkali, alisema ni kutokana na madereva na nao kutokujali usalama wao.

"Dereva umeambiwa uvae kofia ngumu, wewe huvai na unakatisha katikati ya jiji na tena kwa kuchupa na askari wetu nao wamefundishwa mbinu za kukabiliana na watu kama nyie ndio sababu nao wanawarukia," alisema Lugola.

Alisema madereva wanatakiwa kuzingatia Sheria za Usalama Barabarani na kubwa jeshi hilo halitawafumbia macho wanaozikiuka.

Aidha, Lugola alisema pia jeshi hilo litaanzisha utaratibu wa kuzihakiki leseni za madereva, ili kujiridhisha kama wanakidhi vigezo.

Lugola alisema operesheni hiyo itaenda sambamba na kushusha madaraja ya leseni kwa lengo la kupunguza ajali za barabarani.

"Tutaanza uhakiki wa leseni za madereva upya, ili tufahamu kama kweli wana vigezo vinavyotakiwa, na ikibainika dereva hajui chochote kuhusu sheria za usalama barabarani tutawashusha madaraja au kuwanyang'anya leseni," alisema Lugola.

Kwa mujibu wa taarifa iliyotolewa hivi karibuni na Kaimu Mkurugenzi Mtendaji wa Taasisi ya Mifupa (MOI), Dk. Samuel Swai, majeruhi wa pikipiki 20 kila siku wanafikishwa katika taasisi hiyo.

Aidha, wagonjwa 25 kila siku wanafanyiwa operesheni kila siku kutokana na majeraha mbalimbali ya ajali.

Maeneo yanayotajwa kuathiriwa zaidi ni mifupa mikubwa, migongo, kichwa na nyonga hali inayosababisha kupoteza viungo, kupooza na ulemavu wa kudumu.

# Wenye viwanda wapata nafuu tozo

**Na Gwamaka Alipipi**

SERIKALI imefuta tozo mbili zilizokuwa zinatozwa na Wakala wa Usalama Mahala pa Kazi(Osha) kwa wenye viwanda, ili kuvutia wawekezaji na kufikia malengo ya Tanzania ya Viwanda ifikapo mwaka 2025.

Waziri wa Nchi Ofisi ya Waziri Mkuu (Sera, Bunge, Kazi, Ajira, Vijana na Watu wenye Ulemavu), Jenista Mhagama aliyasema hayo alipotembelea banda la Osha kwenye maonyesho ya 42 ya Kimataifa ya Biashara kwenye viwanja vya Mwalimu Julius Nyerere.

Mhagama alizitaja tozo hizo kuwa ni, Sh.500,000 kwa ajili vifaa vya zimamoto, ambavyo mwekezaji alikuwa anatozwa mara mbili.

"Mwekezaji alikuwa anatozwa na Osha, pia alikuwa anatozwa na Jeshi la Zimamoto na Uokoaji, sasa hivi tumeondoa tozo hiyo," alisema Mhagama.

Waziri Mhagama alitaja tozo nyingine kuwa ni gharama ya cheti ambayo walikuwa wanamtoza mwekezaji kiasi cha fedha kwa ajili ya kupata cheti baada ya kukaguliwa.

Alisema kwa sasa tozo hiyo imeondolewa, lakini ukaguzi utaendelea kufanyika, na cheti kitatolewa bila ya gharama yoyote.

Aliongeza kuwa uwapo wa Osha ndiyo ulinzi pekee wa wafanyakazi sehemu za kazi, na kuwataka waajiri kutoa ushirikiano pindi maofisa wa Osha wanapofika katika kampuni zao kufanya ukaguzi.

"Osha kazi yao ni udhibiti mahali pa kazi, kazi yao ni kuhakikisha wafanyakazi katika mazingira salama, bila ya hawa afya zetu zipo hatarini," alisema Mhagama.

Kwa upande wake, Kaimu Mtendaji Mkuu wa Osha, Khadija Mwenda, alisema mbali na kuhakikisha usalama wa wafanyakazi unakuwapo sehemu za kazi, Osha wamekuwa wakitoa elimu kwa kampuni kuhusu masuala mbalimbali.

Alisema wamekuwa wakitoa elimu ya namna ya kuzuia upotevu wa umeme, kwa kuwapeleka wataalamu wa umeme kufanya marekebisho kwenye viwanda.

"Hatuna sheria inayolazimisha kampuni kuwa na ofisa usalama na afya, lakini kuna sheria inayotaka kampuni kuwa na kamati za usalama na afya mahali pa kazi," alisema Mwenda.

Alisema hata sheria iliyopo inakumbana na changamoto kwa sababu waajiri wengi hawataki kuitekeleza kwa kuogopa kuongeza gharama.

Alisema Osha wamekuwa wakihakikisha mazingira bora ya kufanyia kazi yanakuwapo katika kampuni husika, kwa wafanyakazi kuvaa vifaa maalum vya kujikinga na viatarishi.

HABARI KITAIFA

# Kanisa lafanya maombi ya ajali

**Na Elizabeth Zaya**

KANISA la Mlima wa Moto la jijini Dar es Salaam, jana lilifanya maombi maalum kwa ajili ya kuliombea taifa liepushwe na ajali zinazoendelea katika maeneo mbalimbali nchini.

Maombi hayo yaliongozwa na Mchungaji Mkuu wa Kanisa hilo, Dk. Getrude Rwakatare.

Dk. Rwakatare alisema kuna haja ya kuungana kuendelea kuliombea taifa dhidi ya hila za shetani ambaye anapitia ajali kupoteza roho za Watanzania.

"Tusinyamaze kimya, wakati serikali inafanya jitihada zake na sisi Watanzania tuiunge mkono, kwa pamoja kuendelea kufanya maombi, Mungu atatusikia na ataepusha hizi ajali na pia atazidi kulinda nchi yetu katika mambo mbalimbali," alisema Dk. Rwakatare na kuongeza:

"Maombi ndio silaha ya kila jambo, na Mungu wetu ni mwaminifu, kila tunaloomba lazima atende, hakuna linalomshinda."

Pia Dk. Rwakatare alimpongeza Rais John Magufuli kwa jitihada anazozichukua katika kupambana na ajali.

Alisema Rais Magufuli ni zawadi ambayo Mungu ameitoa kwa Watanzania, hivyo wanapaswa kumuunga mkono katika kila jambo analofanya pamoja na kuendelea kumuombea ili maono yake aliyoanayo katika nchi yazidi kutimia.

"Tumeshuhudia mambo mengi makubwa na mazuri ambayo Rais wetu ameyafanya kwa nchi yetu katika kipindi hiki tangu aingie madarakani, tuendelee kumuombea ili azidi kuyatimiza yale yote ambayo anatamani kufanyanya kwa ajili ya manufaa ya nchi," alisema Dk. Rwakatare.

Kanisa la Mlima wa Moto lililopo Mikocheni, lilifanya maombi hayo maalum ya kuliombea taifa liepushwe na ajali ikiwa ni siku moja baada ya viongozi wa dini mkoani Mbeya kufanya maombi ya namna hiyo.

Viongozi hao wa Mbeya walifanya maombi kuombea mkoa wao ambao hivi karibuni ulipatwa na ajali mfululizo zilizosababisha vifo na majeruhi.

PIMA



Mfanyakazi wa kampuni ya Group SIX akichukua vipimo katika barabara ya The Guardian iliyopo Mikocheni Mtaa wa Viwanda jijini Dar es Salaam tayari kwa ujenzi ambao utachukua miezi mitatu hadi kukamilika. **PICHA: SELEMANI MPOCHI**

# Tuhuma zilivyoondoa askari wote hifadhini

**Na Mwandishi Maalum**

WAZIRI wa Maliasili na Utalii, Dk. Hamisi Kigwangalla, amewasimamisha kazi maofisa na askari wanyamapori wote 27 wa Mamlaka ya Usimamizi wa Wanyamapori Tanzania (TAWA) katika Pori la Akiba Uwanda, mkoani Rukwa kwa tuhuma za kuomba na kupokea rushwa.

Miongoni mwa waliosimamishwa ni Kaimu Meneja, Lackson Mwamezi kwa kushindwa kusimamia vizuri pori hilo na kutuhumiwa kujihusisha na vitendo vya kuomba na kupokea rushwa.

Uamuzi huo umefanyika siku tatu tangu alipomsimamisha kazi Meneja wa Pori hilo, Mark Chuwa, kwa tuhuma kama hizo pamoja na tuhuma nyingine ikiwamo kushindwa kuondoa ng'ombe zaidi ya 12,000 ambao wamedaiwa kuwapo ndani ya pori hilo.

Pori la Akiba Uwanda lipo katika bonde la ziwa Rukwa katika Wilaya ya Sumbawanga mkoani Rukwa na linasimamiwa na TAWA.

Dk. Kigwangalla alifanya uamuzi huo jana alipotembelea pori hilo sambamba na kufanya mkutano wa hadhara uliofanyika katika Kijiji cha Kilyamatundu, ambapo alipokea taarifa ya malalamiko kuhusu askari hao kupokea rushwa kutoka kwa watu wenye uwezo na kuwaruhusu kuchunga hifadhini huku wakiwanyanyasa maskini kwa kukamata mifugo yao.

Alifafanua tuhuma hizo kuwa ni pamoja na kudaiwa kujihusisha na vitendo vya kuomba na kupokea rushwa kutoka kwa wavuvi wanaovua samaki Ziwa Rukwa kwa kuwatozwa kila mmoja Sh. 100,000 kwa mwezi na kuruhusu mifugo kuchungwa hifadhini kwa kipindi cha miezi mitatu ambapo kila mfugaji hutozwa kati ya Shilingi milioni sita hadi saba.

Dk. Kigwangalla pia ameiagiza Taasisi ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa (Takukuru), kuchunguza mali na tuhuma za rushwa walizopewa askari wote wa pori hilo wakiwamo watano walioutuhumiwa kwenye mkutano wa hadhara kwa kuomba rushwa ya shilingi milioni sita kwa Shija Imeli, ili wamruhusu kulisha mifugo yake hifadhini kwa muda wa miezi mitano.

Shija alisema Januari 5, mwaka huu akiwa nyumbani kwake na Shemen Kuzenza, askari watano wa pori hilo walifika kwake na kumtishia kuwa endapo atalisha mifugo hifadhini wangemkamata huku wakijua hana sehemu nyingine ya malisho, hivyo wakamtaka kutoa rushwa ya shilingi milioni sita, ili aruhusiwe kulisha mifugo yake hifadhini kwa muda wa miezi mitano.

Alisema walifanikiwa kuwapa askari hao jumla ya shilingi milioni 5.8 kwa nyakati tofauti na walipo shindwa kumalizia Sh. 200,000 zilizobakia askari hao walikamata mifugo yao nje ya eneo la hifadhi.

Kufuatia malalamiko na tuhuma hizo, Dk. Kigwangalla aliitisha gwaride la utambuzi lililohusisha askari wa Jeshi la Wananchi wa Tanzania (JWTZ), askari wa usalama barabarani na maofisa na askari wanyamapori wa TAWA waliokuwapo katika mkutano huo wa hadhara.

Shija na mwenzake Kusenza

INAENDELEA UK. 8

# Wasiosomeka mfumo TRA wasamehewa kulipa faini

**Na Mary Geofrey**

NAIBU Waziri wa Fedha na Mipango, Ashatu Kijaji, ameiagiza Mamlaka ya Mapato Tanzania (TRA), kutowatoza faini walipa kodi waliolipa kwa hiari mwaka jana kutokana na kutoingizwa kwenye mfumo wa mamlaka hiyo.

Kijaji alisema hayo alipotembelea banda la TRA lililoko katika Maonyesho ya 42 ya Kimataifa ya Biashara, yanayoendelea viwanja vya Mwalimu Nyerere, Barabara ya Kilwa, jijini Dar es Salaam.

Alisema amepokea malalamiko kutoka kwa wananchi kuwa, walilipa kodi kwa hiari mwaka jana, mfumo haukusoma kama walelipa.

"Nimepokea malalamiko kutoka kwa walipa kodi kwa hiari mwaka jana, wanalalamikia kutakiwa kulipa kodi nyingine kutokana na mfumo kutosoma kuwa wamelipa," alisema Kijaji.

Kijaji aliitaka TRA ifutilie na kufanyia kazi malalamiko hayo na kila aliyelipa kodi asitakiwe kulipa faini.

"Watanzania bado wanahitaji elimu zaidi ya kodi, kwa kuwa ni jukumu la TRA kuhakikisha inawafikia walio wengi pamoja na wale waishio mbali zaidi, hivyo malalamiko haya yafanyiwe kazi," alisema Kijaji.

Aidha, aliwataka wafanyabiashara kununua karatasi za risiti kwa wasambazaji waliopitishwa na kuthibitishwa na serikali kwa kuwa karatasi hizo zilizothibitishwa hufutika baada ya miaka mitano.

Alisema kumekuwapo na malalamiko ya risiti zinazofutika ndani ya muda mfupi na kusema kuwa wafanyabiashara wanatakiwa kuzingatia maagizo ya serikali.

"Niwatahadharishe tu vishoka wanao husika kusambaza karatasi za risiti zisizo na viwango, fanyeni kazi kwa kuzingatia misingi ya maadili na uadilifu, wanaharibu utaratibu uliowekwa na serikali," alisema.

MAHOJIANO MAALUM

# Vigingi vitatu vinavyo kwamisha elimu Tanzania



Mbunge wa Vunjo (NCCR-Mageuzi), James Mbatia.

**Na Sanula Athanas,** DODOMA

JAMES Mbatia ni Mbunge wa Vunjo (NCCR-Mageuzi) ambaye kwa muda mrefu amekuwa akilalamikia bungeni ubovu wa mfumo wa elimu nchini, akieleza kuwa kuna haja ya kuufumua kwa maslahi mapana ya taifa.

Kwa kuzingatia uzito wa hoja yake hiyo inayopigiwa upatu na marais wastaafu Benjamin Mkapa na Dk. Jakaya Kikwete, ambao wameshaweka wazi kuwa kunahitajika mjadala wa kitaifa kuhusu mfumo wa elimu nchini, Nipashe ilimtafuta Mbatia na kufanya naye mahojiano.

Katika mahojiano hayo yaliyofanyika bungeni mjini Dodoma wiki iliyopita, mbali na mambo mengine, kiongozi huyo wa NCCR-Mageuzi alibainisha changamoto tatu ambazo anaona zinaathiri sekta ya elimu nchini.

Mbatia (54), alisema miongoni mwa changamoto hizo ni mfumo wenyewe wa elimu nchini kutokuwa endelevu na kutoboreshwa kwa maslahi ya walimu.

Ifuatayo ni sehemu ya mahojiano ya Nipashe na mtaalamu huyo wa masuala ya mazingira:

**SWALI: Kasoro tatu kubwa katika utoaji wa elimu nchini ni zipi kwa mtazamo wako?**

**MBATIA:** Mtazamo ambao nimeufanyia utafiti. Changamoto kubwa kwenye mfumo wetu wa elimu nchini ni kwanza hatuna mfumo wa elimu ambao ni endelevu.

Yaani, tunapaswa kuwa na elimu ambayo mfumo wake unakubaliwa na wote. Siyo waziri kuagiza. Mfano, wakati wa serikali ya awamu ya nne, Dk. Shukuru Kawambwa akiwa Waziri wa Elimu, aliagiza mitihani isahihishwe kwa mfumo wa GPA. Suala hilo likaletwa bungeni wabunge wakashangilia.

Waziri huyu amekuja amerudi kwenye Divisions wameshangilia tena. Kwa hiyo, unajikuta elimu ya Tanzania inategemea ni nani aliyepo pale na anataka kufikiria nini. Na huwezi kuendesha jamii kwa msingi huu.

Kwa hiyo, tuna tatizo kubwa la kimfumo. Na hili tatizo la mfumo ndiyo linazaa matokeo mengine yote, Ukiangalia walimu wetu wako kwenye hali gani. Wako katika hali mbaya na naona kama kuna mgomo baridi.

**Kwa hiyo, tuna tatizo kubwa la kimfumo. Na hili tatizo la mfumo ndiyo linazaa matokeo mengine yote, Ukiangalia walimu wetu wako kwenye hali gani. Wako katika hali mbaya na naona kama kuna mgomo baridi.**

Maslahi ya walimu wetu yako namna gani? Wanalipwa namna gani? Wanaishi namna gani? Wanaheshimika katika jamii? Mwalimu ndiyo sekta kuu ya uzalishaji kuliko sekta nyingine yoyote ile. Kwa hiyo, ni lazima kuangalia yale maslahi yao. Walimu hawa kutowatenda haki kunasababisha elimu yetu kuyumba.

La tatu, ni miundombinu yote sasa katika elimu; masuala ya vitabu, masuala ya majengo, miundo ya kufundishia, masuala yote yale yanayotakiwa yatumike kumfanya mwanadamu aweze kuelimika vizuri.

**SWALI: Ikitokea ukawa Waziri wa Elimu, kipi cha kwanza utakachofanya ukiacha kuviondoa vitabu ambavyo umekuwa ukivipigia kelele bungeni?**

**MBATIA:** Suala la elimu ni la kimfumo na elimu ni mapigo ya moyo ya nchi yoyote ile. Na ukitaka kuua taifa lolote, anza kuua mifumo yake ya elimu inayolinda utu wa mwanadamu. Hapa kuna mfumo wa elimu ulio rasmi na mfumo wa elimu usio rasmi.

Elimu inayofaa ulimwenguni leo, na kama ningekuwa na mamlaka, ningesisitiza kutengeneze mfumo wa kumfanya mwanadamu kujitambua zaidi, yaani kuwa creative (mbunifu) na innovative (mvumbuzi). Siyo suala la copy and paste (kuchukua na kubandika).

Na tatizo kubwa tulilonalo, lazima kuwa na mtazamo mpana. Ukiangalia Sera yetu ya Elimu ya mwaka 2014 haina mtazamo mpana wa kuliangalia Taifa la Tanzania la miaka 20 ijayo, tunataka liwe la aina gani, miaka 100 mbele huko liwe la namna gani katika ushindani huu wa sayansi na teknolojia ya dunia ya leo.

Kwa hiyo, umewekeza zaidi kwa mwanadamu kujitambua zaidi. Na ukishawekeza kwa kutengeneza sera ambayo ni shirikishi; jamii inataka ijiongeze namna gani, suala si mpaka kufika vyuo vikuu, kuwa na vyuo vikuu vingi au kuwa na ma-PhD mengi. Suala ni binadamu anajitambua namna gani.

Mimi nimesoma Uholanzi. Nchi hii ina watu milioni 17, lakini ukubwa wake ni kilometa za mraba 36,000, ni ndogo kuliko Mkoa wa Kagera, lakini ina uwezo wa kuzalisha ikalisha watu wake na mpaka kusaidia nchi nyingine kama Tanzania yenye kilometa za mraba zaidi ya laki tisa (900,000) na watu milioni 50.

Kwa nini wameweza kufanya hivi ilhali ni 'ka-nchi' kadogo namna hiyo? Jibu ni kwamba wamewekeza kwenye rasilimali watu na rasilimali iliyo kubwa kuliko zote duniani ni rasilimali watu. Uholanzi wameweza kusuma hadi maji wakajenga tuta la bandari na uwanja wa ndege na kuwa na shirika lao imara la ndege.

Unaweza kuona ni namna gani wameweza kutumia akili zao kuwekeza kwenye utu wa mwanadamu kwanza kujitambua na ndipo mengine yakafuata.

Kwa hiyo, mimi ningekuwa Waziri wa Elimu, ningesisitiza kwanza ni namna gani Watanzania wanatambua thamani ya uhai, kujitambua kwamba katika mfumo ulio rasmi kwenye sera.

Ukitoka kwenye sera unakuja sasa kwenye mitaala ambayo inaona mbele; ione miaka 20, miaka 50 ijayo. Unatoka pale unakwenda kwenye mihtasari ya elimu na vitabu vinavyoendana na karne hii. Siyo vitabu vya kukaririsha bali vitabu vya kumfanya mwanadamu kujitambua kulingana na mazingira ya utamaduni wetu.

Tujiulize swali tu; hivi inakuwaje watoto wanaweza kutumia busati wakaweza kusoma na kuhifadhi vizuri vitabu vitukufu vya Mungu, lakini watoto hao hao unawaweka kwenye madawati mazuri na wakashindwa kuchukua a,b,c,d?

Ni kwamba kuna mbinu mbalimbali. Ni lazima kuileta jamii pamoja tunataka tuwe na mwelekeo gani unaofanana na tukubaliane fikra tofauti ili tufike pazuri na si mimi kama James Mbatia, Waziri wa Elimu naamua kila kitu. Yaani mimi ndiyo mfumo wa elimu. Hapana! Lazima tufike mahali tuweke utaratibu endelevu. Dunia ya leo ni endelevu.

Nitahakikisha tunatoa elimu shirikishi, sawa na bora kwa wote kwenye mfumo rasmi. Katika mfumo usio rasmi, tunahakikisha vyombo vyetu vya habari tunavipa kipaumbele na ruzuku kuhakikisha vinatoa elimu iliyo bora kwa jamii ili kuwa na taifa lenye mwelekeo sahihi na endelevu.

**SWALI: Hivi karibuni kumekuwa na kamatakamata ya viongozi wa kisiasa hasa wa vyama vya upinzani, lakini changamoto hii haijatokea kwako. Nini siri ya kutoingia kwako katika kadhia hiyo?**

**MBATIA:** Nimekaa muda mrefu katika siasa. Miaka ya 1990 hasa 1992, nakumbuka ilikuwa Februari 10 siku ya Jumatatu nilikamatwa na tulipigwa sana. Tulishawekwa kizuizini, nilishang'olewa kucha, niliwekwa ndani mara nyingi sana katika harakati hizi za vyama vingi vya siasa.

Lakini, unaambiwa kwamba kila neno linazaa neno jingine. Unaongea nini, na nani, mahali gani na wakati gani? 'Halafu' ni muhimu sana unapoongea mambo ya kisiasa.

Sasa ni namna gani jamii yetu inaweza kuwa katika hali ambayo ni endelevu ya kukuza mifumo ambayo ni endelevu.

Serikali ya awamu ya nne tulishiriki sana katika kumaliza migogoro iliyokuwa inatokea inayohusisha masuala ya udini, vyama vya siasa dhidi ya serikali na maandamano yaliyokuwa yanasababisha raia na polisi kufariki dunia.

Tulipoona askari wa Jeshi la Polisi na raia wanakufa, ilibidi tuwe na meza ya mazungumzo na hakuna jambo la heri dunia hii kama meza ya mazungumzo.

Na serikali naona badala ya kuwa na kamatakamata tu kunakoweka rekodi mbaya katika demokrasia yetu kwenye dunia ya leo na kuweka taswira ambayo si nzuri, kuna haja ya kuwa na meza ya mazungumzo.

Kamatakamata ya viongozi wa kisiasa haijengi nchi hii, inaibomoa maana inaonyesha kuna ukiukwaji mkubwa wa haki za binadamu.

Tukumbuke kwamba wakati wa uongozi wa Mwalimu (Julius) Nyerere, kanuni ya kwanza ilikuwa inasema binadamu wote ni ndugu zangu na Afrika ni moja. Tanzania ikapata heshima hiyo.

Leo hii tujiulize ile heshima ya Tanzania iko wapi? Wakenya wameweza kuonyesha mfano, sasa wametupiku katika kuwaweka pamoja viongozi wao na kuonyesha ni mfano katika ukanda huu wakati nafasi hiyo tulikuwa nayo sisi.

Hii inatokana na kutokuwa wavumilivu, kutokuwa tayari kusikiliza fikra mbadala, kutokushirikiana pamoja kuonyesha kwamba Tanzania ni yetu sote.

***Usikose kufuatilia sehemu ya pili ya mahojiano haya kesho, Mbatia akieleza msimamo wake kuhusu kuwania ubunge mwaka 2020.**

# Wanaume wachache wajitokeza kupima VVU

**Na Timothy Itembe,** TARIME

WANAUME wachache wamejitokeza katika uzinduzi wa upimaji wa virusi vya Ukimwi, ulioandaliwa na Chama cha Madaktari Wanawake nchini (MEWATA), Nyamongo wilayani hapa, mkoani Mara.

Upimaji huo pia ulihusisha saratani ya mlango wa kizazi na matiti na ulifadhiliwa na kampuni ya kuchimba madini ya Acacia.

Upimaji huo utafanyika siku saba katika vijiji 11 vinavyozunguka mgodi wa Acacia.

Lengo ni wananchi waende kupima na kujua afya zao na kwa wale watakaobainika kuwa na maambukizi ya virusi vya Ukimwi wataanzishiwa mara moja tiba, pamoja na wanawake na wasichana ambao watakutwa na viashiria vya saratani ya mlango wa kizazi na matiti kupewa ushauri wa kuanza matibabu.

"Upimaji huo unatolewa bure na umelenga kuwanufaisha wanawake zaidi ya 2,500 hadi 3,000 huku wanaume wote wanaoishi maeneo hayo wanahitajika kwenda kupima Ukimwi na kujua hali zao," alisema Kaimu Meneja Mkuu wa Acacia, Saimon Sanga.

Alisema upimaji huo ambao ulizinduliwa juzi na Mkuu wa Wilaya ya Tarime Glorius Luoga, wanaume waliojitokeza ni wachache kuliko wanawake ambao idadi yao imekuwa kubwa.

Luoga aliwataka wanaume wote kujitokeza kwa wingi na kuchangamkia fursa hiyo ya kupima na kujua Afya zao kwa sababu huduma hiyo imewafuata hadi mahali walipo na imekuja kwa wakati mwafaka.

Kwa upande wake Dk. Liliani Mnaburiro, alisema ugonjwa wa saratani wa mlango wa kizazi unaongoza kwa vifo katika Afrika hususani kwa wanawake wa Tanzania ambao 140 hufariki kila mwaka.

Mnaburiro aliwahamasisha wanawake na wasichana kujitokeza na kunufaika na huduma hiyo ya bure kwenda viwanja vya shule ya Ingwe Sekondari kupima na kujua afya zao.

"Kwa wiki nzima tutakuwa hapa tukipima afya, HIV, saratani ya mlango wa kizazi na matiti kwa wanawake na wasichana, shinikizo la damu, ambayo ni magonjwa yasiyoambukizwa huku tukiwa na huduma ya kuchangia damu kwa hiari ili kunusuru wanawake wakati wa kujifungua pamoja na upungufu wa damu kwa watoto," alisema Mnaburiro.

Dk. Anderea Mwita, aliwataka wakazi wa Tarime kumthamini mtoto wa kike na kumsomesha ili kuwekeza na kuachana na mila potofu ya ukeketaji ya kumuandaa kwaajili ya kumuoza kwa lengo la kujipatia mahari.

Mkuu wa Wilaya Luoga aliwataka waliofika kupata huduma hiyo kwenda kuwa mabalozi kwa wengine ili wajitokeze kwa wingi kuchangamkia fursa hiyo ambayo ni adimu badala ya kupuuza na kuishia kutumia gharama kubwa watakapokuwa wanaihitaji.

# Wananchi wapewa mbinu kuwanasa waomba rushwa

**Na Renatus Masuguliko,** GEITA

TAASISI ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa (Takukuru) mkoani hapa, imetangaza mbinu mpya ya kuwakabili watumishi wa sekta ya afya wanaoomba rushwa kwa wanaoenda kupata huduma ya matibabu.

Mbinu hizo ni pamoja na kuwatambua kwa sura watumishi wa afya wanaoomba rushwa kabla ya kuwapa ili baadaye waweze kuwatambua wakati wa gwaride la utambuzi.

Mbinu hiyo imetolewa kufuatia malalamiko kutoka kwa wananchi wakati wa tathmini ya vitendo vya rushwa katika sekta tofauti za umma na binafsi mkoani hapa.

Ofisa Mawasiliano wa Takukuru Mkoa wa Geita, Hurriet Nkya, aliyeongoza timu ya maofisa kutoka Takukuru na baadhi ya waandishi wa habari wakati wa kufanya tathmini na kutoa elimu kwa umma mitaani kwa nyakati tofauti, katika sekta ya afya, alisema mbinu hiyo itakuwa mwarobaini.

Nkya alifikia hatua hiyo baada ya mamia ya wananchi waliojitokeza kutoa malalamiko yao dhidi ya sekta ya afya kudai kuwa ni vigumu kutoa taarifa ya rushwa wakati mgonjwa ana hali mbaya na anahitaji huduma ya haraka wakihofia kupoteza maisha ya mgonjwa.

Kwa masharti ya kutoandikwa majina yao magazeti, kwa nyakati tofauti, walificha mbinu kadhaa zinazotumiwa na baadhi ya watumishi wa sketa hiyo katika vitengo tofauti ikiwamo kuachwa bila kupatiwa tiba wala ushauri ili kumfanya ndugu au mgonjwa atoe rushwa.

Mbinu nyingine zilizotajwa ni kupokea rushwa kupitia mikono ya watu zaidi ya mmoja na kugawanywa kuanzia wahudumu hadi maofisa.

Nkya alisema ndugu wa wagonjwa wakiona hakuna jinsi wanaweza kutoa rushwa ili kuokoa maisha ya wagonjwa wao au wenyewe na kisha kuwatambua kwa sura waliowapatia.

Alisema baada ya kupatiwa huduma watoe taarifa au kabla ya kufanyika gwaride la utambuzi na kuwanasa.

Kwa nyakati tofauti wakati wa zoezi hilo la kufanya tathimini, Nkya alitaja majukumu ya Takukuru kuwa ni pamoja na kuchunguza, kukamata, kushitaki na kutoa elimu kwa umma kuhusu rushwa.

ELEZA



Kaimu Ofisa Mtendaji Mkuu wa DAWASA, Dk. Suphiani Masasi (kulia), akimpa maelezo Waziri wa Maji na Umwagiliaji, Prof. Makame Mbarawa, alipotembelea mitambo ya Ruvu Chini mkoani Pwani jana. **NA MPIGAPICHA WETU**

# Mafunzo wanasheria kuwawakilisha wateja wanaofungua mashauri

**Na Mwandishi Wetu,** ARUSHA

ZAIDI ya wanasheria 30 waliojiandikisha katika Mahakama ya Afrika ya Haki za Binadamu na Watu (AfCHPR), kuwawakilisha wanaofungua mashauri katika mahakama hiyo, wameanza mafunzo ya umahiri.

Kwa mujibu wa taarifa iliyotolewa na msajili wa mahakama hiyo jana yenye makao yake makuu jijini hapa, Dk. Robert Eno, mafunzo hayo yatatolewa kwa siku tatu kuanzia leo (Jumatatu) hadi Julai, 11.

Alisema mafunzo hayo ni ya pili kufanyika baada ya yale yaliyofanyika mwaka jana yaliyokuwa na wanasheria zaidi ya 40 kutoka nchi mbalimbali wanachama wa Umoja wa Afrika.

Hadi kufikia Juni 30, mwaka huu, mahakama hiyo ilipokea maombi 178 ya wanasheria kuchaguliwa kupata mafunzo hayo, lakini ilifikia kuchagua wanasheria 48.

Rais wa AfCHPR, Jaji Sylvain Oré, alisema lengo la mafunzo hayo ni kuwawezesha wanasheria kutambua masuala mbalimbali na mwenendo wa uendeshaji wa mashauri katika mahakama hiyo na pia kuwajuza kuhusu skimu ya msaada wa kisheria.

"Baada ya mafunzo hayo, wanasheria wataweza kuwawakilisha wateja wao mahakamani hapo kwa kikamilifu," alisema.

Alisema hadi sasa, wanasheria 74 kutoka Afrika tayari wamekwishasajiliwa na mahakama hiyo kuwawakilisha wateja wao.

Mahakama hiyo ina majaji 11 kutoka nchi wanachama wa AU na hufanya vikao mara nne katika mfululizo wa kawaida wa kusikiliza mashauri na inaweza kusikiliza pia mashauri nje ya mfumo wa kawaida.

Nipashe
MWANGA WA JAMII

BUSARA

NGUZO KUU ZA UCHUMI ZINAKUMBUKWA?
TULIKUWA NA VIWANDA VYA NGUO VYENYE SIFA, KOROSHO, MAJEMBE N.K. VIMEKWENDA WAPI? NDEGE ZETU ZILE ZIMEKWENDA WAPI, NA TRENI YETU ILE MAARUFU IKOJE? HIVI ZILE NGUZO ZETU KUU ZA UCHUMI ZIMETELEKEZWA? TUZIFUFUE!
BALOZI CHRISTOPHER LIUNDI

# *Usajili Simba, Mtibwa umulike michuano Caf*

**DIRISHA** la usajili Ligi Kuu Bara limeshafunguliwa tangu Juni 15 na linatarajiwa kufungwa rasmi Julai 26, mwaka huu, na tayari klabu zimeshaanza kujiimarisha kwa ajili ya msimu ujao.

Hata hivyo, Ligi Kuu Bara msimu ujao inatarajiwa kuwa ngumu kutokana na kushirikisha jumla ya timu 20 tofauti na 16 za msimu uliomalizika.

Hivyo, klabu zinapaswa kufanya usajili makini zaidi na kujitahidi kuwa na vikosi vipana ili kuweza kuhimili mikikimikiki ya ligi hiyo inayotarajiwa kuanza Agosti mwaka huu.

Aidha, klabu za Simba na Mtibwa Sugar, hazipaswi kufanya makosa katika dirisha hili la usajili kutokana na jukumu kubwa lililo mbele yao la kuiwakilisha nchi kwenye michuano ya kimataifa kwa ngazi ya klabu.

Simba ambayo imetwaa ubingwa wa Ligi Kuu msimu uliomalizika, mwakani itaanza kuipeperusha bendera ya nchi kwenye kinyang'anyiro cha Ligi ya Mabingwa Afrika wakati Mtibwa Sugar ikiwa na jukumu la kuhakikisha bendera hiyo inapepea vema katika Kombe la Shirikisho Afrika.

Mtibwa imepata tiketi hiyo ya kushiriki michuano hiyo inayoandaliwa na Shirikisho la Soka Afrika (Caf), kutokana na kutwaa Kombe la Shirikisho la Soka nchi (TFF) maarufu kama Kombe la FA.

Kutokana na jukumu hilo, ni wazi Simba na Mtibwa zinapaswa kuwa na vikosi vipana zaidi vyenye wachezaji wazoefu wa mechi za kimataifa ili kuweza kufanya vizuri.

Tunasema hivyo kutokana na ukweli kwamba ifikapo Februari mwakani, michuano hiyo ya Caf huanza kutimua vumbi na wakati huo huo Ligi Kuu ikiendelea, jambo ambalo kila mwaka tumekuwa tukishuhudia visingizio vingi kutoka kwa timu wakilishi.

Ni kawaida kusikia timu za Tanzania zikidai kufanya vipaya kumetokana na ratiba ngumu za ligi na wachezaji wao kuchoka, huku suala la kutokuwa na nyota wazoefu likichukua nafasi kubwa zaidi.

Kutokana na hilo, tunaamini huu ni wakati sasa kwa wawakilishi wetu msimu huu kufanya usajili makini utakaokwenda kuondoa malalamishi yote.

Tunatarajia kuona Simba na Mtibwa zikiwa na mtazamo mpana zaidi katika usajili wao kwa kumulika nyota wazoefu badala ya kuendelea kukimbizana na wachezaji ambao hawana nafasi katika timu zao za Taifa.

Tunaamini kama usajili wa timu hizo, utamulika zaidi wachezaji wanaozichezea timu zao za Taifa, zitakuwa na wazoefu wengi kwenye michuano hiyo ya Caf ambayo ina utajiri mkubwa katika ngazi ya klabu barani Afrika.

Matarajio yetu ni kuona Simba na Mtibwa zinavunja mwiko kwa kutwaa mataji hayo makubwa kwa klabu barani Afrika na hilo linawezekana kwa kuwa makini katika dirisha hili la usajili ikiwa ni pamoja na kuimarisha vema mabenchi yao ya ufundi.


Tunatambua Simba kuwapo katika mchakato wa kusaka kocha mkuu kufuatia kuachana na Mfaransa Pierre Lechantre, hivyo hilo nalo halina budi kufanywa kwa umakini zaidi hasa kwa kutazama kocha mwenye uzoefu na soka la Afrika.

Nipashe tunavutiwa kuona ligi yetu ikisheheni wachezaji wenye uwezo wa juu kutoka nje sambamba na makocha, kwani kwa uwapo huo, kutasaidia soka letu kukua na kuwa na timu bora na imara ya Taifa.

Hivyo, si Simba na Mtibwa tu, bali tunataka kuona klabu zote 20 zitakazoshiriki Ligi Kuu msimu ujao zikifanya usajili makini hususan zile zinazosajili wachezaji kutoka nje.

Nipashe hutolewa na kuchapishwa na:
THE GUARDIAN LIMITED

**Mhariri Mtendaji:** Beatrice Bandawe
**Mhariri Wikiendi:** Epson Luhwago
**Meneja Usambazaji na Masoko:** Emmanuel Lyimo
**Meneja Matangazo:** Prosper Kwigema
**Chumba cha Habari:** 022 700735/8, 0779633447
**Idara ya Matangazo:** 022 700735/8, 0766 721072
Baruapepe: inquiries@guardian.co.tz
bookings@guardian.co.tz
csm@guardian.co.tz : **Website:** www.ippmedia.com






Na Faustine Feliciane

## Muungwana Lazima Nilonge

# *Tunajifunza nini Kombe la dunia?*

**FAINALI** za Kombe la Dunia zimeingia kwenye hatua ya nusu fainali.

Timu za taifa za Uingereza, Croatia, Ufaransa na Ubelgiji ndizo zilizofanikiwa kutinga kwenye hatua ya nusu fainali ya michuano hiyo.

Fainali za kombe la Dunia la mwaka huu limeleta msisimko zaidi kwa kuwa timu zilizokuwa zikipewa nafasi kubwa ya kufanya vizuri zimetolewa.

Timu kama Brazil, Ureno, Hispania, Argentina na Ujerumani zilikuwa zikipewa nafasi kubwa ya kufanya vizuri, lakini mwisho wa siku wameanguka vibaya na kuondoka kwa aibu.

Kuna timu zilikuwa hazipewi nafasi kwenye fainali hizi, timu kama Ubelgiji na Croatia achilia mbali Uingereza, zilikuwa hazipewi nafasi, lakini mwisho wa siku zimetinga hatua ya nusu fainali.

Hapa kuna jambo la kujifunza kwetu Watanzania.

**Bila shaka timu kama Ubelgiji na England ambazo hazijatinga hatua hiyo kwa miaka mingi kwa miaka yote zilikuwa zikijiandaa kwa miaka mingi na matokeo yake yameonekana kwenye fainali za mwaka huu.**

Bila shaka timu kama Ubelgiji na England ambazo hazijatinga hatua hiyo kwa miaka mingi kwa miaka yote zilikuwa zikijiandaa kwa miaka mingi na matokeo yake yameonekana kwenye fainali za mwaka huu.

Shirikisho la Soka Tanzania (TFF) linapaswa kujifunza sasa kupitia kwenye fainali hizi za Kombe la Dunia.

TFF ijifunze namna ya kuandaa timu kuelekea kwenye michuano ya kimataifa.

Hakuna kinachoshindikana kwetu kuwa na timu imara ya kututambulisha duniani.

Ni aibu kwa nchi yenye watu zaidi ya milioni 50 kutokuwa na timu imara, kwani hakuna vipaji?, vipo vingi sana.

Ni suala la kuamua ni tunaanzia wapi kuandaa timu yetu.

Wachezaji, makocha na TFF tujiangalie kupitia fainali hizi.

Hakuna ubishi kuna mengi ya kujifunza kwetu kupitia michuano hii inayoendelea, hata CECAFA wajifunze hapa.

Binafsi kikubwa ambacho naona kinapaswa kufanyika ni kujielekeza zaidi katika kujenga vituo vya michezo (Academies). Ni kupitia vituo hivi tunaweza kutengeneza vijana wenye uwezo wa kusakata kandanda.

Vijana hao baadaye ndio wanakuwa tegemeo katika timu za vijana kisha baadaye kuchezea timu ya taifa.

Nchi zinazotamba kwa uchezaji wa hali ya juu wa soka walipatikana huko na vile vile suala la kusaka vipaji katika maeneo mbalimbali ya nchi yetu linapaswa kuwa mkakati.

Haiingii akilini kuona nchi ndogo na zenye idadi ndogo ya watu zinakuwa na vipaji, wakati nchi yetu yenye watu takribani milioni 50 ikishindwa kupata wachezaji wenye vipaji vya soka 22!

Ushauri huu ukizingatiwa na kutekelezwa kupitia programu mbalimbali na kwa hatua, hakika tutafika mbali miaka ya usoni.

## BARUA/MJADALA

### *Tanesco iajiri mafundi wa kutosha!*

**Mhariri habari**

*NINAANDIKA barua hii katika gazeti letu linalotuhabarisha mambo mengi yenye faida kwa ustawi wetu wa kila siku na maendeleo ya taifa kwa ujumla.*

*Ninajitokeza kuzungumzia kero inayotupata sisi wakazi wa Magomeni jijini Dar es Salaam inayohusiana na kukatika umeme mara kwa mara.*

*Tatizo hili linasababishwa na hitilafu zinazojitokeza kwenye transfoma iliyoko katika eneo letu kiasi cha kuharibika mara kwa mara.*

*Sasa wajibu wetu kama wakazi wa eneo hili ni kutoa taarifa Tanesco pale umeme unapokatika, ili waje kuitengeneza transfoma hiyo na kwa kweli mara nyingi wamekuwa wakiitikia wito.*

*Tatizo sasa ni kwamba kila mara mafundi wanapofika na kutengeneza, wanapoondoka muda mfupi baadaye tatizo hujirudia tena.*

*Sasa hali hii imekuwa kero kwetu kwa sababu tatizo linashindikana kumalizika.Ninaomba kwa Tanesco kama hawana mafundi wa kutosha basi wamwambie Rais Magufuli ili aajiri mafundi wa kuweza kutengeneza na kulimaza tatizo hili mara moja, kuliko hii ya njoo, rudi huku tatizo likiendelea kubakia palepale.*

**Jamila Hussein- Mapipa Dar**

### *Tabia hii si ya kiungwana!*

**Mhariri, pole na Majukumu**

*NINAANDIKA kwa kweli kulaani kabisa tabia hii isiyo ya kistaarabu ya baadhi ya wasafiri wanaotumia usafiri wa umma katika majiji na miji yetu nchini na hasa daladala jijini Dar es Salaam, Vifodi jijini Arusha na Express jijini Mwanza.*

*Tabia ninayoilaani ni ile ya baadhi ya wasafiri katika mabasi hayo kutematema mate ovyo tena bila ya kujali kwamba kitendo hicho si cha kiungwana kwa sababu kinakwaza abiria wengine walio ndani ya basi husika.*

*Mhariri, utakuta mtu amekaa na abiria mwenzake tena hayuko dirishani ama wakati mwingine amesimama, lakini utaona ananyanyuka na kufungua dirisha bila hata ya kuomba, huyo anatema mate pwaa.*


*Mbaya zaidi basi likiwa katika mwendo na hivyo kuwa karaha tu na tena mtu mwenyewe wala hana hata mpango wa kuomba samahani kana kwamba hakuna kitu kisichofaa alichofanya.*

*Ninaomba watu wa aina hii wajifunze ustaarabu na waelewa kuwa kitendo hicho si cha kiungwana na kinawakwaza wasafiri wengine.*

**Mstaarabu, D'Salaam**

**WASILIANA NASI:**

TUNAKARIBISHA BARUA NA MAONI YA MSOMAJI, UNAWEZA KUTUMA KUPITIA KWA MHARIRI S.L.P. 31042, DAR ES SALAAM AU mhariri@nipashe.co.tz




# England imefuta dhana ya 'mapro' kwa wazawa

**Na Adam Fungamwango**

SOKA la Tanzania lina matatizo mengi sana yanayosababisha lisisonge mbele. Lakini kuna baadhi ya wadau, wakiwamo hata viongozi wenyewe huwa wanajibu majibu mepesi tu, wanapoulizwa sababu hasa ya kuporomoka kila uchao.

Sababu hizi zimekuwa zikibebwa na kuaminiwa na Watanzania wengi wa soka nchini kuwa ni kweli, badala ya kutafuta viini halisi vinavyodumaza mpira.

Kwa miaka mingi moja ya sababu dhaifu ni kupinga wachezaji wa kigeni. Kuna ambao wanataka idadi ya wachezaji sababu wanaoruhusiwa kwa sasa ipunguzwe ibakie watatu tu.

Wengine wanakwenda mbali zaidi na kutaka wasiwepo hata mmoja.

Hawa wote ukiwauliza wanadai kuwa wachezaji wa kigeni ndiyo sababu ya kudumaa, kuporomoka, au kutopanda kwa soka la Tanzania.

Ukihoji zaidi wanakwambia hata England haifanyi vizuri kwenye michezo ya kimataifa kwa sababu ya kuruhusu wachezaji wengi wa kigeni kuingia nchini humo kucheza soka la kulipwa.

**Ukihoji zaidi wanakwambia hata England haifanyi vizuri kwenye michezo ya kimataifa kwa sababu ya kuruhusu wachezaji wengi wa kigeni kuingia nchini humo kucheza soka la kulipwa.**

Hii imekuwa ni silaha kubwa kwa viongozi na mashabiki wengi wa soka chini.

Lakini sasa tumeanza kujionea wenyewe kuwa hilo linalofikiriwa na Wabongo na kutuaminisha sivyo. Inawezekana ni kinyume chake. Hivi tunavyozungumza England imeingia hatua ya nusu fainali ya Kombe la Dunia.

Juzi Jumamosi ilifanikiwa kuingia hatua hiyo kwa kuitwanga Sweden mabao 2-0. Yalikuwa ni mabao ya Harry Maguire na Dele Alli.

Mwaka huu, England imeonekana ina kikosi imara cha vijana wadogo wenye uwezo mkubwa wa kusakata kandanda na wote wanacheza Ligi ya England.

Kwa miaka mingi England imekuwa haifanyi vizuri kwenye mechi za kimataifa na wahafidhina wamekuwa wakiitumia hiyo kudai kuwa sababu ni kuwaruhusu wageni wengi kwenye ligi yao.

Ukweli umeanza kudhihiri kuwa tatizo la England si kujaza wageni, ila tu haikuwa na wachezaji wengi wazuri au 'kizazi cha dhahabu.'

Hiki sasa kilichopo ndicho kizazi chenyewe ambacho miaka minne ijayo kinaweza kufanya makubwa zaidi ya haya.

Kuwapo kwa wachezaji wengi wa kigeni kwenye nchi yao pia kunaweza kuwa kumechangia kuwafanya wachezaji hao ambao wengi ni vijana wawe imara zaidi na kutokuwa na woga wa mechi au nchi yoyote kwa sababu wanacheza na timu za mataifa zenye wachezaji ambao wanawafahamu.

Kutokana na hayo, ile dhana ya kwamba England haifanyi vema kutokana na kujawa wachezaji wengi wageni na kusababisha wao kutoonyesha vipaji vyao, sasa inakufa rasmi.

Hapa sasa Wabongo tuanze kuangalia sababu halisi la soka letu kuporomoka na si kusingizia eti kwa sababu ya kuingiza wageni wengi nchini.

Inawezekana kuna mapungufu tu ya kuruhusu wageni wasiokuwa na viwango, lakini ni dhambi kuwa kuwa kwenye soka lolote lile kupinga wachezaji wa kigeni kwa sababu tu eti ya kulinda vipaji vya wazawa.

Siku zote vipaji vya wazawa vinalindwa kutokana na kushindana na wageni, ama wazawa watoke kwenda kushindana nje ya nchi, au waletwe wageni washindane nao ndani.

Wachezaji wa England wamefurukuta mbele ya wageni lukuki kwa muda mrefu na sasa wamepata kile ambacho walikuwa wanakihitaji. Wabongo na sisi tuendelee kukuza soka letu kwa misingi bora na ya kisayansi na si kwa hoja zisizo na mashiko za kutaka kupunguza wachezaji wa kigeni, kwani England tuliokuwa tunawatolea mfano sasa wametusuta.

**KABWELA** **NA FADHIL MOHAMMED**






Naibu Katibu Mkuu Wizara ya Maliasili na Utalii, Dk. Aloyce Nzuki (katikati), akizungumza na waandishi wa habari (hawapo pichani) baada ya kumalizika kikao kilichowakutanisha na Bodi ya Utalii Tanzania (TTB) na Shirika la Ndege Tanzania (ATCL), kujadili namna ya kuboresha na kutangaza sekta ya utalii kufuatia kuwasili kwa ndege kubwa ya Dream liner itakayochochea watalii wengi kuja nchini. Kushoto ni Mwenyekiti wa Bodi ya ATCL Mhandisi Emmanuel Korosso na kulia ni Mwenyekiti wa Bodi ya Utalii TTB, Jaji mstaafu Thomas Mihayo. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# JK awa kivutio, mamia wamshangilia Sabasaba

**Na Mary Geofrey**

RAIS mstaafu wa awamu ya nne, Jakaya Kikwete jana ametembelea Maonyesho ya 42 ya Kimataifa ya Biashara yanayoendelea jijini Dar es Salaam na kuwa kivutio kwa mamia ya wananchi walioingia katika maonyesho hayo kwa kumzunguka.

Kutokana na kusongwa na idadi hiyo kubwa ya watu, alilazimika kukatisha ziara yake ya kutembelea mabanda.

Kikwete aliwasili katika viwanja hivyo saa 8:00 mchana na kuanza kutembelea banda la Chuo Kikuu cha Dar es Salaam (UDSM).

Mabanda mengine aliyotembelea ni la Viwanda, Biashara na Uwekezaji na Mfuko wa Fursa Sawa kwa Wote (EOTF).

Baada ya wananchi kumuona, walinza kushangilia na kusema wamemmisi, hali hiyo iliendelea katika kila banda alilotembelea licha ya ulinzi mkali uliokuwa umewekwa na usalma, skauti na askari polisi.

Akizungumza na waandishi wa habari kuhusu maonyesho hayo, Kikwete aliishauri Wizara ya Viwanda, Bashara na Uwekezaji kuwawezesha wajasiriamali waliofika kuonyesha bidhaa zao kupenya katika soko la kimataifa.

Alisema ni jukumu la wizara hiyo kuwasaidia wafanyabiashara kulifikia soko la kimataifa kwa sababu bidhaa zao ni nzuri na zina ubora unaokubalika kimataifa.

Kikwete pia aliwataka wafanyabiashara wa ndani kujifunza kwa wafanyabishara walioendelea kwa kutumia maonyesho kujifunza na kubuni vitu vyenye ubora.

# Tuhuma zilivyoondoa askari wote hifadhini

**INATOKA UK. 3**

waliweza kuwatambua askari watano wa TAWA waliowatuhumu kuwaomba rushwa na papo hapo Waziri Kigwangalla akawaamuru kukabidhi silaha zao na kumwagiza Mkuu wa Polisi wa Wilaya ya Kipolisi ya Laela, Aloyce Nyatola, kuwakamata mara moja na Takukuru ianze uchunguzi wa tuhuma hizo ili sheria ichukue mkondo wake na liwe fundisho kwa wengine.

Baada ya mkutano wa hadhara, Dk. Kigwangalla aliamua kukagua baadhi ya maeneo ndani ya pori hilo na kubaini uharibifu mkubwa uliofanywa na mifugo huku dalili zikiwa ni kinyesi cha ng'ombe kilichokuwa kimezagaa kila mahali.

Hapo hapo alimwagiza Mkurugenzi Mkuu TAWA, Dk. James Wakaibara, ambaye aliwakilishwa na Mkurugenzi wa Biashara na Huduma za Utalii wa mamlaka hiyo, Imani Nkuwi, kuwasimamisha kazi wafanyakazi wote wa pori hilo na kuleta wengine wapya walisimamie ili kupisha uchunguzi.

"Hawa wote wasimamishwe kazi na uchunguzi ufanyike, kitu gani kilikua kinaendelea hapa, kwanza ifanyike parade (gwaride) kuhusu suala la kuomba rushwa yule mfugaji, wabainike moja kwa moja wafunguliwe mashtaka," alisema na kuongeza:

"Na hawa wote nataka wachunguzwe na mali walizonazo kama ambavyo imeelezwa kuwa hawa wametumia hili pori kama kitega uchumi chao binafsi, huu ni uhujumu uchumi."

Wakati huo huo, Dk. Kigwangalla ametoa siku 30 kwa wananchi wote wenye mifugo ndani ya pori hilo kuitoa kwa hiari yao wenyewe kabla ya operesheni maalum itakayowaondoa kwa nguvu.

Alisema kama walijua pori hilo ni shamba la bibi sasa wasahau na wajipange namna ya kutafuta malisho au kupunguza idadi ya mifugo yao na kuanzisha miradi mingine ya maendeleo.

# JPM ataja sababu tatu kufufua ATCL

**INATOKA UK. 2**

Victoria na Nyasa watashindwa kusafirisha samaki wao.

"Wengi tulishindwa kutumia usafiri wa ndege kwa sababu kulikuwa hakuna usafiri wa uhakiki wa ndege nchini, zamani ATCL ilikuwa inaenda Dar es Salaam, Mwanza na Arusha tu," alisema Rais Magufuli.

Alisema Watanzania walishindwa kutumia usafiri wa ndege kwa sababu gharama zake zilikuwa juu, akitolea mfano Mkoa wa Kagera ilikuwa ni zaidi ya Sh. milioni moja kwenda, lakini kwa sasa ni Sh. 400,000 kwenda na kurudi.

Rais Magufuli alitaja sababu ya tatu ni kukuza sekta ya utalii, ambapo alisema Tanzania ni nchi ya pili kwa kuwa na vivutio vingi vya utalii duniani, lakini ilikuwa haina ndege.

Alisema sekta ya utalii licha ya kuongoza katika kuleta fedha za kigeni, mchango wake bado siyo mkubwa, kuliko sababishwa na kupokea idadi ndogo ya watalii.

"Mwaka jana tulipokea watalii milioni 1.3, wakati Misri inapokea watalii milioni 10.1, Morocco inapokea watalii milioni 12, Afrika ya Kusini watalii milioni 12.29 kwa mwaka, hata Kenya wanatuzidi," alisema Rais Magufuli.

Alisema nchi hizo zimekuwa na mashirika ya ndege imara, hivyo ni rahisi kwao kuwasafirisha watalii kwenda katika nchi zao.

Rais Magufuli alisema kwa mwaka jana watu bilioni nne walitumia usafiri wa ndege, na watu bilioni 1.3 walifanya utalii, na asilimia 70 kati yao walitumia ndege.

Alisema serikali inataka kuona ndege hiyo mpya inafanya safari za kimataifa, ili ilete watalii wengi zaidi.

Rais Magufuli alisema miaka ya nyuma ATCL ilikuwa na ndege moja ndogo yenye uwezo wa kubeba watu 51, na ilikuwa inafanya kazi katika miji mitatu tu.

Alisema ndege hiyo moja ilikuwa inashinda karakana, Alisema ndani ya miaka miwili serikali imenunua ndege mpya saba.

Alisema ndege zingine mbili aina ya Bombadier CS 300 zenye uwezo wa kubeba abiria 132 kila moja zitawasili Novemba mwaka huu, na moja kubwa itawasili mwaka 2020.

Alisema matokeo hayo ni jitihada za Watanzania ambao wamekuwa wakilipa kodi.

Alisema kwa sasa serikali inaimarisha huduma za majini, kwa kupanua bandari ya Dar es Salaam, Mtwara na Tanga.

Alisema kwa sasa wasafirishaji wengi wa mizigo wanaitumia bandari ya Dar es Salaam kusafirisha mizigo yao.

Alisema katika barabara, serikali inajenga barabara nyingi, ujenzi wa barabara za juu, ujenzi wa reli ya kisasa pamoja na utekelezaji wa miradi ya umeme.

Naye Katibu Mkuu Sekta ya Uchukuzi, Leonard Chamriho, alisema ndege hiyo itaanza kufanya safari za ndani katika mikoa ya Kilimanjaro, Mwanza, na Dar es Salaam.

Alisema ifikapo Septemba mwaka huu, ndege hiyo itaanza kwenda katika miji ya Bombay, Guangzhou na nchi za Thailand, Uingereza. Naye Katibu Mkuu Kiongozi, Balozi John Kijazi alisema uamuzi wa serikali kununua ndege saba ni wa manufaa makubwa na utaongeza ushindani wa kibiashara kati ya ATCL na mashirika mengine, na kupanua shughuli za utalii.

Viongozi wengine waliokuwapo ni Makamu wa Rais, Samia Suluhu Hassan, Waziri Mkuu, Kassim Majaliwa, mawaziri, wabunge, wakuu wa mikoa, viongozi wa dini na sekta binafsi.

HABARI KITAIFA

# Wito kusaidia wenye ulemavu

**Na George Tarimo,** IRINGA

JAMII imetakiwa kujenga utamaduni wa kuwasaidia na kuwapatia msaada watu wenye mahitaji maalumu (ulemavu) wa elimu kwa kuwa msingi wa kumsaidia mwenye ulemavu ni elimu pekee.

Kauli hiyo ilitolewa na Mbunge wa Viti Maalum, Amina Mollel (CCM), alipotembelea familia moja yenye watu watatu wote ambao ni walemavu katika Kijiji cha Lulanzi wilayani Kilolo mkoani Iringa.

Familiya hiyo ina watoto watano wote walizaliwa wakiwa wazima, lakini kadiri wanavyozidi kukua wanaanza kuugua miguu na hatimaye wanakuwa walemavu.

Mollel (pichani) alitoa msaada wa vitu mbalimbali ikiwamo baiskeli ya kutembelea kwa walemavu hao ambao ni Jenipha Mpogole , Catherine Mpogole na Eliasi Mpogole.

Pia Mollel alisema kuwa Bunge limetenga asilimia mbili kwa ajili ya walemavu kote nchini, hivyo kuwataka wenye ulemavu ambao wana uwezo wa kufanya kazi na kujiajiri kwa kuwa tayari serikali ya awamu ya tano imeshawawekea mazingira mazuri.

Aliwataka walemavu kuunda vikundi ambapo halmashauri itawasaidia asilimia mbili kwa sababu asilimia nne imeshatolewa kwa vijana na asilimia nne kwa wanawake.

"Kuwa na ulemavu ni jambo la baraka kutoka kwa Mungu, mimi mwenyewe ni mlemavu nisingesoma nisingefika hapa nilipo na ndio maana natamani sana walemavu wote kote nchini msingi wa maisha yao yote iwe ni elimu na ndio maana leo hii narudisha fadhila kwa walemavu kwa sababu hata mimi nilisaidiwa," alisema Mollel na kuongeza:

"Tuwe na moyo wa upendo, kusaidia, unapotaka kusaidia mlemavu mpe elimu, jamii isiwanyanyapae. Pamoja kuwa na watoto hawa mimi nasema siku zote ndio baraka za Mungu, wasikate tamaa ili wao wajisikie binadamu kama wengine," alisema Mollel.

Mama wa walemavu hao, Anjelista Kihanza, alishukuru kwa msaada huo huku akisema kuwa aliwazaa wakiwa wazima na ilipofika kipindi walianza kupata ulemavu hadi sasa.



# Jaji aonya mawakili wasiotambulika

**Na Halima Ikunji,** TABORA

MAHAKAMA Kuu kanda ya Tabora imekemea mawakili matapeli wasio tambulika kisheria na mahakama kuacha kujinadi na kutoa huduma za kimahakama kwa wananchi, hatua kali zitachukuliwa dhidi yao pindi watakapobainika.

**Mawakili wasiotambulika na mahakama wamekuwa wakijipatia fedha hizo kwa njia hiyo ya udanganyifu kinyume cha sheria ambapo ni kosa kisheria.**

Akitoa elimu kwa wananchi katika eneo la mahakama ya kanda hiyo, Jaji Mfawidhi wa Mahakama Kuu Kanda ya Tabora, Sam Rumanyika, amebainisha kuwapo kwa mawakili wasiotambulika na mahakama kujiingiza katika utapeli wa fedha kwa wananchi wakijinadi kutoa huduma za kuwasaidia kesi zao.

Jaji Rumanyika alisema kuwa mawakili hao wasiotambulika wanaowashawishi wananchi kwamba wao wana uwezo wa kuwasimamia katika kesi zao zilizopo mahakamani na uwachukulia fedha zao, ili wawafanyie kazi huku wakitambua kuwa hawana sifa na uwezo huo.

Alisema mawakili wasiotambulika na mahakama wamekuwa wakijipatia fedha hizo kwa njia hiyo ya udanganyifu kinyume cha sheria ambapo ni kosa kisheria na wanaipaka matope tasnia ya sheria na mahakama kwa ujumla.

Alisema mahakama imejipanga kupambana nao na kukomesha suala hilo ambapo amewataka wananchi kuunga mkono juhudi za kuwabaini kwa kutoa taarifa kwao na kwa vyombo vingine vya dola, ili kufanikisha kuwakamata na kuwachukuliwa hatua kali za kisheria.

"Watu hawa ambao naweza kuwaita ni makanjanja wamekuwa wakiwalaghai wananchi kuwa wana uwezo wa kushughulikia kesi zao na wengine wamekuwa wakidai wameagizwa na jaji ili watoe pesa kwa ajili ya kumaliza kesi zao, kitu ambacho si kweli na ni utapeli wa hali ya juu na ni kupakana matope," alisema jaji huyo.

Alieleza mahakama imejipanga kupambana na watu hao wakishirikiana na wananchi.

KATAPILA




Katapila likisawazisha barabara jana eneo la Mbezi Mwisho jijini Dar es Salaam, yakiwa ni maandalizi ya ujenzi wa barabara ya Mbezi hadi kwa Hossama kwa kiwango cha lami. **PICHA: SABATO KASIKA**

# TTB, ATCL wateta ujio wa ndege

**Na mwandishi Wetu**

BODI ya Utalii Tanzania (TTB) na Shirika la Ndege (ATCL) wamekutana kujadili namna ya kuboresha na kutangaza sekta ya utalii muda mfupi kabla ya kuwasili kwa ndege kubwa ya Dream Liner itakayochochea utalii kuwasili nchini.

Katika kikao hicho kilichohudhuriwa na Naibu Katibu Mkuu Wizara ya Maliasili na Utalii, Dk. Aloyce Nzuki, kimelenga kuunganisha nguvu kwa pamoja kati ya taasisi hizo mbili ili kuchochea ukuaji wa sekta ya utalii hasa kwa uwapo wa ndege za Tanzania ikiwa ni juhudi ya Rais John Magufuli za kuinua shirika la ndege na sekta ya utalii kwa ujumla.

Kupitia kikao hicho Dk. Nzuki aliagiza TTB kufanya mabadiliko ya makusudi katika mikakati ya kutangaza vivutio vya utalii na hasa kupitia ujio wa ndege kubwa ya Dream Liner inayobeba abiria 262 itakayokuwa inafanya safari zake katika nchi ya China na India.

"Umuhimu wa ndege hii kubwa ni kufanya safari ndefu za moja kwa moja zitakazochochea ongezeko la watalii hivyo ni vyema taasisi hizi kutazamia fursa hiyo na kufanya juhudi za makusudi kujitangaza kimataifa," alisema Dk. Nzuki.

Aliongezea kuwa uwapo wa ndege hizo zitampunguzia gharama mtalii kwani wamekuwa wakiingia gharama kubwa katika safari za ndege wapokuja nchini kutembelea vivutio vyetu vya utalii hivyo tunaamini uamuzi wa serikali wa kuwa na ndege zake utachochea zaidi utalii.

Aliziagiza taasisi hizo mbili kuwa na vikao vya mara kwa mara vya kupanga mikakati ya kuboresha sekta ya utalii itakayosababisha kuongezeka kwa idadi ya watalii nchini na kufanya sekta kuwa na mchango kubwa katika pato la taifa.

Dk. Nzuki aliitaka TTB kutafuta wakala maalum atakayeshughulika za kuvitangaza vivutio hasa katika nchi ya India na China ambapo ndege yetu itaanza kufanya safari zake hivyo ni lazima kuwa na wakala atayesaidia kututangaza kimataifa.

Mwenyekiti wa Bodi ya TTB, Jaji mstaafu Thomas Mihayo, alisema mchakato wa kutafuta wakala wa moja kwa moja katika nchi za India na China atakayesaidia kutangaza vivutio vyetu ilishaanza.

"Tayari tumeshateua ofisa atakayeshughulika na masoko ya utalii kwa India na China ambako ATCL itaanzisha safari za moja kwa moja mara ndege ya Dream Liner itakapowasili nchini," alisema Jaji Mihayo.

Naye Mwenyekiti wa Bodi ya Wakurugenzi wa ATCL, Mhandisi Emmanuel Korosso, alisema lengo la kikao hicho ni kuwa na mkakati wa pamoja kati ya TTB na ATCL ni kuchochea ongezeko la watalii nchini baada ya kuanza kwa safari za India na China baada ya kuwasili kwa ndege ya Dream liner.

# Mwenyekiti aliyetoweka mwaka 2017 apata mrithi

**Magreth Magosso,** KIGOMA

HALMASHAURI ya Wilaya ya Kibondo mkoani Kigoma, imefanikisha kuziba nafasi ya mwenyekiti wake kwa kumchagua Falesi Nzobona baada ya sintofahamu ya alipo aliyekuwa akishikilia nafasi hiyo, Simon Kanguye.

Kanguye hajulikani alipo tangu mwaka 2017 hadi leo.

Baraza la Madiwani kupitia sheria, taratibu na miongozo ya kikanuni, Jumamosi lilifanya uchaguzi na Nzobona kupitia CCM alishinda kwa kura 20 kati ya wajumbe 25, hivyo kuwa mwenyekiti mpya wa halmashauri, huku mshindani wake kutoka Chadema, Julius Kihuna, akipata kura tano.

Baraza hilo linaundwa na madiwani 26 tu, wa kuchaguliwa ambapo CCM ina kata 12,na vyama vya upinzani vikigawana kata sita pamoja na madiwani wa viti maalum watatu, huku chama tawala kikiwa na madiwani wa viti maalum watano.

**Wanatambua upo upinzani wa kisiasa, ila wanachoomba upinzani uwapo wa kutatua kero na changamoto za umma na si kuligawa taifa na watu wake kwa itikadi za chama ama dini.**

Akizungumza baada ya uchaguzi huo, Nzobona aliwashukuru madiwani wenzake kwa kumpa nafasi hiyo kwa kuona uwezo wake kiutendaji utasukuma shughuli za maendeleo kwa wilaya na jamii kwa ujumla.

Baadhi ya viongozi wa dini wakiwamo Askofu Themeo Ndenza wa Dayosisi ya Kibondo wa Kanisa la Anglikana na Mwakilishi wa Shekhe wa Wilaya, Uled Issa kwa nyakati tofauti walieleza kuwa changamoto zilizopo kwa wananchi ni fursa ya kuonyesha uwezo wake kwa jamii hususani ukosefu wa maji na adha inayoikabili sekta ya elimu, zitatuliwe kwa umoja wa viongozi kwa ustawi wa umma.

Walisema wanatambua upo upinzani wa kisiasa, ila wanachoomba upinzani uwapo wa kutatua kero na changamoto za umma na si kuligawa taifa na watu wake kwa itikadi za chama ama dini.

Mkuu wa wilaya hiyo, Luis Bura, aliwakumbusha madiwani waache tabia ya migawanyiko kwa umma, ambayo inasababisha kuzorotesha shughuli za uzalishaji mali hatimaye wanalaumiana.

Aidha, Bura aliwataka watumishi wa umma na viongozi kwa ujumla waungane ili watoe huduma bora zenye tija kwa ajili ya kuwaondolea wananchi umaskini wa kipato.

WANAJESHI



Mtaalamu wa upishi wa bia katika kiwanda cha TBL Ilala jijini Dar es Salaam, Christian Tarimo, akiwaeleza baadhi ya wanajeshi wa Zimbabwe juu ya uzalishaji wa bia, walipotembelea kiwanda hicho mwishoni mwa wiki. **NA MPIGAPIGA WETU**

# Fedha ruzuku shule changamoto

**Na Happy Severine,** BARIADI

IMEELEZWA kuwa licha ya serikali kutoa ruzuku kuendesha shule za msingi na sekondari kama mpango wa kutoa elimu bila ya malipo, bado ruzuku hiyo inayotolewa kwa kila shule haitoshelezi mahitaji.

Aidha, ruzuku hiyo inayotolewa kila mwezi, inaelezwa kutoendana na idadi halisi ya wanafunzi kwa baadhi ya shule, huku wakati mwingine ikidaiwa kuchelewa kuzifikia shule kwa muda mwafaka.

Hayo yalibainika jana wakati wa uwasilishwaji wa ripoti ya matokeo ya ufuatiliaji wa fedha za ruzuku kwa wadau wa elimu Wilaya ya Bariadi, iliyofanywa na Mtandao wa marafiki Elimu Bariadi chini ya taasisi ya Haki Elimu.

Akiwasilisha ripoti hiyo katibu wa mtandao huo, Julian Mbakiza, alisema kuwa utafiti huo ulifanyika katika halmashauri tatu, Itilima, Halmashauri ya Mji wa Bariadi na Halmashauri ya Wilaya ya Bariadi mkoani Simiyu.

Mbakiza alisema utafiti huo uliofanyika mwaka huu, ulizishirikisha jumla ya shule 10 kutoka kwenye halmashauri hizo, ambapo ulilenga kuangalia hali ya uelewa, upoaji, matumizi, na utoshelezi wa ruzuku hiyo.

Alisema asilimia 100 ya walimu wakuu wa shule hizo walihojiwa, walisema kuwa ruzuku hiyo haitoshelezi mahitaji ya shule zao, ambapo wanapokea fedha kidogo kulingana na idadi ya wanafunzi walionao.

"Kuletwa kwa ruzuku ndogo imekuwa ikiwapashida ya kuhakikisha wanatekeleza mahitaji yote yaliyopo kwenye shule zao, kwa muda mmoja, hali hiyo inawafanya kutekeleza baadhi ya mambo na mengine kuacha," alisema Mbakiza.

Aidha, aliongeza katika utafiti huo, walimu wakuu wengi hawana taaluma ya uhasibu, hali ambayo imekuwa ikisababisha wengi kushindwa kutoa taarifa sahihi za mapato na matumizi ya pesa hizo.

"Tulibaini kuwa walimu wakuu wana majukumu mengi sana, lakini wameongezewa kuwa wahasibu wa fedha hizi, wengi wamepata matatizo ya kutoa taarifa sahihi ya mapato na matumizi na kusababisha kutoeleweka kwa wananchi," aliongeza Mbakiza.

Mwenyekiti wa mtandao huo Janeth Kato, alisema walimu wakuu wengi walidai kupata matatizo ya kutakiwa kurejesha baadhi ya fedha kutoka kwenye mifuko yao kutokana na kutotoa taarifa sahihi za mapato na matumizi.

Naye Meneja wa idara ya ushiriki na uwajibikaji jamii kutoka Haki Elimu, Pius Makomelelo, alisema kwenye utafiti huo, baadhi ya walimu wakuu hawajui ni kiwango gani wanatakiwa kupokea kwa kila mwanafunzi kwenye shule zao.

# Wadau kilimo wapewa somo

**Na George Tarimo,** IRINGA

MKUU wa Mkoa wa Iringa, Amina Masenza amekitaka Kituo cha Kuendeleza Kilimo katika Ukanda wa Nyanda za Juu Kusini na wadau wengine kusimamia utekelezaji wa changamoto zilizoainishwa katika mkutano huo wa mwaka uliomalizika jana.

Akifunga mkutano wa siku mbili wa kupitia utekelezaji wa mpango wa kuendeleza kilimo katika ukanda huo, Masenza alisema katika kikao hicho kuna changamoto nyingi zilizoainishwa na wadau ambazo lazima zipatiwe ufumbuzi.

"Kila mdau chini ya uratibu wa SAGCOT aone ana sababu za kutekeleza wajibu wake katika changamoto zilizoainishwa ikiwamo serikali kuu, serikali za mitaa, sekta binafsi tunapokutana mwakani kila madau awe amefanyia kazi changamoto katika eneo lake," alisema.

Changamoto moja aliyotaka ifanyiwe kazi kwa haraka ni ile ya uuzaji wa mazao ya kilimo kama viazi mviringo kwa kutumia vifungashio vijulikanavyo kama lumbesa ambavyo alisema havionyeshi uhalisia wa kipimo cha mzigo husika na kutaka vipimo mbadala vya kilo ndivyo vitumike.

"Kuwa na lumbesa katika zao la viazi mviringo ni uuaji na wizi wa nguvu za wakulima. Naomba viongozi wenzangu tuongeze nguvu katika kusimamia jambo hili ili kipimo kinachojulikana cha kilo ndicho kitumike kila mahali," alisema.

Kuhusu changamoto ya barabara, mkuu huyo wa mkoa aliitaka SAGCOT na mamlaka inayohusika na ujenzi na uendelezaji wa barabara za vijini kushirikiana katika kushawishi wawekezaji zaidi, ili kuwaondelea wakulima adha za kusafirisha mazao yao.

Aidha, mkuu huyo wa mkoa amemtaka Mkurugenzi Mtendaji wa Mfuko Kichocheo wa SAGCOT CTF, John Kyaruzi kutembelea kongani za Mbarali na Ihemi ili kuwaelimisha wakulima vigezo na masharti ya kupata ufadhili wa mfuko huo.

Aliitaka mamlaka inayohusika na kusimamia sekta ya mbolea (NFRA) kuongeza juhudi katika upatikanaji wa mbolea, ili wakulima waweze kupata mbolea kwa wakati mwafaka na kwa bei nafuu kuliko ilivyo kuwa nyuma.

Utekelezaji wa mpango wa kuendeleza kilimo katika ukanda wa nyanda za juu kusini umeleta mapinduzi makubwa kwenye sekta ya ufugaji na kilimo kwa kuongeza thamani ya mazao yanayotokana na sekta hizo.

# Mradi kugundua vimelea TB waanza

**Na Cynthia Mwilolezi,** ARUSHA

MRADI wa kugundua kwa haraka vimelea vya kifua kikuu kwa wagonjwa wapya na kuwatibu umezinduliwa.

katika nchi za Jumuiya ya Afrika Mashariki (EAC), umezinduliwa.

Mradi huo wa miaka mitatu uliozinduliwa mwishoni mwa wiki jijini hapa, utafanya kazi katika nchi za Jumuiya ya Afrika Mashariki (EAC).

Kaimu mkurugenzi wa kuratibu tafiti za afya kutoka Taasisi ya Taifa ya Utafiti wa Magonjwa ya Binadamu (NIMR)), Dk. Paulo Kazyoba, alisema lengo la mradi huo ni kuboresha mfumo wa afya jinsi ya kugundua vimelea vya ugonjwa wa kifua kikuu kwa nchi za Afrika Mashariki.

NIMR inashirikiana na mtandao wa kujengea uwezo tafiti za afya Afrika Mashariki katika kufanikisha mradi huo.

Alisema mradi huo umekuja kwa wakati muafaka na wao kama taasisi ya utafiti wa magonjwa ya binadamu, utawasaidia kufanya tafiti ambazo zitachangia kuboresha sera na utendaji kazi katika sekta ya afya.

"Mradi huu utachangia kwa kiwango kikubwa kutupatia majibu mazuri jinsi ya kugundua kwa haraka vimelea vya ugonjwa wa kifua kikuu, hivyo, mradi huo ni muhimu kwa Tanzania na nchi zingine za Afrika Mashariki katika kutokomeza ugonjwa wa TB," alisema.

Kwa upande wake, Prof. Sayoki Mfinanga, kutoka NIMR Muhimbili, alisema mkutano huo unawahusisha watafiti wa afya kutoka nchi tano za Afrika Mashariki.

Alisema pamoja na taratibu nzuri za kutoa tiba ya wagonjwa wa TB, bado kunahitajika mkakati mkubwa zaidi wa kuibua wagonjwa wa TB walioko kwenye jamii na kuhakikisha wanapatiwa matibabu hospitalini.

Alisema tatizo la TB bado ni kubwa kwa nchi za Afrika na kwamba ugonjwa huo upo wa aina mbili ikiwemo TB ya mapafu na viungo na hivyo, jitihada zaidi zinahitajika kufanya tafiti ya matibabu ili iwe chini ya miezi sita.

Naye Mganga Mkuu wa Mkoa wa Arusha, Dk. Timoth Wonanji, alisema wamefanikiwa kuibua wagonjwa wa kifua kikuu ambapo kwa mwaka 2016, walibua wagonjwa kwa asilimia 74 ikiwa ni zaidi ya takwimu za taifa ambazo ni asilimia 72.

"Mwaka 2017 tumetambua wagonjwa kwa asilimia 75 na takwimu za Januari hadi Machi, mwaka huu, tumevuka lengo la serikali na kufikia asilimia 85 na hii ni kutokana na ufuatiliaji maeneo ya vijijini," alisema.

Alisema takwimu zinaonyesha katika kipindi cha Januari hadi Machi, mwaka huu, wamefanikiwa kuibua wagonjwa wapya wapatao 3,180 walipimwa na kugundulika kuwa wanamaambukizi ya ugonjwa wa TB. "Ila changamoto kubwa ipo kwa upande wa watoto kuwatambua kama wana maambukizi au la," alisema.

Mradi huo unaofadhiliwa na taasisi ya EDCTP kutoka Umoja wa Ulaya (EU).



**KABIDHI**

Kaimu Mkuu wa Wilaya ya Arumeru ambaye ni Mkuu wa Wilaya ya Monduli, Iddi Kimanta, akikabidhi vyeti kwa wanafunzi wahitimu wa mafunzo ya shahada ya afya na uzalishaji kwa Wakala wa Vyuo vya Mafunzo ya Mifugo (Lita) kampasi ya Tengeru jana. Kushoto ni Mkurugenzi wa chuo hicho, Joseph Msemwa. **PICHA:ALLAN ISACK**

# 'Fugeni kuku mtakaowaita NSSF'

**Na Jaliwason Jasson,** BABATI

WANACHAMA wa vyama vya msingi vya ushirikia na Saccos, wameshauriwa kufuga kuku na kuwabatiza 'NSSF' ili baadaye wauze mayai yatakayowawezesha kupata Sh. 20,000 za mchango wa kila mwezi kwa Shirika la Taifa la Hifadhi ya Jamii (NSSF).

Ushauri huo ulitolewa na Afisa Ushirika wa Mkoa wa Manyara, Godamen Merinyo, wakati wa uhamasishaji wa kuwapata wanachama wapya kutoka sekta isiyo rasmi kujiunga na shirika hilo.

"Ninawashauri kila mmoja afuge kuku watatu na kuwabatiza NSSF, muuze mayai na kulipa mchango wa kila mwezi wa 20,000 ili kujihakikishia kupata matibabu," alisema.

Kwa upande wake, Abdul Msangi, kutoka Hanang', alisema mpango wa kuwaingiza NSSF utakuwa mkombozi kwa wakulima maana wao wanategemea kilimo hivyo wakiingizwa kwenye bima ya afya itawasaidia kupata matibabu na kuwapunguzia gharama.

Mapema Meneja wa NSSF, mkoani hapa, Alexander Joseph, alisema maisha ya mwanadamu kwa ujumla yanazungukwa na majanga na uzee, hivyo ni vema wakajiwekea akiba ili baadaye wapate pensheni itakayowasaidia.

Alisema iwapo mmoja atajiunga atatakiwa kuchangia Sh. 20,000 kila mwezi naye kwa wake atapata uhakika wa matibabu, mafao ya uzee akifikisha miaka 60, kupewa mafao ya ulemavu kama atapata majanga na kupata mafao ya uzazi kwa wanawake wakijifungua.

Alisema NSSF ipo kwa ajili yao maana inawalenga watu ambao hawako sekta rasmi, yaani, waliojiajiri na ambao wameajiriwa na mashirika ya kimataifa na makampuni ya watu binafsi.

"Majanga yanaweza kumpata mtu yeyote bila kujali yuko sekta rasmi au hayuko, majanga haya yanaathiri maisha yetu kwa ujumla, hivyo, tunatakiwa kujiandaa kukabiliana nayo maana hatujui yanakuja lini," alisema.

Naye Meneja wa NSSF, Mkoa wa Arusha, ambaye aliwakilisha viongozi kutoka makao makuu Dk. Frank Maduga, alisema asilimia 87 ya Watanzania ndio watu waliojiajiri hivyo kisheria ndilo kundi kubwa limegundulika lilikuwa limeachwa lakini kwa sasa wameamua kulipigania ili liweze kunufaika na mafao ya NSSF.

Alisema miongoni mwa changamoto walizonazo ni kuwa na wanachama waliozidi umri wa miaka 60, uchangiaji wa michango kuwa duni.

# Ushauri kilimo mkataba

**Na Mwandishi Wetu,** ARUSHA

BARAZA la Kilimo na Ufugaji nchini, (ACT), limewahamasisha wakulima kujikita katika kilimo cha mkataba ili waweze kuondokana na changamoto za upatikanaji wa masoko ya uhakika ndani na nje ya nchi.

Mwakilishi kutoka baraza hilo wilayani Arumeru, Victor Lazaro, alisema hayo katika mkutano uliowashirikisha wakulima, makampuni na wadau kutoka serikalini.

Mkutano huo ulilenga kuleta mrejesho kuhusu utafiti wa kilimo cha mkataba uliofanywa na baraza hilo wilayani Arumeru.

Alisema utafiti wa baraza hilo katika kilimo cha mbogamboga ulibaini kuwa na manufaa makubwa kwa wakulima kutokana na kuwepo soko la uhakika.

Alisema kilimo hicho cha mkataba kina manufaa makubwa endapo kitaboreshwa zaidi kwa kuwashirikisha wadau wakiwemo serikali ambao watasaidia kuboresha mikataba na kuifuatilia kwa karibu endapo inawanufaisha walengwa.

"Kilimo cha mkataba kitawanufaisha zaidi wakulima endapo watajiunga kwenye vikundi ili wafanye kazi kwa ushirikiano na kuingia mikataba na makampuni ambayo wana uhakika nayo katika utendaji kazi," alisema.

Kwa upande wake, mwenyekiti wa kikundi cha Kilimo biashara na Ufugaji wilayani Arumeru, (KIBIU) Jeremiah Ayo, alisema kilimo cha mkataba kina manufaa makubwa endapo kampuni husika itakubaliana na mzalishaji.

Alisema kwa kawaida mkulima anapoingia kilimo cha mkataba, kampuni humlipa mkulima asilimia 50 na nyingine hulipwa baada ya uhakiki wa masharti waliyokubaliana kama yamezingatiwa katika kilimo hicho.

Alisema changamoto kubwa inayowakabili wakulima wengi ni kutokuwa na elimu ya kutosha juu ya kilimo hicho cha mkataba hali inayowafanya wengi kutokufikia makubaliano.

Aliiomba serikali kutoa ushirikiano kwa wakulima wakati wanapoingia mikataba hiyo kwa kuwapeleka wataalam wa kilimo ambao watakuwa wanafuatilia hatua moja baada ya nyingine na kuhakikisha wakulima wanalipwa haki zao kwa wakati.

Naye Mhadhiri wa Shule ya Biashara Chuo Kikuu cha Dar es Salaam, Dk. Renger Kanani, alisema kilimo cha mkataba kwa wakulima kina manufaa makubwa endapo wakulima watazingatia masharti ya mikataba watakayoingia na makampuni kwani wanakuwa na uhakika wa soko na kuongeza pato.

"Lakini vema wakulima hawa tukawahamasisha kujiunga kwenye vikundi ili kunufaika zaidi na mfumo huu," alisema.

# Polisi sasa yafunguka mfugaji kupigwa risasi

**Na Godfrey Mushi,** SAME

UCHUNGUZI wa awali wa Jeshi la Polisi mkoani Kilimanjaro unaonyesha kuwa tukio la kujeruhiwa kwa kupigwa risasi mgongoni na kutokea tumboni kwa mmoja wa wafugaji katika eneo la Stelingi, Wilaya ya Same kulitokana na tafrani iliyomlazimisha askari wa wanyamapori, Gilbert Bobewe (34) kutumia nguvu.

Jana, Kamanda wa Polisi mkoa wa Kilimanjaro, Kamishna Msaidizi (ACP), Hamisi Issah, alisema mfugaji huyo ambaye ni mkazi wa Kijiji cha Masandare, Hassan Cheyavyo (43) alipigwa risasi wakati askari wa wanyamapori wakiwa katika zoezi la kuondoa mifugo kwenye Hifadhi ya Msitu wa Chambogho. "Chanzo cha kupigwa risasi (Cheyavyo) kilitokana na tafrani, wakati hawa askari wa wanyamapori wakiwaondoa wafugaji katika msitu wa Chambogho na matokeo yake kwenye hatua hizo za kuondoa mifugo ya wafugaji, ndipo silaha ilipotumika kumjeruhi. Hata hivyo, mtuhumiwa amekamatwa na sheria itafuata mkondo wake," alisema.

Inaelezwa askari waliokuwa wakilinda msitu huo wa hifadhi, Juni 29, mwaka huu wakiwa wanatekeleza majukumu yao ya kazi, walikamata ng'ombe zaidi ya 90 pamoja na mbuzi na kulazimika kuziswaga kwenda makao makuu ya Wakala wa Huduma za Misitu (TFS), Kanda ya Kaskazini.

Ulinzi wa misitu hiyo ya hifadhi unafanyika kwa mujibu wa Sheria ya Misitu, Namba 14 ya Mwaka 2002 na Kanuni zake za Mwaka 2004 pamoja na Tangazo la Serikali (GN), la Mwaka 2017, ambavyo ndivyo vitendea kazi vyao kwa mujibu wa sheria zinazosimamia rasilimali ya misitu. Aidha, hali ya majeruhi huyo aliyekuwa amelazwa katika Hospitali ya Wilaya ya Same, baada ya kufanyiwa upasuaji mkubwa ulichukua saa saba kunusuru maisha yake, inaendelea vizuri. Mganga Mfawidhi wa Hospitali hiyo, Dk. Iddi Juma aliiambia Nipashe jana kuwa Cheayavyo tayari ameruhusiwa kuondoka katika wodi ya upasuaji aliyokuwa amelazwa na amеruhusiwa kwenda nyumbani.

"Afya yake inazidi kuimarika na tumemruhusu kwenda nyumbani baada ya madaktari waliokuwa wakimtibu kujiridhisha kwamba anaweza kula na kuanza mazoezi. Tunawasiliana nae tangu Ijumaa na anaendelea vizuri,"alisema Dk. Juma Wiki iliyopita, Mwenyekiti wa Chama cha Wafugaji,

Kanda ya Kaskazini (CCWT), Lekey Ole Milakoni ambaye pia ni Katibu wa Baraza la Wazee wa Mila wa jamii ya wafugaji wa Kimasai (Maleigwanani), alisema kwa mujibu wa mashuhuda wa tukio hilo pamoja na baadhi ya wafugaji wenyewe, kuna utata kuhusu tukio hilo kwa vile Cheyavyo, anadaiwa kupigwa risasi akiwa katika makazi ya watu.

SALIMIANA



Mbunge wa Viti Maalum mkoa wa Manyara, Ester Mahawe, akizungumza na aliyekuwa Diwani wa Kata ya Bagara Mjini Babati, Andrew Ombay kwa mwaka 2010/2015. Kushoto ni aliyekuwa diwani wa kata hiyo 2015/2020, Nicodemus Tlaghasi (aliyekuwa Chadema akajiunga na CCM) ambaye ameshinda kura za maoni kwa kupata kura 57, dhidi ya Ombay aliyepata kura 35 kwenye uchaguzi wa chama hicho uliofanyika juzi. **PICHA: GIFT THADEY**

# Askofu ahamasisha bima ya afya

**Na Godfrey Mushi,** MOSHI

ASKOFU mstaafu wa Dayosisi ya Kaskazini ya Kanisa la Kiinjili la Kilutheri Tanzania (KKKT), Dk. Martin Shao, ameanzisha kampeni maalum ya kuhamasisha kila familia na ngazi ya kaya katika kila koo, kujiunga na Mfuko wa Taifa wa Bima ya Afya (NHF) ili kukabiliana na changamoto ya afya.

Alikuwa akizungumza jana kwenye mkutano mkuu wa mwaka wa wanafamilia wa ukoo wa Shao unaojumuisha mababu zao kutoka familia za Kalachu, Kimengechi, Mosi na Kiwong'a.

"Kuna gharama kubwa sana za kupata huduma za tiba katika hospitali zetu na sio kila wakati mtu unakuwa na fedha za kugharamia matibabu hasa kipindi hiki ambacho fedha ni changamoto. Kwa hiyo, tumepitisha katiba itakayotubana, sasa kila familia, kaya tumekubaliana kwa pamoja kwamba ukoo huu, tutakuwa na kadi za bima ya afya hadi kufikia mwezi Julai mwaka 2019," alisema Dk. Shao.

Alitaka katika kampeni hiyo, watambue kwamba bima ni jambo muhimu na la msingi kwa kila mtu, inasaidia kupunguza umaskini kwenye familia, kwa kuwa nguvu na akili inaelekezwa sasa kwenye uzalishaji na siyo kutafuta fedha kwa ajili ya matibabu na hakuna mbadala wa afya ya binadamu.

Kwa mujibu wa Askofu huyo mstaafu, maendeleo mazuri ya afya ya mtu ni pamoja kuwa na uhakika wa kupata matibabu akiugua au kupata ajali na bima ya afya ni njia mojawapo inayomuhakikishia mtu kupata huduma za afya wakati wowote na mahali popote pasipo kujali hali ya kipato chake.

Zaidi alisisitiza kuwa, idadi ya wananchi wanaomiliki bima ya afya ni wachache, ikilinganishwa na wale wanaotumia gharama kubwa kupata matibabu katika hospitali mbalimbali ikiwamo Hospitali ya Rufani ya KCMC.

Pamoja na mambo mengine, askofu huyo alihimiza koo hizo kuitafakari upya dhana ya usharika na kujikita katika kuanzisha miradi itakayowakwamua kiuchumi hasa kwa kuanza kujenga miundombinu ya kuziwezesha kaya zao kiuchumi.

"Ni vizuri tukaanza kujifunza kufanya kazi za kuibua miradi mbalimbali itakayoingiza kipato katika kila familia kama wanavyofanya mchwa au siafu na tujenge mazingira ya kusaidiana. Natamani sana tuonyeshe mfano kwenye koo nyingine kwa kupeleka watoto shule," alisisitiza.

Kuhusu changamoto ya vijana kutozingatia maadili kwa kujihusisha na vitendo vya ujambazi, wizi, ulevi na kutotunza familia yake, Dk. Shao alisema kwa koo hizo wamekubaliana kwa pamoja kwamba ni marufuku kwa watoto wao kujihusisha na ikigundulika wanatengwa na ukoo.

# Kesi madai ya utapeli yakwama

**Na Paul William,** MOSHI

KESI ya kujipatia fedha zaidi ya Sh. milioni 500 kwa njia ya utapeli kutoka kwa mfanyabiashara mmoja wa mji wa Moshi ambayo inawakabili watu sita, ilishindwa kuendelea katika Mahakama ya Hakimu Mkazi Moshi, baada ya jalada la shauri hilo kupelekwa kwa Jaji Mfawidhi wa Mahakama Kuu, Kanda ya Moshi.

Jalada hilo limepelekwa kwa Jaji Aishiel Sumari, baada ya kuliitisha kutoka kwa Hakimu Mkazi, Pamela Mazengo ambaye kesi hiyo iko mbele yake kwa sasa.

Taarifa ya kupelekwa kwa jalada hilo kwa Jaji huyo, ilitolewa mahakamani hapo na Wakili wa Serikali, Verediana Mleza.

Kabla ya kutolewa kwa taarifa hiyo, Wakili huyo alidai kuwa kesi hiyo inayohusisha makosa 11 likiwamo la uhujumu uchumi ilikuja kwa ajili ya kutajwa.

Baada ya taarifa hiyo, Hakimu Mazengo alisema kuwa washtakiwa hao hawatakiwi kujibu lolote kwa kuwa mahakama hiyo haina uwezo wa kusikiliza shauri hilo na baadaye kuahirisha kesi hiyo hadi Julai 20, mwaka huu itakapotajwa tena na washtakiwa wote kurudishwa mahabusu.

Washtakiwa hao Salim Maua, Leonard Nicholaus, Emanuell Roman, James Matei, Eptas Steven na Jonhson Godfrey wanatetewa na Wakili Majura Magafu.

Inadaiwa kuwa, kwa nyakati tofauti kati ya Aprili mwaka 2017 hadi Aprili mwaka 2018, washtakiwa hao wanatuhumiwa kutenda kosa la kutakatisha fedha, ambapo walikuwa wakichukua fedha kwa viwango tofauti kutoka kwa mfanyabiashara Rose Temba, huku wakitambua kuwa ni kosa kisheria.

Hata hivyo, wakati taarifa hiyo ikitolewa mahakamani hapo, wakili wa utetezi, Magafu, hakuwapo kutokana na kile kilichoelezwa kwamba yupo Mahakama ya Rufani.

Awali, kabla ya kuahirishwa shauri hilo, mshtakiwa wa pili Leonard Nicholaus alinyoosha kidole na kuiomba mahakama hiyo kuiamuru Jamhuri kubadili hati ya mashtaka, kwa kuwa muda mrefu umepita bila hoja hiyo kutolewa ufafanuzi.

Nipashe
# Spotika
NIPASHE JUMATATU JULAI 9, 2018



USAJILI UNAVYOTINGISHA BONGO UK.18

## NDIYO ZANGU



Beki wa kati wa England, John Stones, akiucheza mpira dhidi ya kiungo mshambuliaji wa Sweden, Ola Toivonen, katika mechi ya robo fainali ya Kombe la Dunia iliyopigwa katika Uwanja wa Samara, Urusi juzi na England kushinda 2-0. **HABARI UK. 29**

ISIKUPITE

### SOKA LINARUDI NYUMBANI?

Mwaka 1966
- Man City ilitwaa Ubingwa wa Ligi
- Burnley ilifuzu michuano ya Ulaya
- Chelsea ilimaliza nafasi ya 5 kwenye Ligi
- Real Madrid ilitwaa Ubingwa wa Ulaya
- England ilitwaa Kombe la Dunia

Mwaka 2018
- Man City imetwaa Ubingwa wa Ligi
- Burney imefuzu michuano ya Ulaya
- Real Madrid imetwaa Ubingwa wa Ulaya
- England?

MICHEZO



# PICKFORD;

## SULUHISHO 'MATOBO' LANGO LA ENGLAND

**MOSCOW,** Urusi

LABDA anaweza kuwa mdogo kwa kimo, lakini Jordan Pickford anajitengenezea jina kubwa yeye binafsi kwenye Kombe la Dunia kufuatia kipa huyo wa Everton kuokoa michomo mitatu ya hatari ambayo ingeweza kuizamisha England dhidi ya Sweden, hivyo kuisaidia timu yake hiyo kutinga nusu fainali ya michuano hiyo kwa mara ya kwanza katika kipindi cha miaka 28.

Ikiwa ndiyo kwanza ana mechi nane tu mkononi za kimataifa, Pickford amekuwa kipa kinda zaidi England kuweza kumaliza mechi bila kuruhusu bao ('clean sheet') kwenye Kombe la Dunia, kazi kubwa akiifanya kwa kuokoa mchomo wa Marcus Berg na Viktor Claesson juzi.

Kwa mechi hiyo ambayo England ilitawala sehemu kubwa ya mchezo wakati wakishinda 2-0, ukweli Pickford alitangazwa mchezaji bora wa mechi kwa mchango wake wa kuwahakikisha 'Three Lions' wanahusika katika hatua ya nusu fainali.

Ilikuwa ni kazi nyingine ya kuvutia juzi ikiwa ni baada ya kipa huyo mwenye umri wa miaka 24, kutokea kuucheza mkwaju wa penalti wa Carlos Bacca wa Colombia na kuisaidia England kutinga hatua ya robo fainali ya Kombe la Dunia kwa mikwaju ya penalti 4-3.

"Hivi ndivyo soka lilivyo kwa ujumla, kuwa katika hatua kubwa," alisema Pickford. "Sijiweki mwenyewe katika presha yoyote, Ninaukubali wakati huo na kucheza wakati huu.

"Hakuna chohote kinachonisababishia, nyasi mara zote zinakuwa zile zile, mistari ile ile, urefu wa magoli ule ule, ni mechi tu ya soka."

Hata hivyo, kwa nchi ambayo ina hazina kubwa ya makipa, kulikuwa na hofu kubwa kuhusu ni kipa gani Gareth Southgate atamchagua katika safari hiyo ya Urusi.

Joe Hart alianza safari hiyo kwa kucheza mechi za kufuzu, lakini Southgate alizingatia kukosa ubora kwa kipa huyo wakati akicheza kwa mkopo West Ham na kujikuta akikosa nafasi kikosini jumla.

**Southgate amchambua**

Kigezo kikubwa cha Southgate kufanya uamuzi wa kumpa nafasi Pickford siyo tu kutokana na ubora wake wa kuokoa michomo langoni, bali pia ni kutokana na mchango wake kwa mabeki.

"Usambazaji wa Pickford ulikuwa mzuri sana ukoaji wake dakika ya 20 ulikuwa muhimu," alisema Southgate. "Ni mfano wa namna kipa wa kisasa anapaswa kuwa."

Kwa kipa ambaye ni kinda sana kama yeye, Pickford pia ameonyesha uimara mkubwa licha ya kukosolewa kwa bao la Adnan Januzaj ambalo liliipa Ubelgiji ushindi wa 1-0 hivyo kuongoza Kundi G.

**Courtois amkubali**

Kipa wa Ubelgiji, Thibaut Courtois, alionekana kuhoji kimo cha Pickford, kwa mlinda mlango bora kuwa na futi sita na inchi moja (6ft 1ins) sawa na mita 1.85. Lakini baadaye kipa huyo wa Chelsea alikiri kuwa ni shabiki mkubwa wa Pickford.

"Kamwe sikudharau kimo chake, ni kipa mzuri. Ninapenda kuweka hilo wazi," Courtois alisema baada ya kuonyesha kiwango cha juu dhidi ya Brazil na kuisaidia Ubelgiji kutinga nusu fainali.

"Kamwe siwezi kufanya hivyo kwa kipa mwingine, nilikuwa nikimaanisha kuwa na urefu wa sentimeta 15, ningeweza kufikia mpira," Courtois alisema.

Pickford kukosa urefu, kunamfanya kuwa na kasi kulizunguka goli.

**Pickford afunguka urefu**

"Sijali kama sina umbo kubwa," alisema Pickford. "Nimekuwa na nguvu hiyo na uwezo wa kuzunguka goli. Ni mzuri sana katika hilo."


Sweden ilishuhudia namna alivyo bora wakati England ikitinga nusu fainali na sasa itaivaa Croatia Jumatano.

**JE, WAJUA?**

Mabao yote ya Marouane Fellaini aliyoifungia Ubelgiji kwenye Kombe la Dunia, amefunga kwa kichwa.

# MICHEZO

## NJE YA UWANJA



### Griezmann akitupia Ufaransa haipotezi

UFARANSA haijawahi kupoteza mechi yoyote kati ya 20 ambazo Antoine Griezmann alifunga bao; imeshinda 18 na kutoka sare mbili (W18 D2). Kadhalika, Griezmann amefunga mabao saba katika mechi sita alizocheza kwenye hatua ya mtoano ya michuano mikubwa.



### Kane tishio England akivaa kitambaa

Harry Kane amefunga mabao 14 katika mechi 11 alizoichezea England chini ya kocha Gareth Southgate, huku pia akishindwa kutupia kwenye mechi moja tu (dhidi ya Sweden juzi)kati ya tisa alizocheza akiwa amevaa kitambaa cha unahodha (na ametupia jumla ya mabao 12).



### Varanes yeye kwa kichwa tu

BAO alilofunga Raphaël Varanes dhidi ya Uruguay kwenye hatua ya robo fainali ya Kombe la Dunia, ni la tatu kwake kuifungia Ufaransa, na yote matatu amefunga kwa kichwa.



Juma Kaseja

# Makipa hawa ujipange unapopiga penalti

**Na Adam Fungamwango**

KWENYE fainali za Kombe la Dunia, tumeona baadhi ya timu zikifurushwa kwenye hatua ya 16-Bora kwa mikwaju ya penalti.

Kadhalika tumeona baadhi ya makipa wakizibeba timu zao kwa kuokoa michomo ya penalti.

Wakati hayo yakiendelea, Kombe la Kagame linaendelea kwenye hatua za mtoano na huenda baadhi ya mechi zikaamuliwa kwa kupigiana penalti.

Tunaweza kuona makipa wakifanya vitu vyao kwa kucheza penalti kama tunavyoona mwaka huu kwenye Kombe la Dunia.

Nchini, pia kuna makipa ambao si rahisi kuwafunga penalti zote tano.

Na si hivyo tu, hata ikipatikana penalti wakati wa mchezo, inabidi mpigaji awe mwangalifu kwani inaweza kuokolewa...

**1. Deogratius Munishi 'Dida'**

Huyu anaweza kuwa msaada mkubwa kwa Simba kwenye michuano ya Kombe la Kagame, kama timu hiyo itakuwa imeingia hatua ya nusu fainali jana usiku.

Amesajiliwa hivi karibuni akitokea Afrika Kusini alikokuwa akicheza soka la kulipwa. Awali alikuwa akiichezea Yanga.

Kipa huyu wa zamani wa klabu za Simba, Mtibwa na Azam, ni mzuri mno wa kudaka penalti.

Mfano alipokuwa Yanga wakati mwingine alikuwa akiibeba timu hiyo inapofika hatua hiyo. Alikuwa hafungwi penalti zote tano hata kama Yanga itatolewa. Aliwahi kuibeba Yanga kwenye mabega yake na kuiingiza hatua ya makundi ya Ligi ya Mabingwa Afrika alipookoa penalti iliyotolewa dakika za mwisho nchini Angola dhidi ya Sagrada Esperanca.

**2. Juma Kaseja**

Ni kipa mkongwe ambaye hadi sasa bado anaonekana ana uwezo mkubwa wa kucheza penalti.

Itakumbukwa kuwa kwenye mechi ya mwisho wa ligi akiichezea Kagera Sugar dhidi ya Simba, aliokoa penalti ya mpigaji stadi wa Simba, Emmanuel Okwi.

Kaseja anajulikana tangu enzi akiwa kwenye klabu ya Simba kuwa pamoja na kuwa ni kipa bora, lakini alikuwa na uwezo mkubwa wa kucheza mikwaju ya penalti, akiwa ni mrithi sahihi wa Mohamed Mwameja. Alishawahi kudaka penalti zilizoiingiza Simba kwenye hatua ya makundi Ligi ya Mabingwa Afrika mwaka 2003. Msimu unaofuata ataidakia KMC.

**3. Aishi Manula**

Huyu ndiye kipa namba moja wa Simba kwa sasa. Naye pia ni mtaalam linapokuja suala la penalti. Iwe za ndani ya dakika 90 au zile tano-tano ni lazima mpigaji awe makini.

Amekuwa na rekodi nzuri ya kucheza penalti na ni mmoja wa makipa ambaye si rahisi kumfunga penalti yoyote ile tangu akiwa Azam mpaka sasa Simba.

**4. Manyika Peter**

Ni kipa chipukizi aliyeibukia kwenye kikosi cha pili cha Simba.

Kwa sasa anaichezea Singida United. Naye si mbaya kwenye kuokoa mikwaju ya penalti. Utakumbuka kwenye michuano ya Super Cup nchini Kenya alivyofanya mambo, kiasi cha Wakenya wengi kuanza kuwaogopa makipa wa Tanzania linapokuja suala la penalti kutokana na yeye pamoja na Manula kuwa vinara.

**5. Said Mohamed Nduda**

Ingawa kwa sasa inaonekana hana maisha marefu ndani ya Simba, lakini ni mmoja wa makipa ambaye ni wazuri kwenye kucheza mikwaju ya penalti. Utakumbuka ndiye kipa bora kwenye mechi za COSAFA mwaka jana alipocheza mechi ya kutafuta mshindi wa tatu, akaokoa magoli mengi, ikiwa ni kudaka mikwaju ya penalti na kuipa Taifa Stars ushindi wa tatu.

## NUKUU

"Tunajua kuna mechi ngumu mbeleni katika nusu fainali, lakini tunajisikia vizuri na tunajiamini. Tutakwenda tena. Tunalifurahia hilo na tunaendelea kufanya tunachokifanya na kulipa taifa letu fahari," **alisema Harry Kane baada ya kutinga nusu fainali kwa kuichapa Sweden mabao 2-0 juzi.**



"Hii haikuwa mechi nzuri, ilikuwa ni mapigano, vita vya nusu fainali, hatutaki kuvisitisha, tutajaribu kucheza mchezo wetu bora (dhidi ya England). Tuna mechi mbili za kucheza na tumehamasika sana, tunajitoa kwa kila kitu, itakuwa ni vita tena lakini tunaimani, nina imani kwa upande wetu," **alisema kocha wa Croatia, Zlatko Dalic, baada ya timu yake kutinga nusu fainali ya Kombe la Dunia kwa mara ya kwanza tangu mwaka 1998, kwa kuitoa Urusi kwa penalti 4-2, kufuatia sare ya 2-2 baada ya dakika 120 juzi.**



"Ni mwenye fahari sana duniani, kwa sababu nimewapa wachezaji zoezi la mbinu ngumu sana na kwa namna walivyoamini hadi dakika ya mwisho ilikuwa jambo la kushangaza. Wamefanya kitu cha kipekee na ninatumai kila mmoja Ubelgiji anajisikia fahari sana. Lakini kwa sasa tunahitaji nguvu zaidi kujaribu kuhakikisha tunakuwa wazuri nusu fainali," **Kocha wa Ubelgiji, Roberto Martinez, baada ya kuichapa Brazil mabao 2-1 kwenye mechi ya robo fainali ya Kombe la Dunia.**



# MABEKI 10 WAKUMSAIDIA VAN DIJK LIVERPOOL



Van Dijk

**LIVERPOOL,** England

LIVERPOOL inatarajia kusajili beki mwingine wa kati majira haya ya joto, na kocha Jurgen Klopp ana mibadala kibao ya kuitazama ili kuimarisha safu yake ya ulinzi.

'Majogoo wa Anfield' wataenda sokoni wakihitaji beki mwingine wa kati atakayeshirikiana vema na Virgil van Dijk, na Dejan Lovren, Joel Matip na Joe Gomez wote wamekuwa wakisumbuliwa na majeraha, wakati Ragnar Klavan Oktoba mwaka huu atatimiza miaka 33.

Kutua kwa Van Dijk kulileta mabadiliko katika safu ya ulinzi ya Liverpool, ingawa bado Klopp amekuwa akimuona Lovren kama beki wa kiwango cha juu duniani, lakini swali linabaki kuhusu kubeba majukumu kwa muda mrefu.

Iwe, pacha wa Van Dijk, anakuja ni jambo la kusubiri kuona, lakini hapa kuna mabeki 10 bora ambao wanaweza kuwa mbadala sahihi Liverpool au klabu nyingine zilizopo sokoni kusaka beki wa kati...

### 10. JAMAAL LASCELLES

**Umri:** Miaka 24
**Klabu:** Newcastle United
**Uraia:** Uingereza

Lascelles ni beki imara ambaye ameenda hewani vema, mwenye uwezo mkubwa dimbani na aliyejizatiti kwa umiliki wa mpira, na kama kiongozi asilia, anaweza kuhimili changamoto Anfield.

Licha ya kutojumuishwa kwenye kikosi cha England katika Kombe la Dunia, Lascelles anaweza kuwa tayari kuingia katika kikosi cha Klopp tayari kwa kujiandaa na msimu mpya, na tayari yupo kwenye rada za Liverpool kwa mujibu wa Gazeti la Independent.

**Uwezekano:** Bado ana majukumu 'Magpies', lakini kama akipigiwa simu ataikataa Liverpool?

### 9. JAMES TARKOWSKI

**Umri:** Miaka 25
**Klabu:** Burnley
**Uraia:** Uingereza

Liverpool inaweza kuhitaji kuongeza wazawa katika usajili wa majira haya ya joto endapo Danny Ward na Danny Ings wataondoka, hivyo Tarkowski anaweza kuwa muwaniwa sahihi katika kigezo hicho.

Kama ilivyo kwa Lascelles, tayari naye ameshahusishwa na Liverpool na ni beki ambaye anaweza kuendelea vema akicheza pembeni ya Van Dijk.

**Uwezekano:** Liverpool itakuwa hatua moja juu kwake katika kupata nafasi ya kucheza mara kwa mara kikosi cha England.

### 8. JONATHAN TAH

**Umri:** Miaka 22
**Klabu:** Bayer Leverkusen
**Uraia:** Ujerumani

Tah kwa muda mrefu amekuwa akielezwa kama mchezaji anayewezekana kuwindwa na Liverpool, na kuna sababu za kuridhisha kwa nini; kwa umri wake tu wa miaka 22, tayari amekuwa staa Bundesliga kwa kipindi cha miaka mitatu na nusu.

Kujengeka kimwili kumemfanya kusimama vema katika safu ya ulinzi, lakini soka lake limezidi kuimarika na anaweza vema kusaidiana na Van Dijk.

**Uwezekano:** Ukichukulia amesaini mkataba wa muda mrefu hivi karibuni, itakuwa ni vigumu kupatikana.

### 7. KOSTAS MANOLAS

**Umri:** Miaka 26
**Klabu:** AS Roma
**Uraia:** Ugiriki

Manolas alikuwa na wakati mgumu Roma ilipopoteza kwa mabao 5-2 dhidi ya Liverpool kwenye hatua ya nusu fainali ya Ligi ya Mabingwa Ulaya katika Uwanja wa Anfield, lakini kipigo hicho kilihitaji mbinu zaidi za kufanya kwa kocha Eusebio Di Francesco.

Lakini hili haliwezi kuharibu wasifu wake, hasa ukizingatia Mgiriki huyu ni beki wa kati wa kiwango cha juu na tayari amezivutia timu kama Real Madrid na Napoli.

**Uwezekano:** Makato makubwa ya 'kodi kwa Salah' yanaweza kuzuia mazungumzo, lakini anaweza kuwa na thamani.

### 6. KALIDOU KOULIBALY

**Umri:** Miaka 26
**Klabu:** Napoli
**Uraia:** Senegal

Koulibaly alikuwa katika rada za Liverpool majira ya joto yaliyopita, akitazamwa kama mbadala wa Van Dijk, lakini baada ya msimu mwingine wa kuvutia akiwa Napoli, beki huyu mwenye kimo cha futi sita na inchi tano (6'5"), huku akiwa mwingi wa mbinu, anapaswa kutazamwa tena.

Ingawa kiasili anacheza kama beki wa kati kushoto kama ilivyo kwa Lovren, anaweza pia kucheza kulia na kuwa pacha sahihi wa Van Dijk.

**Uwezekano:** Chelsea na Barcelona ni miongoni mwa klabu zinazohitaji saini yake, jambo ambalo linaongeza ugumu wa uhamisho wake.

### 5. MATTHIJS DE LIGT

**Umri:** Miaka 18
**Klabu:** Ajax
**Uraia:** Uholanzi

De Ligt ni kipaji cha shule ya makinda ya Ajax, na kutokana na majukumu mazito anayobeba, yamemfanya kuwindwa na klabu kubwa.

Tayari ameshaanza mara kadhaa katika kikosi cha kwanza cha Uholanzi akicheza sambamba na Van Dijk chini ya kocha Ronald Koeman na ameelekeza mawazo yake katika kuondoka majira haya ya joto, ingawa Liverpool inaweza kukabiliwa na upinzani mkubwa kutoka kwa kilabu kubwa Ulaya.

**Uwezekano:** Hakuwezi kuwa na wahitaji wachache wa huduma yake, na pengine Van Dijk anaweza kufanikisha kupatikana kwake.

### 4. BENJAMIN PAVARD

**Umri:** Miaka 22
**Klabu:** Stuttgart
**Uraia:** Ufaransa

Alihusishwa na kutua Merseyside, Mkurugenzi wa Michezo wa Stuttgart, Michael Reschke, alidai kuwa bado Pavard ni wazo lao, lakini akakubali kuwa hawawezi kuzuia usajili mkubwa kumshukia.

Inaweza kuelezwa kuwa tayari ameshaimarika katika kikosi hicho akicheza Bundesliga, akicheza soka la akili sana na ni kiraka, lakini akicheza zaidi kama beki wa kulia.

**Uwezekano:** Ni nyota wa baadaye wa Ufaransa, lakini Liverpool kama itampata mapema italeta maana.

### 3. CAGLAR SOYUNCU

**Umri:** Miaka 22
**Klabu:** Freiburg
**Uraia:** Uturuki

Soyuncu aliibuka kuwa kama beki anayewindwa na Liverpool, kufuatia taarifa kwamba walikuwa wakiwinda kinda kutoka Uturuki hivi karibuni wakati wakitoka sare ya bao 1-1 Urusi, lakini Arsenal nayo hivi karibuni iliripotiwa kuulizia dau la pauni milioni 35 zinazohitaji ili kumpata.

Utamu zaidi ni kwamba, Soyuncu ni mtumiaji wa miguu yote miwili dimbani na ambaye anaweza kucheza vema nafasi ya beki wa kati sambamba na Van Dijk.

**Uwezekano:** Kama kutakiwa huko ni kweli, anaweza kuwa lengo linaloweza kufikia.

### 2. YERRY MINA

**Umri:** Miaka 23
**Klabu:** Barcelona
**Uraia:** Colombia

Mei mwaka huu Liverpool walihusishwa na kuhitaji huduma ya beki huyu kwa mkopo, anayeonekana kutohitajika Barcelona, miamba ya La Liga wanaonekana kutaka kumuacha aondoke katika kikosi hicho cha Ernesto Valverde.

Mina ni aina ya beki ambaye anaweza kufiti vizuri Anfield, na kama anaweza kuongeza umakini wake kutokana na umbo lake la asili na nguvu za kiufundi kunaweza kuipa Liverpool mbadala sahihi katika safu yake ya ulinzi.

**Uwezekano:** Barca inaonekana kutaka kuachana naye, hivyo atakuwa rahisi kupatikana.


### 1. DAYOT UPAMECANO

**Umri:** Miaka 19
**Klabu:** RB Leipzig
**Uraia:** Ufaransa


Mbali ya Pavard, Upamecano anachukuliwa kama mmoja wa mabeki bora matarajio ya Ufaransa, na tayari kinda huyo ameonyesha ubora wake tangu alipojiunga na Leipzig.

Matatajio mengine yaliyopo ni kwamba Upamencano kwa sasa bado anacheza vizuri licha ya umri wake na anaweza kutinga moja kwa moja Liverpool na kucheza beki namba nne zaidi kama Davinson Sanchez anavyofanya Tottenham.

**Uwezekano:** Itategemea endapo Leipzig bado inamuwinda kutokana na dili la Keita.




Lascelles




Tarkowski



Tah




Manolas




Koulibaly




De Ligt




Pavard



Soyuncu



Yerry Mina



Upamecano

## Michezo

# USAJILI UNAVYOTINGISHA BONGO

**Na Adam Fungamwango**

WAKATI michuano ya Kombe la Dunia inaendelea nchini Urusi, Kombe la Kagame pia likirindima nchini, barani Ulaya mambo ya usajili yamekuwa yakiendelea kama kawaida.

Nchini pia mambo ni hivyo hivyo, usajili umekuwa ukipamba moto.

Kila klabu inasaka wachezaji ambao inaona kuwa itawasaidia kwenye msimu mpya wa Ligi Kuu Tanzania Bara 2018/19.

Tayari Shirikisho la Soka nchini (TFF), limeshafungua dirisha la usajili tangu Juni 15 na linatarajiwa kufungwa Julai 26, mwaka huu.

Wafuatao ni wachezaji kutoka ndani na nje ya nchi ambao tayari wameshatua kwenye klabu mpya na kuthibitishwa rasmi.

**1. Donald Ngoma-Azam FC**
Straika huyu hatari wa zamani wa Yanga raia wa Zimbabwe, ametua kwenye klabu ya Azam FC. Ingawa imeelezwa bado ana majeraha, lakini wakati ligi itakapokuwa imeanza atakuwa amebakisha wiki chache kati ya zile alizotakiwa kupumzika kwa mujibu wa madaktari wake.

**2. Tafadza Kutinyu-Azam FC**
Ni Mzimbabwe mwingine aliyetua kwenye klabu ya Azam FC kwa ajili ya msimu ujao wa Ligi Kuu. Huyu naye si mgeni sana masikioni mwa mashabiki wa soka, kwani msimu uliomalizika alikuwa akiichezea Singida United.

**3. Meddie Kagere-Simba**
Ni mzaliwa na Uganda mwenye uraia wa Rwanda. Ni mmoja wa mastraika hatari kwenye ukanda huu wa Afrika Mashariki na Kati.

Straika huyo amesajiliwa na klabu ya Simba akitokea Gor Mahia ya Kenya. Ameanza kuonyesha cheche zake kwenye michuano ya Kagame inayoendelea.

**4. Tiba John-Singida United**
Anacheza kama kiungo wakati mwingina straika. Msimu uliomalizika alikuwa akiichezea Ndanda FC. Lakini msimu ujao wa ligi mashabiki watamuona akiwa ametinga uzi wa timu ya Singida United. Tayari ameanza kung'ara kwenye Kombe la Kagame.




Mastraika wapya wa Simba waliosajiliwa hivi karibuni, Meddie Kagere (kushoto) na Adam Salamba (kulia), kwenye moja ya mechi za Kombe la Kagame linaloendelea. **PICHA: MAKTABA**

**5. Adam Salamba-Simba**
Msimu uliomalizika alichezea timu mbili. Nusu msimu wa kwanza alikuwa na Stand United, kabla ya kujiunga na Lipuli kwenye mzunguko wa pili wa Ligi Kuu iliyomalizika.

Kwa sasa amesajiliwa na Simba kwa ajili ya msimu ujao. Ameshaanza kuichezea timu hiyo kwenye michuano mbaliambali; ya SportPesa Super Cup nchini Kenya na Kagame Cup inayoendelea nchini.

**6. Juma Kaseja-KMC**
Ni kipa wa zamani wa klabu za Simba na Yanga na hata Mbeya City. Msimu uliomalizika alikuwa akiidakia Kagera Sugar na kufanya vizuri.

Mkongwe huyo kuelekea msimu ujao amesajiliwa na timu iliyopanda daraja msimu huu ya KMC ya Kinondoni.

**7. Eliuter Mpepo-Singida United**
Huyu alikuwa ni straika tegemeo kwenye timu ya Prisons ya Mbeya.

Kwa sasa amejiunga na Singida United na tayari ameanza kuichezea timu hiyo kwenye michuano ya Kombe la Kagame.

**8. Yusuph Ndikumana-KMC**
Klabu ya KMC iliendelea kushangaza wengi, kwani baada ya kumsajili Kaseja, ikamsajili beki kisiki wa Mbao FC, Yusuph Ndikumana. Msimu uliopita timu za Simba na Yanga zilishindwa kumsajili kutokana na dau lake kuwa kubwa.

**9. Habib Kyombo-Singida United**
Alitwaa tuzo ya straika kijana kwenye Ligi Kuu Tanzania Bara. Msimu huu amejiunga na Singida United, akitokea Mbao FC. Ni mmoja wa mastraika hatari na tegemeo baadaye nchini.

**10. Sadala Mohamed-KMC**
Ni beki aliyekuwa akiitumikia Mbao FC, lakini kwa sasa tayari ameshatua kwenye klabu ya KMC kwa ajili ya kuichezea Ligi Kuu Tanzania Bara msimu ujao wa ligi.

**11. Mohamed Rashid-Simba**
Alikuwa straika wa kutumainiwa na Prisons ya Mbeya msimu uliomalizika. Msimu huu amejiunga na mabingwa wapya Simba na tayari wanachama na mashabiki wa timu hiyo wameshamshuhudia kwenye mechi mbalimbali, zikiwamo za Kombe la Kagame.

**12. Marcel Kaheza-Simba**
Alikuwa na msimu mzuri uliomalizika, akiichezea timu ya Majimaji ya Songea. Msimu ujao ataonekana akiwa amevaa uzi wa Simba.

Tayari wanachama na mashabiki wa timu hiyo wameshaanza kumshuhudia kwenye michuano ya Kombe la Kagame.

**HAIKUHUSU**

Jumla ya mabao sita yaliyofungwa na Japan kwenye fainali za Kombe la Dunia Urusi 2018, ndiyo idadi kubwa zaidi kwa timu hiyo kuwahi kufunga kwenye michuano hiyo tangu ianze kushiriki.



# HAZARD? MBONA MESSI AMEKUBALI




**MOSCOW,** Urusi

UFARANSA tayari imewatoa mabingwa wawili wa zamani wa Kombe la Dunia katika hatua ya mtoano, lakini bado ipo mbali kufikia ubora wake, kwa mujibu wa kocha wa timu hiyo, Didier Deschamps, wakati huu wakijiandaa kuivaa Ubelgiji kwenye mechi ya nusu fainali.

Baada kupenya kivivu hatua ya makundi, Ufaransa iliichapa Argentina mabao 4-3 wakati ikianza hatua ya mtoano (16-Bora) na kisha kuichapa Uruguay 2-0 kwenye robo fainali.

"Tulitatanisha raundi ya kwanza bila ya kujiamini kinidhamu, lakini wenye ufanisi. Ila kuanzia mechi dhidi ya Argentina, tulikuwa imara," alisema .

"Tulikuwa bora dhidi ya Uruguay, lakini bado kuna kutokuwa makini. Tuna mengi zaidi ya kuonyesha."

Deschamps pia anafurahia kikosi chake chenye wachezaji wenye wastani wa umri wa miaka 26, kuonyesha ukomavu katika michuano hiyo, ambapo kilitua Urusi kikiwa cha pili kwa kuwa na wachezaji wenye umri mdogo zaidi.

"Nina kikosi kinachoundwa na makinda kwa sasa tunafanya kazi kama timu. Unaweza kuona upana wa uelewa wao na kumekuwa na maendeleo mengi," alisema Deschamps ambaye alicheza nafasi ya kiungo wakati Ufaransa ikitwaa taji hilo mwaka 1998.

Hata hivyo, wakati Deschamps, akishuka na mistari hiyo, beki wa kushoto wa timu hiyo, Lucas Hernandez, anaamini hawana cha kuhofia mbeleni katika michuano hiyo baada ya kumzuia Lionel Messi na kuitupa Argentina nje.

Hernandez anamtaja Eden Hazard na Romelu Lukaku kama wachezaji hatari kutokana na uzoefu wao kwenye Premier League.

"Tayari tumeshamtoa mchezaji bora duniani [Messi] dhidi ya Argentina," beki huyo wa kushoto wa Atletico Madrid, ambaye pia anaweza kucheza kama beki wa kati aliwaambia wanahabari.

"Hakugusa mpira. Huo ndio ukweli.

"Dhidi ya Ubelgiji pia kuna wachezaji wa kuhakikisha hawagusi mpira, Hazard aguse mpira mara chache kadri iwezekanavyo."

Kuna uwezekano, Hernandez kuunda safu ya ulinzi ya mabeki wa nne ya Ufaransa pamoja na Benjamin Pavard, Raphael Varane na Samuel Umtiti, ambaye alisumbuliwa kidogo na majeraha ya goti.

Varane, alifunga bao la kwanza la Ufaransa dhidi ya Uruguay, hivyo kuna imani kwamba umoja wao na kujiamini utaizimisha safu ya ushambuliaji ya Ubelgiji.

"Hazard ni mchezaji mwenye kipaji kikubwa, akiwa na kasi kubwa na ubora wa hali ya juu," alisema.

"Hakuna suluhisho la muujiza dhidi yake. Unapaswa kumpa fursa ndogo ya nafasi.

"Lukaku anaweza kufanya mambo kuwa magumu kwa sababu ya utimamu wake kimwili. Anayo wachezaji wazuri wanaomzunguka, lakini na sisi tunao pia. Tunaweza kuwaumiza mbele."

## NDANI YA 18

Timu zote nne zilizoingia katika changamoto ya mikwaju ya penalti Kombe la Dunia Urusi 2018, kila iliyoanza kupiga penalti ilitolewa.



Nipashe
Spotika



LIVERPOOL inatarajia kusajili beki mwingine wa kati majira haya ya joto, na kocha Jurgen Klopp ana mibadala kibao ya kuitazama ili kuimarisha safu yake ya ulinzi. 'Majogoo wa Anfield' wataenda sokoni wakihitaji beki mwingine wa kati atakayeshirikiana vema na Virgil van Dijk, na Dejan Lovren, Joel Matip na Joe Gomez wote wamekuwa wakisumbuliwa na majeraha, wakati Ragnar Klavan Oktoba mwaka huu atatimiza miaka 33..

**Uk. 16-17**



# MBAPPE AGEUZWA KOSA LA ZIDANE REAL

**MADRID,** Hispania

REAL Madrid itamshukuru Zinedine Zidane milele kwa kuiwezesha kupiga hatua baada ya kutwaa mikoba ya Rafa Benitez aliyevurunda, na zaidi kutwaa taji la Ligi ya Mabingwa Ulaya na ubingwa wa La Liga na kuondoka kama shujaa, lakini alifanya kosa kubwa kwa kushindwa kutoa msukumo wa kusajiliwa kwa Kylian Mbappe.

Kunaweza kusiwe na malalamiko yoyote kuhusu namna Mfaransa huyo alivyofanya kazi yake ya ukocha, lakini kuondoka kwake mwezi uliopita huenda kukasababisha matatizo mbele kwa timu, ingawa siyo tatizo lake.

Moja ya aina ya ya mambo ya aina ya ufundishaji wa Zidane ilikuwa uaminifu mkubwa kwa wachezaji waliomtumikia vizuri, jambo ambalo limemkumbuka Arsene Wenger katika miaka yake ya mwisho Arsenal.

Alisimama kwa Keylor Navas, licha ya 'Los Blancos' kuwa na mbadala wa kumsajili David de Gea majira ya joto 2016, huku pia akiwa kizuizi kwa Perez kukiimarisha kikosi hicho kwa mustakabali wa baadaye.

Mbappe anayewika kwa sasa Kombe la Dunia akiwa na Ufaransa, alikuwa nyota wa Monaco msimu wa 2016/17, kwa kuiwezesha kutinga nusu fainali na kutwaa ubingwa wa Ligue 1, hivyo kuifanya miamba yote ya soka Ulaya kumtupia macho.

Haraka liliibuka suala la dau lake litakuwa kubwa kufuatia Neymar kutua Paris Saint-Germain kwa Euro milioni 222.

Shabiki huyo kindakindaki wa utotoni wa Real Madrid, Mbappe, alishaelezwa kutaka kutua dimba la Santiago Bernabeu na Perez alivutiwa na mchakato huo.

Licha ya taarifa za hivi karibuni za kupanda dau lake, miamba hiyo ya Hispania ilikuwa tayari kufika bei ambayo hatimaye PSG iliridhia kulipa kumpata kinda huyo, lakini lawama zote ni kwa Zidane ambaye alishindwa kuhakikisha uhamisho huo unakamilika.

Hiyo ilitokana na kushindwa kukikubali kipaji cha raia mwenza huyo wa Ufaransa, kubwa akiwaza kuwa atalazimishwa kumuuza mmoja kati ya Gareth Bale, Cristiano Ronaldo ama Karim Benzema ili kumsajili.

Hali hiyo ndiyo iliyokuwa imetawala kikosini, kwamba kingekuwa kizuizi kwa Zidane kuipata huduma ya Mbappe.

Na bado ikikumbukwe kwamba uhamisho wake huo wa mkopo PSG haukukamilika hadi siku ya mwisho ya dirisha kufungwa.

Zidane alikuwa na nguvu ya kumshawishi Perez kutofanya jambo lolote sokoni ambalo rais huyo alitaka kulifanya.

Licha ya Mbappe kuwa na umri wa miaka 19, anaonyesha kwenye Kombe la Dunia ni kwa nini yeye anatajwa kuwa na kipaji zaidi katika kizazi hiki.

Uwezo alioonyesha wakati Ufaransa inaichapa Argentina 4-2, kufuatia kufunga mabao mawili na kisha kusababisha penalti iliyozaa bao la kwanza kwenye mechi hiyo ya hatua ya 16-Bora ya Kombe la Dunia nchini Urusi, ni mambo ambayo yanaiumiza Real Madrid kwa nini haikusajili.

Macho yake ya kuliona lango ni ya asili na wakati huu tukielekea msimu mpya wa 2018/19, ni vigumu kudai kwamba bado hajawa mmoja wa washambuliaji bora duniani.

Kutua jiji hilo la Hispania kungeweza kuihakikishia timu hiyo kuwa na mustakabali mzuri wa baadaye pasipo zama za Ronaldo, lakini kwa sasa Zidane akiwa ameondoka klabu hiyo inajaribu kuanza maisha mapya huku ikiwa bila kinda huyo.

Real Madrid inatumai kupata mafanikio kupitia kwa Wabrazil wawili Vinicius Junior na Rodrygo, lakini ni sawa na bahati nasibu hasa ukizingatia makinda hao hawajawahi kucheza nje ya Brazil, na ni wadogo sana ukilinganisha na Mfaransa huyo.

Wawili hao wamenunuliwa kwa Euro milioni 90, ambazo ni nusu ya dau lililohitajika kumpata Mbappe, lakini kama hawatafikia matarajio litakuwa ni kosa kubwa kuwahi kufanyika katika historia ya usajili sokoni.

**USILOLIJUA**

Ubelgiji ni timu ya kwanza kutokea nyuma kwa mabao mawili ama zaidi na kisha kushinda mechi ya hatua ya mtoano ya Kombe la Dunia ndani ya dakika 90, tangu Ureno ilipofanya hivyo kwa kuichapa DPR Korea mwaka 1966 kwenye hatua ya robo fainali (Ureno ikitokea nyuma kwa mabao 0-3 na kushinda 5-3).





# Vwawa kunufaika mradi maji ya bomba

**Na Grace Mwakalinga,** MBOZI

ZAIDI ya waka-zi 10,000 wa Mji wa Vwawa katika Wilaya ya Mbozi mkoani Songwe, ambao walikuwa wanakabiliwa na uhaba wa maji kwa kipindi kirefu, wataanza kunufaika na mradi wa 'Kumtua mama ndoo kichwani' baada ya serikali kutoa fedha kwa ajili ya kuboresha vyanzo vya maji na kuweka mabomba.

Akizungumza wakati wa kukagua mradi wa maji, Naibu Waziri wa Maliasili na Utalii ambaye pia ni Mbunge wa Jimbo la Vwawa, Japhet Hasunga, alisema mpaka sasa mradi huo umefikia asilimia 82 kukamilika na Desemba, mwaka huu wananchi wataanza kunufaika.

"Ujenzi wa mradi huu wa maji umefikia asilimia 82 nina imani mwezi wa tisa utakuwa tayari na wananchi wataanza kutumia maji ya bomba, tunapongeza jitihada za mkandarasi wa mradi huu amejitahidi licha ya kuwa tulimpa asilimia 37 ya fedha ambazo tulikubaliana," alisema Hasunga.

Aidha, alisema mradi huo utasaidia kupungua changamoto ya maji kwa wananchi asilimia 40 hususani kinamama, ambao ndio waathirika wanapokwenda umbali mrefu kutafuta huduma ya maji.

Mhandisi wa ujenzi katika mradi huo uliopo Senjele na Iyula, Khamis Makwinya, alisema ucheleweshwaji wa pesa katika miradi yake ndiyo kikwazo kikubwa cha utandazaji wa mabomba kwa zaidi ya kilometa 60 na kwamba endapo atapewa fedha mradi huo utakamilika kwa wakati.

Baadhi ya wananchi hususani kinamama walikiri kuwapo upungufu mkubwa wa huduma ya maji licha ya kuwa karibu na miradi ya maji au vyanzo vya maji.

Waliomba serikali iongeze jitihada za kusogeza miundombinu ya maji karibu na makazi ya wananchi, ili kupata huduma hiyo kwa wakati.

MAOMBI



Chifu Rocket Mwashinga, akizungumza wakati wa kikao kati ya viongozi wa serikali ya mkoa wa Mbeya, wa mila na dini kuhusu maombi maalumu ya kuzuia ajali zilizouandama mkoa huo. **PICHA: NEBART MSOKWA**

# Maombi maalum kuzuia ajali Mbeya

**Na Nebart Msokwa,** MBEYA

AJALI za barabarani zilizofululiza mkoani Mbeya na kusababisha vifo vya watu 45 ndani ya mwezi mmoja na nusu, zimeamsha makundi mbalimbali ya kijamii na viongozi wa dini na mila pamoja na wa serikali, wamekubaliana kufanya maombi maalumu ya kuzuia ajali hizo zisiendelee.

Viongozi hao walifanya kikao jana asubuhi katika Ofisi ya Mkuu wa Mkoa wa Mbeya, Amos Makalla, na kukubaliana maombi hayo yafanyike Julai 12, mwaka huu katika viwanja vya CCM Ruanda Nzovwe na kushirikisha wananchi wote.

Mkuu wa Mkoa wa Mbeya, Makalla, aliwataka wananchi wote mkoani humo bila kujali itikadi zao za kisiasa, dini wala jinsia zao kuhudhuria na kushiriki maombi hayo maalumu ya kumuomba Mungu auepushe na ajali hizo zinazogharimu maisha ya watu na mali zao.

"Tunatekeleza sheria na maagizo yote tuliyopewa na viongozi wa kitaifa, lakini busara zinatuelekeza kumrudia Mungu hivyo tunaomba siku ya Alhamisi, wananchi wote, dini zote na makabila yote, tukutane kumuomba atuepushie matatizo mkoa wetu uwe shwari," alisema Makalla.

Hata hivyo, alisema pamoja na maombi hayo, Kamati ya Ulinzi na Usalama ya Mkoa ilikaa na kukubaliana mikakati saba kwa ajili ya mapambano dhidi ya ajali hizo na kwamba iliridhiwa na viongozi wa kitaifa ambao pia walisaidia kuboresha.

Mwakilishi wa viongozi wa mila, Chifu Rocket Mwashinga, wa Kabila la Wasafwa, alisema viongozi wa mila wanaamini kuwa baada ya maombi hayo ajali hizo zinazogharimu maisha ya watu zitakwisha mkoani humo.

Alisema wao watafanya maombi yao kabla ya siku hiyo iliyopangwa na endapo ajali hizo zinasababishwa na watu, wahusika watabainika mapema na Mungu atasikia maombi yao.

"Maombi yetu huwa yana laana, hivyo kama jinamizi hili limeletwa na watu kwa njia za ushirikina watajulikana na watalaanika, lakini kama zinasababishwa na Mungu, tunaamini atatusikia maombi yetu," alisema Chifu Mwashinga.

Kwa upande wao viongozi wa dini walisema maombi hayo ya pamoja ni mazuri na yatasaidia kupunguza ajali kwa madai kuwa Mungu pekee ndiye mwenye uwezo wa kuzuia ajali hizo

Mmoja wa viongozi hao, Shekhe Hassani Katanga, Imamu Msaidizi wa Msikiti Mkuu wa Mkoa wa Mbeya, alisema mbali na maombi hayo, pia wanaomba vyombo vya habari vya mkoa huo hasa redio za kijamii zitumike kwa ajili ya maombi hayo.

Alisema viongozi wa dini wamekerwa na ajali hizo na wampongeza Rais Dk. John Magufuli kwa kuhuzunika pamoja na wananchi wa Mkoa wa Mbeya kutokana na ajali hizo akidai kuwa walikuwa wanamuona kwenye vyombo vya habari.

Mchungaji mwakilishi wa makanisa ya FPCT, Oscar Hongere, alisema maombi hayo yanatakiwa yasiwe ya zima moto bali yawe endelevu kwa kuyafanya kila mwaka.

Alisema mara nyingi binadamu huwa wanamkumbuka Mungu kipindi wanapopata tatizo, lakini wakiwa hawana shida yoyote hawamkumbuki Mungu, hivyo akaomba maombi yawe yanafanyika mara kwa mara.

# Waziri Kamwelwe apigia debe meli za mizigo

**Na Nebart Msokwa,** KYELA

WAZIRI wa Ujenzi, Uchukuzi, na Mawasiliano, Mhandisi Isack Kamwelwe, ameanza kuzipigia debe la kibiashara meli za mizigo zilizojengwa katika Ziwa Nyasa kwa kuwashauri Watanzania kuzitumia kusafirisha mizigo yao badala ya kuendelea kutumia barabara.

Mhandisi Kamwelwe alianza kupiga debe hilo juzi alipofanya ziara ya kutembelea Bandari za Itungi na Kiwira, zilizopo kwenye Ziwa Nyasa katika Wilaya ya Kyela, Mbeya kwa lengo la kujionea namna meli mbili mpya za mizigo zinavyofanya kazi baada ya kukamilika pamoja na kuangalia maendeleo ya ujenzi wa meli ya abiria ambayo ipo katika hatua za mwisho kukamilika.

Meli hizo zimeundwa na kampuni ya kizalendo ya Songoro Marine Transport ya jijini Mwanza na zimegharimu Sh. bilioni 20, na kusimamiwa na Mamlaka ya Usimamizi wa Bandari nchini (TPA).

Meli mbili za mizigo zina uwezo wa kubeba tani 1,000 za mizigo kwa wakati mmoja na moja ya abiria ikikamilika itakuwa na uwezo wa kubeba abiria 200 na tani 200 ya mizigo kwa wakati mmoja.

Akizungumza baada ya kukagua maendeleo ya meli zote tatu, Mhandisi Kamwelwe alisema, kazi iliyopo sasa ni kujenga barabara yenye urefu wa kilomita 27 kutoka Kyela mjini hadi Bandari ya Itungi na Kiwira zinajengwa kwa wakati, ili kurahisisha zaidi usafirishaji wa mizigo kwenda kwenye bandari hizo.

Mhandisi Kamwelwe alisema upembuzi wa barabara hiyo umeshafanyika na wanatarajia kuanza kujengwa katika mwaka wa fedha ujao, ili kuimarisha miundombinu ya kuunganisha bandari na barabara.

"Ili kuwavutia wawekezaji wetu kuleta mizigo na kutumia bandari hii na uwekezaji mkubwa wa hizi meli ni lazima tuboreshe miundombinu na niseme tu kwamba kwa mizigo inayosafiri kwenda nchini Malawi na nchi nyingine ndugu zangu wafanyabiashara meli zipo tayari zinasubiri mzigo kwa bei ambayo ni nafuu zaidi kuliko kusafirisha kwa barabara," alisema Mhandisi Kamwelwe.

Alisema mpango na mwelekeo wa serikali ya sasa ni kuona inaimarisha usafiri wa reli na meli kwa lengo la kuondokana na usafirishaji wa mizigo kwa kutumia barabara, ambazo zimekuwa zikisababisha ajali za mara kwa mara kutokana na magari makubwa ya mizigo (malori) kuacha njia, kusababisha ajali na kuharibu miundombinu ya barabara.

Awali Meneja wa Bandari ya Itungi, Galus Abeid, alisema pamoja na kujiimarisha katika usafiri wa majini kwenye ziwa hilo, bado wanakabiliwa na changamoto ya miundombinu ya barabara zinazounganisha bandari hizo kwa maelezo kuwa hazipo vizuri hivyo kukwamisha ufanisi wa bandari.





MAFUNZO



Baadhi ya wahudumu wa afya ya mama na mtoto wa Wilaya ya Bahi na Chemba wakiwa kituo cha Mundemu wilayani Bahi wakati wa kufunga mafunzo ya wiki tatu. **PICHA NA IBRAHIM JOSEPH**

# Wahudumu wa afya wanolewa

**Na Ibrahim Joseph,**
DODOMA

ZAIDI ya wahudumu 200 wa afya a mama na mtoto wamewezeshwa kupata mafunzo ya ngazi ya jamii na Shirika la World Vision Tanzania Kanda ya Kati.

Hayo yalibainishwa jana na Meneja wa Shirika hilo, Faraja Kulanga, wakati wa kufunga mafunzo hayo kwa wahudumu afya ngazi ya jamii awamu ya pili kwa Wilaya za Bahi na Chemba yaliyofanyika katika Kituo cha Mundemu wilayani Bahi.

Kulanga alisema shirika hilo limewawezesha wahudumu zaidi ya 200 wa afya ya mama na mtoto kwa kuwapatia mafunzo ya ngazi ya jamii.

Alisema wahudumu hao walipatiwa mafunzo kwa ufadhili wa World Vision Tanzania kwa kushirikiana na serikali kupitia Wizara ya Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto.

Alisema lengo la mafunzo hayo ni kuzuia vifo vya mama na mtoto kuanzia mimba hadi kufikia mtoto anapozaliwa pamoja na kupatiwa lishe inayostahili.

Alisema mafunzo hayo yalifanyika kwa awamu mbili, ambapo awamu ya kwanza yalihusisha wahudumu 154 na awamu ya pili wahudumu 66 pamoja na wasimamizi 15.

Aliyataja maeneo yaliyopo kwenye mradi huo kwa mkoa wa Dodoma ni Tarafa ya Mundemu kwa Wilaya ya Bahi na Tarafa ya Sanzawa kwa Wilaya ya Chemba.

Alibainisha kuwa mradi huo kwa Tarafa ya Sanzawa unatekelezwa kwenye jumla ya kata nne zenye vijiji 13 na Tarafa ya Mundemu iliyopo wilayani Bahi unatekelezwa kwenye kata tatu zenye vijiji 11.

Aidha, alisema sababu ya kuongeza idadi ya wahudumu hao ni kuisaidia jamii kila kitongoji, ili kupunguza vifo vilivyokuwa vikitokea wakati wa kujifungua.

Aliongeza pamoja na mafunzo, wahudumu hao watawezeshwa vitendea kazi kama baiskeli na baadhi ya vifaa tiba kwa ajili ya wajawazito.

Akisoma risala kwa niaba ya wahitimu wa mafunzo hayo, Rehema Augustino alisema mafunzo hayo yamechukua wiki tatu na yalihusisha kutoka wilaya hizo mbili mkoani hapa.

Alisema walianza wakiwa watu 70, lakini wanne walishindwa na kuendelea na kubaki 66 walioweza kuhitimu.

Aliyataja baadhi ya mambo waliyofundishwa ni huduma ya mama wakati wa ujauzito na baada ya kujifungua, mawasiliano kwa ajili ya mabadiliko ya tabia na ushauri nasaha na huduma ya mtoto mchanga na umri chini ya miaka mitano.

Mengine ni unyonyeshaji na lishe kwa mtoto, huduma za uzazi wa mpango ngazi ya jamii, kuzuia maambukizi ya VVU kutoka kwa mama.

# DC aagiza kuanza soko jipya nafaka

**Na Ibrahim Joseph,**
KONGWA

MKUU wa Wilaya ya Kongwa, Deogratius Ndejembi, amewaagiza wajumbe wa Baraza la Biashara la wilaya hiyo na madiwani wakae na kujadili kuhusu kuwa na soko la nafaka katika kijiji cha kibiashara cha Mkoka.

Ndejembi alitoa agizo hilo juzi wakati wa kikao cha baraza hilo la wilaya kilichofanyika wilayani hapo kwa lengo la kujadili masuala ya kibiashara.

Ndejembi aliwaagiza wajumbe hao wa baraza hilo kuhakikisha wanakaa na madiwani haraka iwezekanavyo, ili kujadili kuanzishwa kwa soko hilo katika kijiji hicho.

Hata hivyo, alishauri majadiliano hayo yasiharibu au kuzoretesha uwapo wa soko kubwa la kimatifa la mazao Kibaigwa lililopo katika wilaya hiyo.

Aidha, aliwataka wadau wengine washirikishe katika kikao hicho wakiwamo watu wa Mamlaka ya Mapato Tanzania (TRA), Jeshi la Zimamoto na wakaguzi wa mizani ili kuboresha zaidi mazingira ya uwapo wa soko hilo.

Naye Ofisa Mtendaji wa Baraza la Biashara Wilaya ya Kongwa, Luig Mbuya, alisema kuwa katika hatua za awali wajumbe kwa kushirikiana na idara ya biashara, kamati ya mipango na fedha na ofisa usafirishaji walijadili juu ya punguzo la tozo za karanga zilizobanguliwa kutoka Sh. 3,000 hadi 1,000.

Mbuya alisema katika kikao hicho wajumbe walijadili juu ya kuwa na mradi wa kituo cha mafuta ya alizeti katika Kijiji cha Pandambili barabara ya kutoka Dodoma kwenda Dar es Salaam.

Alisema mradi huo utagharimu Sh. milioni 58.1, ambapo wafadhili Shirika la LIC watatoa Sh. milioni 52.7, umoja wa wauza mafuta ya alizeti Pandambili (UVIWAPA) watatoa Sh. milioni 5.3 na Halmashauri ya Wilaya ya Kongwa itawajibika kuweka umeme na maji katika kituo hicho.

Aidha, utekelezaji wa ujenzi wa kituo umeanza kwa kumwaga mchanga na kokoto kusafisha eneo licha ya kuwa tayari mkataba wa ujenzi huo umeshasainiwa na ofisi ya halmashauri, ofisi ya LIC na UVIWAPA.

Kwa upande wake, Barnabas Masika, ofisa elimu kwa mlipa kodi kutoka ofisi ya TRA Dodoma, aliwataka wafanya biashara kulipa kodi kwa hiari bila usumbufu kwa kutumia mashine za kielektroniki EFD, akisema zinasaidia kuondoa usumbufu wa kufuatiliwa mara kwa mara na watu wa mapato.

# Jumuiya ya amani yaanzishwa

**Na Peter Mkwavila,**
DODOMA

WAUMINI wa madhehebu ya Kikristo na Kiislamu mkoani Dodoma, wameunda jumuiya ya maridhiano Tanzania itakayosaidia kudumisha umoja na amani nchini.

Akizungumza na wanachama wa jumuiya hiyo iliyoanzishwa jijini hapa, mratibu wa umoja huo kwa kanda ya kati, Festo Tumbotele, alisema kazi kubwa ya kuanzishwa ni kuunganisha ili kudumisha amani kuisaidia serikali pale yanapokuwapo mapungufu kati ya dola na wananchi.

Tumbotele alisema jumuiya hiyo ambayo imesajiliwa kitaifa moja ya kazi zake ni kusaidia kutatua kero mbalimbali za wananchi ambazo zipo ngazi ya chini kabla hazijawafikia viongozi wa juu wa taifa.

Alisema kuunganisha kwa madhehebu hayo yataweza kuisaidia serikali pindi inapotokea kuna changamoto za wananchi ambazo jumuiya hiyo inaweza kukabiliana nayo bila hata kuwafikia ngazi ya juu.

Kwa upande wake mratibu wa kitaifa wa jumuiya hiyo, Jovent William, alisema lengo kuu la kuundwa kwa chombo hicho kujenga mahusiano na umoja utakaoleta maridhiano kwa jamii na taifa lake.

Kwa upande wao wajumbe wa jumuiya hiyo wakizungumza kwa nyakati tofauti, walisema kuwa kuanzishwa kwa jumuiya hiyo ya maridhiano kutasaidia kutatua kero mbalimbali zinazotokea katika jamii.

Zabibu Ally ambaye pia ni Katibu wa Wanawake wa Kiislamu Dodoma na Mchungaji John Maliga, walisema ni imani yao kuwa jumuiya ya mariadhiano kwa mkoa wa Dodoma utaimarisha umoja kati yao waumini katika kuiombea serikali kutokana na majukumu waliyonayo viongozi.



AMURU



Waziri wa Maliasili na Utalii, Dk. Hamisi Kigwangalla, akiamuru askari watano wa Pori la Akiba Uwanda wanyang'anywe silaha zao na wawekwe chini ya ulinzi kwa ajili ya uchunguzi, baada ya kutambuliwa kwenye gwaride kwa tuhuma za kupokea rushwa ya Sh. milioni 5.8 kutoka kwa mfugaji, Shija Imeli (kulia). **MPIGAPICHA WETU**

# Waziri aagiza wanaochunguzwa afya wasaidiwe matibabu

**Na Rahma Suleiman,**
ZANZIBAR

WAZIRI wa Afya Hamad Rashid Mohammed amezitaka taasisi mbalimbali zinazojitolea kuisaidia jamii kwa kuchunguza afya zao kuhakikisha zinasaidia kuwapatia matibabu wanapogundulika na maradhi.

Akizungumza jana wizarani kwake na uongozi wa taasisi ya Jamii Yatul Akhlaaqul Islaam (JAI), ambayo inatarajia kufanya uchunguzi wa afya kwa wananchi mwanzoni mwa mwezi ujao, Hamad alisema taasisi nyingi zimekuwa zikijitolea kufanya uchunguzi wa afya kwa wananchi, lakini huiachia mzigo serikali katika suala la matibabu. Alisema ni vyema baada ya kufanya uchunguzi huo wa kiafya, kuwasaidia matibabu hasa ikizingatiwa kuwa serikali inakabiliwa na uhaba wa madaktari bingwa wa magonjwa mbalimbali.

"Mkishafanya uchunguzi ni vyema kuwasaidia wananchi kuwapatia matibabu hasa kwa yale magonjwa ambayo yana uhaba wa madaktari bingwa hapa Zanzibar," alisema.

Aliitaka taasisi hiyo kuwa na uratibu mzuri wanapofanya uchunguzi wa afya ili kutowasumbua wananchi.

Alisema ana imani mwitikio wa wananchi utakuwa mkubwa kujitokeza katika uchunguzi wa afya.

Mwakilishi wa taasisi hiyo, Dk. Soud Mgaya alisema kuwa taasisi hiyo inatarajia kufanya uchunguzi wa afya kwa wananchi, ili kuwasaidia kuwatatulia maradhi mbalimbali yanayowasumbua.

Alisema watachunguza maradhi mbalimbali ikiwamo saratani ya matiti, saratani ya shingo ya kizazi, sinikizo la damu, kisukari na ugonjwa wa macho na meno.

Alisema pia kutakuwa na uchangiaji wa damu kwa hiyari kwa kuwa mahitaji ya damu ni makubwa hivyo itakayopatikana itaweza kunusuru maisha ya wananchi. Alisema madaktari bingwa wa maradhi mbalimbali watakuwapo hivyo aliitaka jamii kujitokeza kwa wingi katika kuitumia fursa hiyo kujua afya zao.

Aidha alisema taasisi hiyo ni kimbilio la wanyonge na imejikita kuisaidia jamii katika huduma za afya.

# Wasanii wapigiwa chapuo kukuza uchumi

**Na Rahma Suleiman,**
ZANZIBAR

MKUU wa Mkoa wa Mjini Magharibi, Ayoub Mohammed Mahmoud, amelitaka Baraza la Sanaa Zanzibar kuendelea kuwaunga mkono wasanii wa hapo, ili kukuza vipaji vyao na uchumi wa taifa. Akifungua mkutano wa wasanii visiwani hapa, alisema iwapo wasanii hao wataendelezwa kuna uwezekano mkubwa wa kuendelea kukuza ushirikiano na sanaa ya Zanzibar. Alisema ili kubadili dhana ya sanaa kutoka katika burudani pekee na kuwa biashara, kuna haja ya kuwapo kwa ushirikiano miongoni mwa wasanii wa fani zote.

Alisema hatua hiyo itasaidia kuibua na kuviendeleza vipaji vipya na vingine sambamba na kukuza mila, silka na utamaduni wa Zanzibar.

Akisoma risala kwa niaba ya wasanii wenzake, Ali Mwalimu Ali, alisema lengo la mkutano ni kutambulishana fursa zilizopo katika tasnia ya sanaa mbalimbali kwa wasanii wa Zanzibar.

Alisema ulimwengu wa sanaa umebadilika hivyo kukutana kwao kutaweza kuikuza sanaa na kuzitambulisha kazi zao za kisanii.

Aidha, waliiomba serikali kuendeleza kazi ya ulinzi wa kazi za wasanii dhidi ya watu wanaodhulumu kazi zao jambo ambalo linarudisha nyuma juhudi zinazochukuliwa na wasanii hao.

Aliwataka wasanii wasiuze kazi zao kiholela bali kwa uzalendo pamoja na kuwasaidia kuwaingiza katika pato la taifa la nchi.

Naye mshauri wa Rais wa Zanzibar mambo ya Sanaa na Utamaduni, Chimbeni Kheri Chimbeni, aliwasisitiza wasanii wa Zanzibar kuzingatia maadili pamoja na kusaidiana kufanya kazi zao zinazohusu usanii.

# Taaluma uzalishaji na usarifu mazao kutolewa

**Na Rahma Suleiman,**
ZANZIBAR

WIZARA ya Kilimo, Maliasili, Mifugo na Uvuvi, imesema inadhamiria kutoa taaluma ya uzalishaji na usarifu wa mazao mbalimbali kwa vitendo wakati wa maonyesho ya Siku ya Chakula Duniani.

Akizungumza katika eneo linalotarajiwa kufanyika maonyesho hayo, huko Chamanangwe kisiwani Pemba, mratibu kutoka katika wizara hiyo, Sharif Maalim Hamad, alisema lengo kuu la maonyesho hayo ni kuonyesha uhalisia katika kasi ya uzalishaji wa mazao ya kilimo pamoja na kupambana na njaa.

Sharif, alisema maonyesho hayo yataiweka Wizara ya Kilimo kuwa na historia kubwa katika kuwaongezea wananchi elimu ya uzalishaji bora.

"Wizara imeamua kufanya hivi kwa makusudi na imani kubwa kuwa wananchi watajifunza mengi ambayo yataongeza uzalishaji katika shughuli za kilimo," alisema.

Alisema maonyesho hayo pia yanatarajiwa kuyashirikisha mashirika ya yasio ya kiserikali, ili kuona kila mmoja anapata fursa ya kushiriki.

Ofisa Mkuu Idara ya Umwagiliaji Maji Pemba, Mbarouk Ali Mgau, alisema kufuatia umuhimu wa maonyesho hayo, matayarisho kwa sasa yameanza, ili kuona wanafanikiwa kwa asilimia kubwa.

"Maonyesho tumeyapokea kwa dhati kabisa na kwa kuwa ni mara ya kwanza tumejipanga kufanya vizuri zaidi iwe ni ya mfano ndani ya nchi yetu," alisema.

Maonyesho ya Siku ya Chakula Duniani yanatarajiwa kufanyika Oktoba 10 hadi 17, mwaka huu, katika shamba la kilimo Chamanangwe, Wilaya ya Wete, Kisiwani Pemba.

MAFURIKO



Picha zikionyesha athari za mafuriko katika mkoa wa Horoshima, Japan. Idadi ya watu waliofariki hadi jana ilifikia 57, huku wengi hawajulikani waliko. **PICHA:AFP**

# Ethiopia, Eritrea mwanzo mpya

**ASMARA,** Eritrea

WAZIRI mkuu mpya wa Ethiopia Abiy Ahmed, ameanza ziara ya kihistoria huko Eritrea siku chache baada ya nchi hizo mbili kutangaza kusitisha uhasama baina hayo.

Ethiopia na Eritrea zimewahi kupigana katika siku za nyuma kutokana na mzozo wa mpakani na tangu hapo wamekuwa na uhasama wa zaidi ya miaka 20.

Hivyo Waziri Mkuu Abiy Ahmed atakuwa wa kwanza kutembelea Eritrea katika kipindi hicho cha miongo miwili.

Mapema mwezi huu Ethiopia ilipokea ujumbe kutoka Eritrean ulioashiria heri njema baina yao.

Kiongozi wa Eritrea Isayas Afewerki alikuwa wa kwanza kuchukua hatua ya mawasiliano na utawala wa Addis Ababa baada ya kusifia hatua za mageuzi ya kisiasa yanayofanywa na waziri mkuu Abiy Ahmed.

Eritrea ilijinyakulia uhuru wake hapo 1993 lakini haikupita zaidi ya miaka mitano, mzozo baina yao ukazuka kuhusu kipande cha ardhi kame iliyompakani mwa mataifa hayo na kusababisha uhasama huo wa miongo kadhaa.

Uchunguzi wa umoja wa mataifa ulibaini kuwa kipande cha ardhi kilichokuwa kinazozaniwa ni cha Eritrea, uamuzi ambao Ethiopia haujaukubali kikamilifu.

Eritrea na Ethiopia walipigana vita kuanzia Mei mwaka 1998 hadi Juni 2000. Licha ya nchi hizo kutumia mamilioni ya dola kwenye vita hivyo na watu wengi kuuawa ni manufaa kidogo sana yaliyopatikana.

Kulingana na uamuzi uliotolewa na tume ya kimataifa huko Hague, Eritrea ilikiuka sheria za kimataifa kwa kuivamia Ethiopia.

Wakati wa kumalizika kwa vita Ethiopia tayari ilikuwa imekalia ardhi yote iliyokuwa ikizozaniwa na kuingia ndani ya ardhi ya Eritrea.

Baada ya kumalizika kwa vita, tume ya mpaka ya Eritrea na Ethiopia iliyobuniwa na Umoja wa Mataifa, iliamua kuwa eneo la Badme ambalo ndilo lilikuwa linazozaniwa lilikuwa la Eritrea.

Hadi sasa Ethiopia inadhibiti eneo hilo lilil karibu na Badme na hata mji wa Badme.

Tarehe Juni 5, mwaka huu muungano wa vyama unaotawala nchini Ethiopia unaoongozwa na Abiy Ahmed, ulikubali kutekeleza kikamilifu makubaliano ya amani waliyoyasaini na Eritrea mwaka 2000.



# Mafuriko yaleta zahama

**TOKYO,** Japan

IDADI ya watu waliofariki dunia katika mvua kubwa katika maeneo kadhaa ya Japan iliongezeka jana na kufikia 57.

Maofisa wamesema, huku zoezi la uokoaji likiendelea kufanywa na wafanyakazi wa uokoaji na wanajeshi, wakijitahidi kujitosa kwenye tope na majini kuokoa maisha ya waathirika.

Chombo cha habari binafsi kilieleza kuwa waliopoteza maisha ni 67, huku idadi kubwa ya watu hawajulikani walipo. Athari za mvua zaidi zinatarajiwa.

Mapema jana Waziri Mkuu wa Japan, Shinzo Abe, akitoa wito wa kuwanusuru waathirika wa mafuriko hayo, huku akisema hakujawa na uhakika wa maisha ya watu wengi.

Mvua hiyo kubwa ilisababisha mafuriko na maporomoko katika maeneo ya magharibi ya nchi na kusababisha ulazima wa kuwaokoa zaidi ya watu milioni mbili.

Mvua hiyo iliharibu kabisa baadhi ya vijiji, na kuwalazimisha wakazi wake kujihifadhi kwenye mapaa ya majengo huku wakinyeshewa na mvua, wakisubiri kuokolewa.

Wananchi wameambia kuondoka kwenye makazi yao, lakini wengi wamebakia majumbani, huku wakizingirwa na maji yanayoongezeka pamoja na maporomoko.

Mamlaka ya hali ya hewa imetoa tahadhari kwa mikoa miwili kuwa mvua kubwa ingenyesha jana.

Barabara kadhaa zimegeuka kuwa mito katika mji wa Mihara, kaskazini ya mkoa wa Hiroshima, kutokana na mvua hiyo.

Hali hiyo ilisababisha magari kukwama kutokana na kufunikwa na maji.

"Eneo limegeuka kuwa bahari," alisema mkazi aliyeishi eneo hilo kwa muda mrefu, Nobue Kakumoto mwenye umri wa miaka 82.

"Nina hofu kwa sababu sijui hali hii itadumu hadi lini."

Baadhi ya wakazi waliamua kwenda maeneo ya vijiji kukagua uharibifu baada ya kutumia usiku mzima kujihifadhi katika mabanda madogo katika maeneo ya miinuko.

"Tunatekeleza operesheni ya uokoaji muda wote," Yoshihide Fujitani, ofisa wa kusimamia majanga katika mkoa wa Hiroshima alisema.

"Pia tunaangalia baada ya uokoaji kuweka sawa miundombinu ya maji na gesi," alisema zaidi.

Katika eneo la magharibi la Okayama, zoezi la uokoaji lilikuwa likiendelea kuwanusuru maelefu wakiwamo watoto na wazee kutoka hospitali, wengine kwa kutumia helikopta.

Waliokuwa kwenye majengo walikwama baada ya mto wa karibu kupasuka kingo zake na kusababisha mafuriko katika eneo hilo, nesi aliyekuwa kwenye majengo hayo alisema hapakuwapo umeme wala maji na kwamba walikuwa wanakaribia kuishiwa chakula.

"Takribani watu 1,000 wanaomba msaada wa kuokolewa jana asubuhi, lakini hatujapata picha halisi ya janga," Mutsunari Imawaka, msemaji wa mamlaka ya kusimamia majanga, aliiambia AFP.

"Tunajitahidi kuwanusuru haraka iwezekanavyo. Tunazidi kwenda," alisema.

Zaidi ya waokoaji 50,000, polisi na wanajeshi wamehamasisha kutoa msaada dhidi ya janga hilo, ambalo limeacha vijiji vikimegwa na mafuriko.

"Nilikuwa kwenye gari na mafuriko makubwa ya maji yalinizingira kutoka mbele na nyuma kisha kufunika barabara. Niliweza kunusurika," alisimulia Yuzo Hori, mwenye umri wa miaka 62 wakati akihojiwa na gazeti la kila siku la Mainichi Shimbun huko Hiroshima jana.

Mvua kubwa zilianza wiki iliyopita huku iliongezeka zaidi Alhamisi, wakati mfanyakazi wa kampuni ya ujenzi aliposombwa na maji ya mafuriko magharibi mwa Japan.

Idadi ya vifo imekuwa ikizidi kuongezeka, na kusababisha ugumu katika kazi ya uokoaji, huku wananchi waliokata tamaa wakitumia mtandao wa kijamii wa Twitter kuomba msaada wa kuokolewa.

# Washa, zima taa kwa ujumbe mfupi

**Na Mary Geofrey**

MAMLAKA ya Elimu na Ufundi (Veta), imebuni mfumo wa kisasa wa kuzima na kuwasha taa za nyumba au ofisi ukiwa mbali kwa kutumia ujumbe mfupi wa maneno.

Mfumo huo pia unaweza kutumika pia kwa kupiga makofi na taa za nyumba zikazimika ikiwa utakuwa hapo hapo.

Mwanafunzi aliyebuni mfumo huo, Robart Assey, akizungumza na Nipashe katika banda la Veta, lililopo kwenye viwanja vya Maonyesho ya 42 ya Kimataifa ya Biashara, alisema waliubuni miezi minne iliyopita.

"Mfumo huu tumeubuni wanafunzi wawili wa Veta, unatumika kwenye ofisi na nyumba, mmiliki anaweza kutoka nyumbani akafika kazini na akatuma ujumbe mfupi wa maneno taa zikazima," alisema.

Anasema mfumo huo pia unaunganisha familia nzima kupata taarifa ukiwa mmoja wa mwana familia atazima taa au kuwasha.

"Baba akiwasha taa akiwa ofisini, mama na watoto watapewa taarifa kwa njia ya ujumbe mfupi wa maneno. Na hata ikitokea mtoto amewasha taa au kuzima au kutumia kifaa kinachotumia umeme watu wote wa familia wanapata ujumbe mfupi wa maneno," alisema Assey.

Aidha, alisema wametengeneza mfumo wa kupunguza matumizi makubwa ya umeme kwenye wigo ya nyumba.

"Badala ya umeme kuwaka wakati wote kwenye uzio, tuna mfumo unaosaidia umeme kuwaka mtu anaposogelea nyumba na kutoa taarifa ni upande upi wa uzio aliposimama mtu, moja kwa moja mlinzi ataenda upande alipo mtu," alisema.

JARIBU



Waziri wa Kilimo, Mifugo na Uvuvi, Dk. Charles Tizeba, akijaribu kupiga simu wakati alipotembelea banda la kampuni ya TTCL katika Maonyesho ya 42 ya Biashara ya Kimataifa jijini Dar es Salaam. **PICHA: HALIMA KAMBI**

## NSSF yaagizwa kuwafikia sekta isiyo rasmi

**Na Mary Geofrey**

WAZIRI wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu Kazi, Ajira, Vijana na Watu wenye Ulemavu, Jenista Mhagama, amelitaka

Shirika la Taifa la Hifadhi za Jamii (NSSF), kuwafikia wote walio katika sekta isiyo rasmi ambao hawajafikiwa na huduma zao.

Mhagama alitoa agizo hilo mwishoni mwa wiki alipotembelea banda la NSSF katika Maonyesho ya 42 ya Kimataifa ya Biashara yanayoendelea jijini Dar es Salaam.

Alisema serikali ilifanya maamuzi sahihi katika mchakato wa kuchagua shirika moja kubaki kuhudumia sekta hiyo na kwamba wanatakiwa kuongeza kasi zaidi katika kuwafikia watu wengi zaidi.

Alisema, tafiti zinaonyesha kuwa mfuko huo unafanya vizuri na uwezo wa kuishi miaka 70 ijayo.

"NSSF tumieni utendaji huu uliotukuka kuhakikisha mnaifikia sekta isiyo rasmi nchi nzima ili iweze kunufaika na hifadhi za jamii kwa kuwa serikali na bunge waliikabidhi NSSF sekta hiyo na kutimiza malengo staili waliyojiwekea," alisema.

Aidha, alipongeza shirika hilo kwa kusaidia utekelezaji wa Tanzania ya viwanda ili nchi kufikia uchumi wa kati kwa kuanisha viwanda vyenye tija na kuleta maendeleo ya watu.

Alisema NSSF imekuwa mstari wa mbele katika kutoa mitaji kwa wajasiriamali wanaotaka kuanzisha viwanda vidogo vidogo hususani maeneo ya vijijini ambavyo vinasaidia kuongeza thamani ya mazao ambavyo gharama ya kuvimiliki ni Shilingi milioni mbili hadi Shilingi milioni tano kwa kutumia Benki ya Azania kutoa mikopo.

Alisema moja ya manufaa ya mifuko hiyo ni kupata matibabu hivyo aliitaka NSSF kuanzisha dawati maalum kwa ajili ya kupima virusi vya Ukimwi kwa wanaume kuunga mkono kampeni ya Waziri Mkuu Kassim Majaliwa kuhamasisha wanaume kupima virusi hivyo na kuacha kutumia wanawake kujua uzima wao.

Naye, Mkurugenzi Mkuu wa NSSF, Profesa Godius Kahyarara, alisema mafanikio ya shirika hilo yanatokana na maelekezo bora ya wizara na kuzaa matunda ikiwamo utekelezaji wa sera ya viwanda na mpaka sasa wana wanachama milioni moja nchi nzima.

# Wataalam kwenda nchi 5 mafunzo treni ya umeme

**Na Mary Geofrey**

SHIRIKA la Reli Tanzania (TRC), limesema linatarajia kupeleka timu ya wataalam wa fani mbalimbali 167 katika nchi tano tofauti kwa lengo la kujifunza namna ya kusimamia uendeshaji wa treni ya kisasa itakayotumia umeme.

Hatua hiyo inakuja wakati serikali ikiendelea na ujenzi wa reli ya kisasa maarufu kama Standard Gauge Rail (SGR), ambayo itasafiri kwa kasi ya umbali wa kilometa 160 kwa saa.

Akizungumza na waandishi wa habari kwenye Maonyesho ya Biashara ya 42 ya Kimataifa yanayoendelea Viwanja vya Sabasaba jijini Dar es Salaam, Mkurugenzi Mtendaji wa TRC Masanja Kadogosa, alisema timu ya wataalam hao itaondoka wakati wowote kuanzia sasa.

Alifafanua kuwa watalaam hao watatoka katika kada mbalimbali zikiwamo za wataalam wa mawasiliano, umeme, madaraja, usafirishaji, mafundi na madereva.

Alitaja nchi ambazo wameingia nazo makubaliano ya kuwafundisha wataalam hao ni Korea Kusini, Uturuki, Ethiopia, China na India.

"Tumeamua hivyo kutokana na kuhitaji kuwajengea uwezo watalaam wetu kutoka kwa nchi ambazo zenyewe zina uzoefu wa uendeshaji wa reli ya aina hii. Watalaam hao wataondoka muda wowote kutoka sasa," alisema.

Alifafanua kwa wanaokwenda nchini Uturuki waliamua kusubiri kidogo kutokana na mchakato wa uchaguzi wa nchi hiyo.

Akizungumzia ujenzi wa reli hiyo alisema utaambatana na ujenzi wa karakana za kisasa ambazo zitaenda sambamba na matumizi na teknolojia mpya inayotumia umeme tofauti na karakana zilizopo.

Aliongeza kuwa, ujenzi wa reli hiyo utamalizika kwa wakati kama ilivyopangwa kwa sababu unaendelea kwa kasi na ufanisi mkubwa na tayari mkandarasi ameahidi kuongeza vifaa na watalaam.

Alisema ujenzi wa nguzo katika eneo la kutoka Stesheni ya Dar es Salaam mpaka Stesheni ya Ilala unaendelea vizuri ambao ni asilimia 30 ya ujenzi wa reli kutoka Dar es Salaam hadi Stesheni ya Pugu.

# MATANGAZO MCHANGANYIKO

## HUDUMA MBALIMBALI

**PATA MKOPO WA HARAKA NA** MASHARTI NAFUU KUTOKA ENTERPRISE FINANCE LIMITED (EFL) Maalum kwa Wafanyakazi na Wafanyabiashara. Kwa mawasiliano piga: 0758 112 332 / 0677 111333

**MICHE YA MANANASI,** Miche ya mananasi toka Kiwangwa kwa mashamba: (i) Madogo (ii) Ya kati (iii) Makubwa, Mawasiliano: 0789 345618.

**MKOPO WA KISIMA KWA GARI**: Utakabidhi gari na kadi Orijino, utachimbiwa kisima kulingana na thamani ya gari na gharama za kisima kwa maelezo zaidi tupipie:0718625262/0769382632.

## ENEO/MASHAMBA

**ENEO LINAUZWA KIMARA,** Eneo kubwa linauzwa Kimara mwisho linafaa kwa kujenga nyumba nyingi za kisasa na kufanya biashara yeyote lipo karibu na barabara ya Morogoro. Huduma zote za jamii kama Maji, Umeme, n.k. na bei yake nafuu sana. Ili kuona piga simu namba 0653 239890 na 0676 418761.

**NYUMBA INAPANGISHWA,** Nyumba inapangishwa Lumo kwa Jimmy. Bedroom 3 master, stoo, jiko, sebule, garage, maji, fence, luku. Kwa piga simu namba 0756 406364.

**ENEO LINAUZWA KIMARA,** Eneo kubwa linauzwa Kimara mwisho linafaa kwa kujenga nyumba nyingi za kisasa na kufanya biashara yoyote lipo karibu na barabara ya Morogoro. Huduma zote zipo kama maji, umeme n.k na bei yake nafuu sana. Ili kuona piga simu namba 0653 239890.

**CHANIKA YETU** Viwanja vinauzwa vipo chanika mjini na maeneo ya jirani bei kuanzia 1,500,000/= na kuemdelea unaweza kulipia kwa awamu hadi miezi 3 Mawasiliano: 0716 232689

**KARIBU DODOMA MAKAO MAKUU**:Tunauza /tunanunua nyumba,viwanja,mashamba wasiliana na Dodoma Pazuri Group(DPG) Simu:0713706649/0715108151

## NAFASI ZA KAZI

**NAFASI ZA KAZI** waalimu wa certificate/ diploma science/hesabu 0656490706

**MAHAKAMA YA ARDHI NA NYUMBA YA WILAYA MBEYA**

**SHAURI NO. 18/2018**

**ESTER KELVIN MWAMUKONDA**
**An Administratix of Estate of the late**
**KELVIN NDINAGWE MWAMUKONDA……………………MDAI**

**DHIDI YA**

1. **ABDI ATHUMANI, and…………MDAIWA WA KWANZA**
2. **RAJABU ATHUMANI**
   **As the Administrators of the estate of Late MOSHI RAJABU…………………..MDAIWA WA PILI**

**YAH: KUITWA SHAURINI**

**KWA:**
1. **ABDI ATHUMANI**
2. **RAJABU ATHUMANI as Administrators of the Late MOSHI RAJABU**

Fahamu kwamba shauri amefungua shauri dhidi yako katika baraza hili. Shauri limepangwa kutajwa tarehe 25/07/2018 saa 2:30 asubuhi mbele ya Mh. A. Mapunda Mwenyekiti wa Baraza. Unatakiwa kuleta utetezi wa maandishi ndani ya siku 21 tangu tarehe ya wito huu.
Nyaraka zinazohusu shauri hili zinapatikana katika masijala ya Baraza la Ardhi na Nyumba Mbeya. Unaamriwa kuhudhuria mbele ya Baraza siku hiyo bila kukosa wewe mwenyewe au mwakilishi anayeruhusiwa kisheria. Ofisi za baraza zipo ndani ya eneo la Sababasa Mbeya Mjini.
**Kumbuka:** Usipohudhuria siku hiyo baraza litatoa amri stahilivu ikiwa ni pamoja na kusikiliza shauri pasipo wewe kuwepo.
Amri hii imetolewa kwa mkono wangu na Lakiri/Muhuri wa baraza hili leo tarehe 04/07/2018.

MWENYEKITI
05/07/18
114686202


*Uza,*
*Chenye Thamani Kubwa*
*Kwa Kutangaza Nasi*
*Kwa Bei Poa*
*Tupigie 0766 721 072*

JE UNAHANGAIKA PA KUUZA BIDHAA YAKO?

Nipashe

NI JIBU LAKO
NJOO UTANGAZE BIDHAA YAKO
KWA BEI NAFUU SANA

Tutumie E-mail: advertise@guardian.co.tz au piga simu: 0766 721 072


TAHADHARI: Wasomaji wanatakiwa kuuliza na kuchukua ushauri sahihi kabla ya kutuma fedha, au kuingia katika gharama yoyote kati yake na mtangazaji THE GUARDIAN LIMITED hawatahusika kwa malipo au manunuzi yoyote kati ya muuzaji na mnunuaji kwa matangazo yaliyochapishwa katika gazeti hili.

# DELE ALLI: SIKUWA BORA DHIDI YA SWEDEN




**SAMARA,** Urusi

DELE Alli hakuridhika na kiwango alichokionyesha wakati England ikiitoa Sweden kwenye robofainali ya Kombe la Dunia, licha ya kufunga bao la pili katika ushindi wa mabao 2-0.

**Kiungo huyo wa Tottenham, Alli awali alionekana kama asingecheza mchezo huo hapa Samara, lakini kocha, Gareth Southgate aliamua kutumia kikosi kilekile kilichoiondoa Colombia kwenye hatua ya 16.**

Baada ya kujaribu mara kadhaa kuonyesha kiwango chake kwenye kipindi cha kwanza, mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 22 alifunga kwa kichwa safi akiunganisha krosi ya Jesse Lingard na kuipeleka England kwenye nusufainali ya Kombe la Dunia kwa mara ya kwanza tangu mwaka 1990.

Ingawa Simba Watatu hao walisonga mbele na kufunga kwa mara ya kwanza hapa Urusi, yeye anahisi kwamba alitakiwa kufanya zaidi katika mchezo huo.

"Ilikuwa ni jambo zuri kwangu kufunga, hasa kwenye tukio kama hili. Lakini sidhani kwamba nilikuwa katika kiwango changu bora kwenye mchezo huu, lakini kufunga goli na kuipelekea timu yao na nchi kwenye nusufainali ni hisia za aina yake," alisema Alli akiiambia BBC.

"Ilikuwa alama nzuri. Ni jambo la muhimu kwamba tulikuwa na imani na mbinu za mchezo wetu, tulicheza vile tunavyotaka kucheza na kila mmoja alijua namna ya kucheza, tulitawala mchezo na kumiliki mpira kwa asilimia kubwa, lakini tulikuwa watulivu. Sweden wamethibitisha kwamba wanapata ugumu zaidi kucheza dhidi yetu.

"Ni mafanikio makubwa kwa timu yetu. Tuliwalipa mashabiki wetu waliopo nyumbani, kwa namna ambavyo wamekuwa wakitupa sapoti. Ni kiwango kikubwa mno."

Golikipa Jordan Pickford alikuwa shujaa wa England wakati wa kupigiana penalti dhidi ya Colombia alichaguliwa kuwa nyota wa mchezo huo baada ya kuokoa penalti mbili za Marcus Berg na Viktor Claesson.

"Alithibitisha katika mchezo uliopita kwa namna alivyo golikipa mkubwa na ameweza pia kuthibitisha kwenye mchezo huu dhidi ya Sweden. Tutakuwa tunasherekea nae pamoja," alisema Alli.

Pickford aliokoa hatari zote tatu zilizoelekea langoni mwake, lakini pia anaonyesha kuwa atakuwa fiti kwa mchezo ujao wa nusufainali dhidi ya Croatia.

"Unatakiwa kuwa tayari kutoka mwanzo, kitu ambacho kwangu nilikuwa nimejipanga. Baada ya kuokoa kutoka kwa Berg ikanifanya nijiamini zaidi," alisema.

"Matokeo mazuri, tulijua kwamba ungekuwa mchezo mgumu, tulijua kwamba, wangeingia kwa kujiamini na kutaka kushinda. Tulifanya kazi vizuri na kuweza kupata matokeo tuliyoyataka.

"Mara zote tumekuwa tukisema tutaingia katika kila mchezo kuhakikisha kuwa tunaweka historia yetu wenyewe.

"Kwa sasa tunapumzika na kujiandaa kwa ajili ya mchezo ujao. Hautakuwa mchezo rahisi, lakini tumejipanga kuwa fiti na tayari kwa mchezo huu ili tuweze kupata matokeo mazuri.



**Jumanne, 10 Julai 2018**
Ufaransa vs Ubelgiji — Uwanja Saint Petersburg **(Saa 3: Usiku)**

**Jumatano, 11 Julai 2018**
Croatia vs England — Uwanja Luzhniki **(Saa 3:00 Usiku)**

**WAFUNGAJI**

| | | |
|---|---|---|
| Harry Kane | England | 6 |
| Cristiano Ronaldo | Ureno | 4 |
| Romelu Lukaku | Ubelgiji | 4 |
| Denis Cheryshev | Urusi | 4 |
| Diego Costa | Hispania | 3 |
| Artem Dzyuba | Urusi | 3 |
| Kylian Mbappe | Ufaransa | 3 |
| Edinson Cavani | Uruguay | 3 |
| Antoine Griezmann | Ufaransa | 3 |
| Luis Suarez | Uruguay | 2 |
| Takashi Inui | Japan | 2 |
| Sergio Aguero | Argentina | 2 |
| Luka Modric | Croatia | 2 |
| Neymar | Brazil | 2 |
| Philippe Coutinho | Brazil | 2 |
| Son Heungmin | Korea | 2 |
| Mile Jedinak | Australia | 2 |
| Eden Hazard | Ubelgiji | 2 |
| John Stones | England | 2 |
| Wahbi Khazri | Tunisia | 2 |

# IBRAHIMOVIC AWAPA SWEDEN MPIRA WA DHAHABU



**SAMARA,** Urusi

ZLATAN Ibrahimovic anafikiri wachezaji wote wa Sweden wanastahili kupewa tuzo ya mpira wa dhahabu kwa kile walichokionyesha kwenye michuano ya Kombe la Dunia.

Sweden waliondolewa hapa Urusi juzi Jumamosi baada ya kufungwa na England mabao 2-0, ambao sasa watacheza na Croatia kwenye hatua ya nusufainali. Lakini Sweden wamefanya makubwa tofauti na matarajio ya wengine na Ibrahimovic ameoneshwa kuridhishwa na kiwango cha kikosi hicho kinachonolewa na kocha Janne Andersson.

"Kila mchezaji anatakiwa kupata mpira wa dhahabu," aliandika Ibrahimovic kwenye ukurasa wake wa mtandao wa kijamii wa Twitter.

"Kile walichokifanya kitakumbukwa milele. Asante kwa mchezo mzuri."

Wayne Rooney ambaye atacheza na mchezaji huyo wa zamani wa Sweden kwenye Ligi Kuu ya Marekani, MLS, baada ya kujiunga na DC United, haraka alimtania mchezaji mwenzake huyo wa zamani pale Manchester United.

"Unajisikiaje leo Ibra?" aliandika Rooney kwenye ukurasa wake wa Twitter. "Kama ukitaka tuchati mimi nipo hapa."

Ibrahimovic pia alitaniana na mchezaji wa zamani wa United, David Beckham. Beckham alimuahidi Ibrahimovic kumnunulia chakula cha jioni popote atakapotaka kama Sweden wangeshinda hapa Samara.

## Southgate awasifia Jones, Cahill, Welbeck

**MOSCOW,** Urusi

GARETH Southgate anaamini mafanikio ya England kwenye michuano ya Kombe la Dunia ni ya kikosi chote, lakini amewasifia zaidi Phil Jones, Gary Cahill na Danny Welbeck.

Wote hao hawakuwepo kikosini wakati England ikiibuka na ushindi wa mabao 2-0 dhidi ya Sweden na kufuzu nusufainali ya Kombe la Dunia kwa mara ya kwanza tangu mwaka 1990.

Harry Maguire na Dele Alli ndio walikuwa wafungaji wa mabao ya England na kuiwezesha kutinga katika hatua hiyo ya timu nne na sasa itacheza na Croatia hapa Moscow Jumatano.

Lakini Southgate alisifia mchango wa wachezaji wakongwe nje ya uwanja, Welbeck, Cahill na Jones licha ya kutopata dakika za kutosha za kucheza kwenye Kombe la Dunia hadi sasa.

"Siwezi kuzungumzia mchezaji mmoja-mmoja kwani timu nzima kuanzia benchi la ufundi wana umoja na wamekuwa kitu kimoja na  na kila mmoja anajua jukumu lake," alisema Southgate akiiambia BBC Sport mara baada ya mchezo huo.

"Baadhi yao hawajapata muda mwingi wa kucheza dimbani kama Jones, Cahill na Welbeck, lakini nidhamu yao na maelekezo wakati wa mazoezi ndio sababu ya mafanikio haya ya kufuzu nusufainali."

Akizungumzia nafasi ya England kwenye hatua ya nusufainali, Southgate aliongeza: "Uwepo wetu hapa una hisia zake. Tulifurahia matokeo na kila moja aliona kilichotokea kwani huwa haitokei mara kwa mara.

"Ninachojua ni kwamba makocha wengine wa England walifika nusufainali kabla ya mimi, naheshimu mafanikio yao na ni hisia za aina yake kuwepo hapa."

England iliitoa Sweden baada ya kutinga hatua hiyo kwa changamoto ya mikwaju ya penalti dhidi ya Colombia kwenye hatua ya 16.

"Tulijua kwamba mchezo tunaokwenda kucheza ni tofauti, kutoka kwenye muda wa nyongeza hadi kwenye penalti inahitaji nguvu na kutulia, ulikuwa ni wakati tofauti kabisa," amesema Southgate.



## Putin ampongeza Cherchesov, Urusi

**MOSCOW,** Urusi

RAIS wa Urusi, Vladimir Putin alimpigia simu kocha, Stanislav Cherchesov kuipongeza timu ya Taifa, licha ya kuondolewa kwao kwenye michuano ya Kombe la Dunia.

Croatia iliiondoa Urusi kwenye hatua ya robofainali kwa kushinda penalti 4-3, huku ile ya ushindi ikifungwa na Ivan Rakitic katika dimba la Sochi.

Denis Cheryshev alianza kwa kuwafungia wenyeji bao la kuongoza katika dakika ya 20, lakini iliwalazimu kusubiri hadi dakika ya 115 kusawazisha kupitia Mario Fernandes baada ya Croatia kuwa mbele kwa mabao mawili ya Andrej Kramaric na Domagoj Vida.

Ingawa Urusi ilishindwa kufuzu kwa nusufainali ambako angecheza na England, Cherchesov alidai kwamba Putin alifurahishwa na namna timu hiyo ilivyocheza.

"Waziri wetu Mkuu, Dmitry Medvedev alikuwepo kwenye vyumba vya kubadilishia nguo. Putin alinipigia baada ya mchezo. Amewasifia wachezaji walivyojituma na kucheza," alisema akiwaambia waandishi wa habari.

"Alisema tumeonyesha soka zuri uwanjani. Nilimuambia kwamba hatukuridhika na matokeo. Lakini akaniambia kwa kile tulichofanya ni kikubwa."

Mkataba wa Cherchesov na chama cha soka cha Urusi unamalizika Agosti mwaka huu na hakuwa tayari kuzungumzia majaliwa yake ya baadae.

"Tusizungumzie hilo kwa sasa. Unaona kwamba kuna mabadiliko yanatokea kwenye timu. Siwezi kuzungumzia yajayo," alisema kocha huyo.

"Tulijua tangu sekunde ya kwanza, nilijua wapi tunapokwenda. Tumefanikiwa, lakini bado tunatakiwa kuendelea mbele."

Matarajio ya Urusi wakati wanaanza michuano hiyo yalikuwa madogo, lakini Cherchesov anahisi jitihada zao zimesaidia mashabiki kuwaona wamepigana haswa.

Aliongeza: "Mnaweza kushangaa, lakini nimekuwa nikijaribu kwa kila njia kupata habari za soka kutoka kila sehemu. Hakukuwa na timu yoyote kwenye michuano hii ya Kombe la Dunia ambayo nchi yao iliwaamini kwa asilimia 100%.

# DONDO OKA
## MAGAZE AYA



# N'ZONZI, TORREIRA VISIKI VIPYA ARSENAL

●●● N'Zonzi anathaminishwa na pauni milioni 30, ana uzoefu mkubwa na soka la Ulaya....

**LONDON,** England

ARSENAL ipo katika mazungumzo na miamba ya La Liga ikitaka kusaini viungo wakabaji wawili, wakati huu kocha Unai Emery akikijenga upya kikosi hicho kilichopoteza mwelekeo msimu uliopita.

**Tayari Arsenal imeripotiwa kuanza mazungumzo na Sevilla kuhusu uwezekano wa kumsajili kiungo Mfaransa Steven N'Zonzi (pichani) wakati ikielezwa mambo yamefikia pazuri kwa kiungo wa Sampdoria, Lucas Torreira.**

N'Zonzi, 29, ambaye kwa sasa anakitumikia kikosi cha Ufaransa katika fainali za Kombe la Dunia nchini Urusi, siyo mara ya kwanza kuwindwa na Arsenal, kwani alikuwa katika rada za Arsene Wenger hapo kabla.

Kwa mujibu wa Sky Sports, N'Zonzi amekuwa akiwindwa kwa muda mrefu na miamba hiyo ya Kaskazini mwa London na kama atatua, ataungana kwa mara nyingine na kocha Emery ambaye alifanya naye kazi msimu wa 2015/16 hapo Sevilla.

N'Zonzi ambaye anathaminishwa na pauni milioni 30, ana uzoefu mkubwa na soka la Ulaya kutokana na kuichezea SC Amiens, Blackburn Rovers na Stoke City kabla ya kutua La Liga mwaka 2015.

Mfaransa huyo amejiimarisha zaidi kama kiungo mkabaji, nafasi ambayo 'The Gunners' inataka kuongeza viungo wenye ubora zaidi kufuatia kuondoka kwa Jack Wilshere huku kiwango cha Granit Xhaka kikiwa ni cha kushuka na kupanda.

N'Zonzi anaweza kuipa uimara safu hiyo ya kiungo mkabaji kutokana na ubora wake wakati huu akiwa ameichezea Sevilla mechi 136 hadi sasa, klabu ambayo ana mkataba nayo hadi majira ya joto 2020.

Kwa upande wa Torreira, ambaye naye ni kiungo mkabaji akiifanya kazi hiyo vema akiwa na Sampdoria pamoja na Uruguay, uhamisho wake wa kutua Arsenal unaelezwa utatangazwa rasmi wiki hii.

Emery ameanza kwa kuimarisha safu yake ya ulinzi akiwasajili mabeki Stephan Lichtsteiner, Sokratis Papastathopoulos pamoja na kipa Bernd Leno, na sasa amegeukia nafasi ya kiungo mkabaji.

## ZISIKUPITE

### MESSI AMTAKA WILLIAN BARCA

MSHAMBULIAJI wa Barcelona, Muargentina Lionel Messi, yupo tayari kucheza pamoja na Willian katika dimba la Nou Camp. ***(Manchester Evening News)***

### WILSHERE AKARIBIA WEST HAM

WEST HAM inajiandaa kukamilisha dili la kumsajili kiungo wa England, Jack Wilshere, ambaye ni mchezaji huru baada ya kuondoka Arsenal. ***(Sunday Mirror)***

### FEKIR KUBAKI LYON

RAIS wa Lyon, Jean-Michel Aulas, bado anadhani kiungo Mfaransa Nabil Fekir, 24, ataendelea kuwamo katika kikosi hicho msimu ujao baada ya uhamisho wake wa kutua Liverpool kushindikana. ***(Goal)***

### UTD YAJIAMINI KWA WILLIAN

MANCHESTER United inaamini itamsajili mshambuliaji wa Chelsea, Mbrazil Willian, 29. ***(Sun on Sunday)***

### YARMOLENKO KUTUA WEST HAM

WEST Ham imetoa ofa ya pauni milioni 17.5 kwa mshambuliaji wa Borussia Dortmund na Ukraine, Andriy Yarmolenko, 28, ambaye alijiunga na klabu hiyo ya Ujerumani mwaka jana kwa pauni milioni 23. ***(Sky Sports)***

### LIVER, SPURS KWA GREALISH

LIVERPOOL inafanya mazungumzo na Aston Villa kuhusu kumsajili kiungo Jack Grealish, 22, lakini Tottenham imeendelea kupewa nafasi kubwa ya kumsajili. ***(Sunday Mirror)***

### CITY YAMTOA BROWN MKOPO

BEKI wa Marekani, Erik Palmer-Brown, ametua kwa mkopo NAC Breda akitokea Manchester City. ***(ESPN)***

### YADUNDA KWA TIERNEY

BEKI Kieran Tierney, 21, anajiandaa kubaki Celtic wakati Everton ikiwa imeshaamua kukubali kufika dau la pauni milioni 25 zilizokuwa zikihitajika ili kumwachia nyota huyo wa kimataifa wa Scotland. ***(Scottish Sun)***

### GONZALEZ ATEGWA UNITED

MANCHESTER United inamuwinda kiungo wa Barcelona, Mhispania Nico Gonzalez, ambaye bado hajakubali mkataba mpya na mabingwa hao wa La Liga. ***(Sport)***

### HAZARD MDOGO KUTIMKA

MDOGO wa mshambuliaji wa Chelsea, Eden Hazard, Kylian, 22, anakaribia kuondoka Stamford Bridge baada ya kiungo huyo kujiunga na Klabu ya VVV Venlo ya Ubelgiji kwa majaribio. ***(Goal)***

### NDOMBELE AGOMEWA LYON

LYON imeiambia Chelsea kuwa Tanguy Ndombele, hatauzwa majira haya ya joto wakati huu 'The Blues' ikisaka mbadala wa N'Golo Kante, anayewindwa na Paris St-Germain majira haya ya joto. ***(Sunday Express)***

### LOZANO AWINDWA UNITED

MANCHESTER United ipo tayari kutoa pauni milioni 40 ili kumsajili mshambuliaji wa PSV Eindhoven Mmexico, Hirving Lozano, 22. ***(Tuttomercatoweb)***

## HABARI MICHEZO



## Ngasa ajigamba kuipaisha Yanga

**Na Mwandishi Wetu**

WINGA aliyerejea kwenye kikosi cha Yanga, Mrisho Ngasa (pichani), amesema bado ana uwezo wa kutumikia timu hiyo na kuipa mafanikio.

Akizungumza na Nipashe, Ngasa 'Anko' alisema anafahamu ukubwa wa klabu ya Yanga na bado ana uwezo wa kuwafurahisha mashabiki wa timu hiyo.

"Kazi yangu ni mpira, lakini kuchezea Yanga ni zaidi ya kazi kwangu, bado nina uwezo wa kuichezea na kutoa mchango wangu, " alisema.

Nyota huyo tayari ameanza mazoezi na klabu hiyo kujiandaa na Ligi Kuu Tanzania Bara.

Ngasa aliipa mafanikio makubwa Yanga na kujitangaza zaidi akiwa na timu hiyo baada ya kutua kuichezea akitokea Kagera Sugar.

"Nina uzoefu na Ligi Kuu, hivyo siwezi kushindwa kuonyesha uwezo wangu," alisema Ngasa.

Nyota huyo wa zamani wa Azam na Simba amejiunga na Yanga akitokea Ndanda FC ya Mtwara.

## Mwigulu agawa mipira Iramba

**Na Jumbe Ismailly,** IRAMBA

ALIYEKUWA Waziri wa Mambo ya Ndani, Mwigulu Nchemba, amekabidhi zawadi za mipira kwa timu 435 za mpira wa miguu zilizopo Jimbo la Iramba Magharibi ili ziweze kujiandaa kwa ligi itakayoshindania kombe pamoja na fedha taslimu.

Nchemba alikabidhi msaada huo kwenye mkutano wa hadhara uliofanyika katika viwanja vya soko la Kijiji cha Misigiri,wilayani Iramba, Singida alipokwenda kuwatoa hofu juu ya dhana iliyoanza kujengeka miongoni mwao kuwa huenda akajiuzulu nafasi yake ya uwakilishi wa Jimbo la Iramba baada ya kuenguliwa nafasi ya Uwaziri wa Mambo ya Ndani.

Alisema pamoja na utamaduni wake wa kugawa vifaa vya michezo kwa timu za jimbo hilo, lakini alikiri pia kwamba bado kuna timu za kata za Urughu, Mtoa, Mtekente na Shelui hazijapatiwa hivyo kuchukua wasaa huo kuwatoa wasiwasi viongozi wa timu hizo kuwa nao watapewa.

"Waliniambia masuala ya michezo na sasa hivi nikimaliza hapa baada ya kikao hiki siku zitakazofuata tutaambizana, sijamalizia kata za Urughu, Mtoa, Mtekente na Shelui mliniambia kuhusu mambo ya michezo,"alifafanua.

# CANAVARO: TARATIBU YANGA ITASHANGAZA

**Na Faustine Feliciane**

NAHODHA wa Yanga, Nadir Haroub 'Canavaro', amekiri klabu yao inapitia wakati mgumu kiuchumi, lakini anaamini viongozi wa timu hiyo wanapambana kuirejesha kwenye mstari wake.

"Naamini tutakaa sawa, kwa sasa kila mtu anajua tunapopitia,", alisema Canavaro.

Alisema wapo wanaoidharau Yanga, lakini msimu ujao hawataamini na watahakikisha wanatwaa ubingwa.

"Tutakuwa na timu nzuri hilo naamini, najua viongozi wanafanya kazi yao, " alisema Canavaro.

Yanga kwa sasa ipo kwenye maandalizi ya kuivaa Gor Mahia kwenye michuano ya Kombe la Shirikisho Afrika.




Mchezaji wa Flying Dribblers Baraka Mopelle (Kulia), akijaribu kumzuia Rich Rova wa Ukonga Hitmen wakati wa mashindano ya Sprite Bball Kings yaliyofanyika katika viwanja vya Ukonga-Airwing katika hatua ya mtoano. Flying Dribblers walishinda kwa vikapu 87-63. **MPIGAPICHA WETU**

# JKT Queens yaweka rekodi ikitwaa 'ndoo'

**Na Mwandishi Wetu,** MLANDIZI

MABINGWA wapya wa Ligi Kuu ya Wanawake Tanzania, JKT Queens 'Maafande', wameweka rekodi ya kutwaa ubingwa wa ligi hiyo bila kupoteza mechi hata moja katika msimu huu wa 2017/18.

JKT Queens ilikabidhiwa kombe la ubingwa baada ya kuibuka na ushindi wa mabao 6-2 dhidi ya wenyeji Mlandizi Queens katika mchezo wa kufunga pazia uliopigwa juzi kwenye Uwanja wa Mabatini, Pwani.

Kutokana na matokeo hayo ya mechi ya mwisho ya hatua ya Nane-Bora, JKT Queens inayoundwa na nyota wengi wa timu ya Taifa (Twiga Stars), ilifikisha pointi 42 na kufuatiwa na Sisterz Kigoma iliyofikisha pointi 30 wakati Alliance Girls wao wamemaliza wakiwa na pointi 24.

Baobab Queens ya Dodoma imemaliza ligi ikiwa katika nafasi ya tano baada ya kujikusanyia pointi 20 ikifuatiwa na Panama Queens yenye pointi 16 wakati Simba Queens na Evergreen ya Temeke Dar es Salaam wamemaliza kila mmoja akiwa na pointi nne.

Mabao ya mabingwa hao katika mchezo huo wa juzi ambao ulihudhuriwa na wageni na viongozi mbalimbali akiwamo Rais wa Shirikisho la Soka Tanzania (TFF), Wallace Karia, yalifungwa na Donisia Minja, Wema Richard, Stumai Abdallah, Asha Rashid "Mwalala" na Fatuma Mustafa aliyetupia mawili.

Mshambuliaji, Mwanahamisi Omary "Gaucho" na Jamilla Hassan, ndio waliofunga mabao kwa upande wa Mlandizi Queens ambayo ilivuliwa ubingwa zikiwa zimebaki mechi tatu mkonpni.

Matokeo ya mechi nyingine zilizopigwa juzi ni wenyeji Baobab Queens walipata ushindi wa mabao 4-1 dhidi ya Simba Queens kutoka jijini Dar es Salaam wakati Sisterz Kigoma iliwachapa Evergreen 5-0 na Panama ilimaliza vyema kwa kuwafunga Alliance Girls mabao 3-2.





Mabingwa wapya wa Ligi ya Wanawake, JKT Queens, wakiwa na kombe lao baada ya kulitwaa rasmi juzi. **MPIGAPICHA WETU**

Michezo
Jumatatu Julai 9, 2018
Nipashe

## N'Zonzi, Torreira visiki vipya ukuta Arsenal



HABARI UK. 30



## Mbappe ageuzwa kosa la Zidane Real

**MADRID,** Hispania

REAL Madrid itamshukuru Zinedine Zidane milele kwa kuiwezesha kupiga hatua baada ya kutwaa mikoba ya Rafa Benitez aliyevurunda, na zaidi kutwaa taji la Ligi ya Mabingwa Ulaya na ubingwa...

INAENDELEA UK 20



## Hazard? Mbona Messi amekubali

**MOSCOW,** Urusi

UFARANSA tayari imewatoa mabingwa wawili wa zamani wa Kombe la Dunia katika hatua ya mtoano, lakini bado ipo mbali kufikia ubora wake, kwa mujibu wa kocha wa timu hiyo, Didier...

INAENDELEA UK 19



## Canavaro: Taratibu Yanga itashangaza

**Na Faustine Feliciane**

NAHODHA wa Yanga, Nadir Haroub 'Canavaro', amekiri klabu yao inapitia wakati mgumu kiuchumi, lakini anaamini viongozi wa timu hiyo wanapambana kuirejesha kwenye mstari wake...

INAENDELEA UK 31

CHA PILI HICHO...



Dele Alli akiifungia England bao la pili kwenye mechi ya robo fainali ya Kombe la Dunia dhidi ya Sweden iliyopigwa katika Uwanja wa Samara, Urusi juzi na wao kutinga nusu fainali baada ya kushinda mabao 2-0. **HABARI UK. 29**

# KANE, MODRIC VITA ENGLAND V CROATIA

### Rekodi na heshima kusakwa Jumatano wakati Ufaransa, Ubelgiji zikilianzisha kesho...

**MOSCOW,** Urusi

STRAIKA Harry Kane amesisitiza England inajiamini itafika fainali ya Kombe la Dunia baada ya kuichapa Sweden na kutinga nusu fainali ya michuano hiyo inayofanyika Urusi mwaka huu, lakini Luka Modric amesema ni mwaka wao wa kuipiku rekodi Croatia iliyoiweka mwaka 1998 nchini Ufaransa.

England na Croatia zitakutana keshokutwa Jumatano katika mechi ya nusu fainali ya michuano hiyo baada ya kuzitoa Sweden na Urusi.

Bao la kichwa kutoka kwa Harry Maguire na lingine la Dele Alli yakifungwa katika kila kipindi yaliiwezesha England kushinda 2-0 katika mechi hiyo iliyopigwa Uwanja wa Samara Jumamosi.

Kane anayeongoza katika orodha ya utupiaji akiwa na mabao sita, hakuziona nyavu Jumamosi, lakini amekuwa nahodha wa kwanza England kuiongoza 'Three Lions' kutinga nusu fainali ya Kombe la Dunia tangu 1990.

"Tumejiandaa sana kwa mechi hii, na kurejea katika kiwango ukilinganisha na raundi iliyopita tulishinda kwa penalti [dhidi ya Colombia]," Kane aliiambia BBC Sport.

"Tulikuwa wazuri. Sweden walifanya mambo kuwa magumu, ilikuwa ni mechi ngumu. Mipira mirefu ambayo tumekabiliana nayo hadi sasa.

"Kuna mechi kubwa mbeleni. Tunajisikia vizuri, kujiamini. Tulimiliki mchezo."

Kwa upande wa Modric anaamini Croatia itavuna kitu kikubwa na kupiku mafanikio yao ya mwaka 1998, wakati ikicheza nusu fainali ya hiyo ya Kombe la Dunia kwa mara ya kwanza ndani ya miaka 20 kufuatia kuitoa Urusi kwa mikwaju ya penalti 4-3 katika hatua ya robo fainali juzi.

Ivan Rakitic alitupia penalti ya ushindi baada ya timu hizo kumaliza dakika 120 kwa matokeo ya sare ya mabao 2-2.

Croatia, ambayo ilimaliza nafasi ya tatu kwenye fainali za Kombe la Dunia Ufaransa miaka 20 iliyopita, sasa inataka kuweka historia mpya kwa kuanza kuitoa England keshokutwa.

"Hili linatufanya kujisikia fahari na furaha kuwa baada ya miaka 20, tumetinga nusu fainali ya Kombe la Dunia," alisema Modric, ambaye alitangazwa mchezaji bora wa mechi dhidi ya Urusi.

"Tumekuwa na safari ngumu. Hatukuwa na bahati kwenye michuano iliyopita. Sasa tunabeba deni kubwa mwaka huu. Tunatumai tutakwenda mbali zaidi kuliko mwaka 1998. Tunayo timu nzuri. Uongozi mzuri na kocha. Natumai tunaweza kupiga hatua ya ziada."

Alipoulizwa endapo anaweza kutoa ushindani katika kinyang'anyiro cha tuzo ya Mchezaji Bora wa Dunia ('Ballon d'Or'), kutokana na kiwango alichokionyesha na Croatia katika Kombe la Dunia, alisema: "Ukweli sifikirii kuhusu hili. Kitu cha muhimu ni timu ya Taifa kufanikiwa na kuvuna kitu kikubwa. Timu hii inaweza kufanya zaidi."

Nusu fainali ya kwanza itavurumishwa kesho kwa Ufaransa kuvaana na Ubelgiji baada ya timu hizo Ijumaa kuzitoa Uruguay na Brazil.

GAZETI HILI HUTOLEWA NA KUCHAPISHWA NA THE GUARDIAN LIMITED, S.L.P 31042

9 770856 541002